

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Nne – Tarehe 15 Mei, 2015

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe Anne S. Makinda) Alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kuanzia wiki iliyopita kulikuwa na Kilele cha Wiki ya Elimu Kitaifa na leo Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete atahutubia Taifa. Kwa maana hiyo basi, kwa asubuhi hii hakutakuwa na matangazo ya moja kwa moja ya TBC hapa Bungeni. Yatawekwa kwenye rekodi zao na baadaye zitachezwa kufuatana na muda utakavyopatikana; kwa hiyo, asubuhi hii tutakuwa tunajiona wenyewe hapa.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Deogratius Aloys Ntukamazina, atauliza swali hilo; naona kwa niaba yake ni Mheshimiwa Mwambalasa!

Na. 25

Shule za A-Level Wilayani Ngara

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA) aliuliza:-

Wilaya ya Ngara ina Shule za Serikali za A-Level tatu; Kabanga, Muyezi na Lukole High School, ambapo kabla ya Julai 2014 zilikuwa ni shule mbili tu zenye wanafunzi 450 zikiwa zinapewa shilingi milioni 32 kwa mwezi, lakini baada ya kuongezeka Muyezi High School wanafunzi wameongezeka kufikia 780 kuanzia Julai 2014 na kwa miezi sita Serikali imetoa shilingi milioni 48 tu wakati Wazabuni peke yao wanandai shilingi milioni 144 ili waweze kununua chakula:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha kwa ajili ya shule hizo tatu badala ya shule mbili?

(b) Je, ni lini Serikali itawalipa wazabuni kiasi cha shilingi milioni 144 wanachodai?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deogaratus Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2014/15, Serikali ilitenga shilingi bilioni 42.1 kwa ajili ya huduma za chakula cha wanafunzi wa shule za sekondari za bweni. Hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya shilingi bilioni 28.1 zilikuwa zimeshatolewa na Halmashauri ya Wilaya Ngara kupata shilingi milioni 171.3, kuwahudumia Wanafunzi wa Shule za Sekondari Kabanga, Lukole na Muyenzi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Januari hadi Aprili 2015, Serikali imetoa fedha kwa ajili ya chakula cha wanafunzi kuwezesha wazabuni wakiwemo Rulenge Traders Company na Muhsy and Asha Company Limited kulipwa sehemu kubwa ya madai yao. Serikali itaendelea kutoa fedha za chakula za kutosha kwa kila Halmashauri kulinagana na Bajeti iliyotengwa kwa mwaka husika hadi kufikia mwisho wa mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kwa juhudi kubwa anazofanya kufuatilia utoaji wa huduma kwa wanafunzi wa Wilaya yake. Aidha, Halmashauri zote nchini zinahimizwa kuwa na takwimu sahihi za wanafunzi wote wakiwemo wa bweni na kuziingiza kwenye Bajeti kwa ajili ya kutengewa fedha ipasavyo.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na pia ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri, lakini pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Mheshimiwa Ntukamazina alikuwa anasema toka Januari mpaka Aprili ni fedha ngapi zimepelekwa kwa ajili ya kuwalipa Wazabuni; lakini Mheshimiwa Waziri anasema ni fedha nyingi, hajasema ni fedha kiasi gani. Ninaomba aseme ni fedha kiasi gani zimepelekwa kwa ajili ya kuwalipa wazabuni?

(ii) Shule zilizoko Wilaya ya Ngara ni sawasawa na shule zilizoko Wilaya ya Chunya; kwa mfano, Sekondari ya High School ya Kiwanja na ya Maweni. Je, ni lini Serikali itakuwa inapeleka fedha za kutosha kuwalipa wazabuni kwa ajili ya huduma za wanafunzi hao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwambalasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni kweli limekuwa na kelele nyingi miezi miwili iliyopita, pale ambapo shule nyingi zilionekana kama zinataka kufungwa, kwa sababu ya kukosa fedha ya chakula. Suala hili halikuwa sahihi, kwa sababu Serikali imeendelea kutuma fedha kwenye maeneo yote na kuhakikisha shule za bweni zinapata fedha kwa ajili ya chakula cha wanafunzi wetu.

Kwa hiyo, suala hili la kwanza la kiasi gani kimepelekwa Ngara ili aweze kufahamu tumepeleka kiasi gani kule, kama ambavyo nimesema, kuanzia Julai 2014 mpaka Aprili 2015, jumla ya shilingi 171,330,000 zilishatumwa Wilayani Ngara kwa ajili ya kuhudumia shule zake tatu za bweni. Mchanganuo upo, kuanzia Julai na miezi yote, kila mwezi tumetuma fedha ambazo mwezi Julai 2014 shilingi milioni 15.1, mwezi Septemba 2014 tulituma shilingi milioni 30.2, mwezi Oktoba tulituma shilingi milioni 15.1, mwezi Novemba milioni 9.2 na mwezi Januari 2015 shilingi

milioni 15.1, Februari 2015 ni milioni 15.1, Machi 2015 milioni 15.3, Aprili 2015 jumla ya milioni 20. Fedha zote hizi ni kwa ajili ya Wilaya ya Ngara, kwa matumizi ya chakula kwa shule tatu zilizoko pale.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ambalo linataka kujua takwimu za utumaji wa fedha; kama ambavyo nimesema, nchi nzima kwa shule zetu za bwani, tumeshazitumia jumla ya shilingi bilioni 28.1 kwa ajili ya shule zilizoko kwenye Halmashauri zetu zile za bwani. Kuanzia Julai mpaka Machi, fedha iliyotumwa inatosha kabisa kila Halmashauri kupeleka shule na kulipa wazabuni hata kama si kwa asilimia 100, lakini kiasi cha kumuwezesha mzabuni kuendelea kutoa huduma bila kuwa na matatizo makubwa.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, tunaomba suala hili Serikali iwe *very serious*, ni tatizo kubwa sana. Kwa Mkoa wa Mara peke yake, wazabuni wanaosambaza vyakula mashuleni wanadai bilioni mbili madeni. Nimepata message kutoka Njombe na kutoka Mikoa mingine, watu wanaosambaza vyakula katika Taasisi za Serikali na Mashule hali yao ni mbaya. Wengine wamekopa benki wanashindwa kulipa na wamepata magonjwa ya moyo. Tunaomba Wabunge tunapouliza jambo hili ni jambo nyeti sana, wazabuni wanadai na wengine walifikia hatua ya kugoma.

Sasa je, ni lini Serikali mtapeleka pesa ikiwepo na Mkoa wa Mara? Ahsante.

SPIKA: Umesemea Mkoa wa Mara tu, Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bulaya, kama ifuatavyo:-

Kwanza, mimi ninataka kuwahakikishia wazabuni wote nchini ambao wanatoa huduma kwenye shule zetu za sekondari kwamba, madeni yao ambayo tayari wametuhudumia na hatujamudu kukamilisha yatakamilishwa. Ninataka niwahakikishie tu kwamba, kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2014/15, mwezi Julai 2014 mpaka leo hii, kila mwezi tumepeleka fedha kwenye Halmashauri zetu zote nchini kwa ajili ya kuwalipa wazabuni ili waendeleo kununua chakula kwenye shule zetu. Hakuna mwezi ambao hatujapeleka fedha; kwa mfano, mwezi Julai 2014 mpaka Oktoba, kila mwezi tumepeleka bilioni 3.5 nchi nzima. Mwezi Novemba tumepeleka bilioni 2.1, lakini mwezi Machi 2014 tumepeleka bilioni 8.4 nchi nzima, ambazo zinatoshia kila Halmashauri kupata mgao na kuweza kuwahudumia wazabuni wetu kuweza kupeleka chakula kwenye mashule.

Mheshimiwa Spika, ambacho ninataka niwahakikishie Mheshimiwa Wabunge, ninajua kama alivyoeleza Mheshimiwa Bulaya kwamba, jambo hili nisingependa litokee; ninataka kuwahakikishia haitatokea shule kufungwa kwa sababu ya ukosefu wa chakula. Kitu kilichotokea Kagera, Mkuu wa Shule alikuwa na hofu ya upungufu wa chakula, lakini siyo kukosekana kwa chakula moja kwa moja; na tayari mwezi uleule fedha ilikuwa imeshaingia Bukoba kwa ajili ya shule zao zote za bwani na kwenye Halmashauri ya Manispaa walishakuwa na mgao huo. Pale hakukuwa na mawasiliano kati ya Mkurugenzi wake na Mkuu wa Shule.

Ninataka nieleze katika hili, Mkuu wa Shule hana mamlaka ya kufunga shule bila kumconsult Mkurugenzi wa Halmashauri, kuona kama tatizo analompeleka kufunga shule kweli lipo. Mkuu wa Shule hana mamlaka hiyo, lazima atoe taarifa kwa Mkurugenzi na Mkurugenzi hawezi kufunga shule mpaka apate confirmation kwa Katibu Tawala wa Mkoa. Katibu Tawala

wa Mkoa atapata mawasiliano na Katibu Mkuu, ndiye atakayetoa kibali cha kufunga shule, kama kweli shule hiyo ina tatizo kubwa la chakula. (Makofi)

Kwa hiyo, ninatakata kuwahakikishia kuwa, huduma hizi tunaendelea kuzitoa na shule zetu ziendelee, watoto wetu watapa chakula kama ambavyo tumekubaliana.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo!

Na. 26

**Kutenga Asilimia Kumi ya Mikopo ya Vijana
na Wanawake**

MHE. DIANA M. CHILOLO aliuliza:-

Halmashauri nyingi nchini zimekuwa hazitengi ipasavyo asilimia kumi kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana kama ilivyo utaratibu wa Serikali kwa kila Halmashauri:-

(a) Je, ni Halmashauri ngapi hadi sasa zinadaiwa fedha hizo kwa ajili ya Mfuko wa Wanawake na Vijana?

(b) Je, Serikali inasemaje kuhusu Halmashauri ambazo hazitekelezi agizo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Wanawake na Vijana ulianzishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa mwaka 1993 kwa Azimio la Bunge kwa Mujibu wa *Ex-chequer* na *Audit Ordinance* ya Mwaka 1961. Lengo lilikuwa ni kuwawezesha akina mama na vijana kupata ajira binafsi na kushiriki kuchangia pato la kaya na jamii kwa ujumla kwa kupata mikopo yenye riba nafuu katika Halmashauri zao.

Halmashauri kutokana na mapato ya ndani hutenga 5% kwa ajili ya vijana na 5% nyingine kwa ajili ya wanawake. Utekelezaji wa Mfuko huu umekuwa ukikabiliwa na changamoto kubwa ya kutotengwa na kutorejeshwa kwa mikopo iliyotolewa kwa wanawake na vijana, hali ambayo husababisha lengo halisi la Mfuko huo kutofikiwa.

Katika kipindi cha mwaka 2010/15, takwimu zinaonyesha kuwa, Halmashauri zote zinadaiwa kwa viwango tofauti. Fedha zilizopaswa kupelekwa katika kipindi hiki ni shilingi bilioni 65.8, ambayo ni 10% ya fedha zilizokusanywa, lakini fedha zilizopokelewa ni jumla ya shilingi bilioni 6.2, ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 59.6.

(b) Mheshimiwa Spika, ninachukua fursa hii kuwakumbusha Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini, kuhakikisha wanapeleka fedha hizi za Mfuko wa Wanawake na Vijana kama ambavyo imeshaelekezwa kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri zao. Kwa zile Halmashauri ambazo zitaendelea kukiuka maagizo haya, Wakurugenzi wake watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Mamlaka iliyowateua.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri wazi kwamba karibu Halmashauri zote nchini zinadaiwa hazijatenga 10% kwa ajili ya akina mama na vijana; na kwa kuwa imekuwa mara zote Serikali ni kukumbusha tu; ni lini sasa Serikali itakuwa na mkakati wa makusudi kuhakikisha sasa hizi Halmashauri nchi nzima zinatenga fedha hizi ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Singida ambayo mpaka sasa ni miaka minne hazijatenga 10% kwa ajili ya vijana na akina mama?

(ii) Kwa kuwa 10% kwa ajili ya akina mama na vijana ni ndogo haitoshi, wanawake ni wengi na vijana ni wengi; wako ambao sasa wameanza kukopa kwenye mablenki yetu kama NMB, CRDB, NBC na Mablenki mengine; na kwa kuwa watu hawa sasa wanakabiliwa na kukosa dhamana ya kukopa huko; je, Serikali itakuwa tayari sasa kuzielekeza Halmashauri zote nchini kutenga viwanja kwa ajili ya vijana ili vijana waweze kupata dhamana ya kuanza kukopesheka kwenye mablenki ili kuondokana na tatizo hili la kusubiri 10% za Halmashauri?

SPIKA: Haya kwa hotuba yako; Mheshimiwa Naibu Waziri majibu! *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninajua hii ni *issue* na nimeona Wabunge wengi wamesimama. Labda kwa faida yao na kwa ajili ya mjadala huu tuweze kuelewana vizuri, baadaye tutajibu wakati tutakapokuwa *tuna-wind up*, Mheshimiwa Waziri wa Nchi atajibu ataeleza ni hatua gani tutazichukua, lakini nieleze kwa hapa.

Habari anayoizungumza Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo ni kweli. Mimi siwezi kulidanganya Bunge hapa, ninajua watatafuta katika takwimu wataona na ndiyo maana tumekiri hapa kwamba, ni *about 10%* tu ndiyo ambayo imepelekwa kule. Halmashauri hii anayoisema Manispaa ya Singida, milioni 554 ndizo walitakiwa kuwa wameshapeleka toka mwaka 2011 – 2015. Tukazungumza nao, hawakupoleka hata senti tano! Mimi siwezi kuliongopea Bunge hapa.

Nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji, nimemwita ofisini. Nimezungumza pia na Mweka Hazina, amekiri kwamba, walikuwa hawapeleki hela anasema mafungu yalikuwa ni kidogo, nikamwambia hayo mafungu kidogo, 5% yake kwa ajili ya wanawake na vijana.

Ninalisema hili ili tuweze kuelewana vizuri, tumekubaliana kuwa, hawa wote wanaozungumzwa kwa nchi nzima, lazima watulettee Mpango wa Halmashauri utakaonyesha jinsi watakavyofidia hiki kiasi ambacho hakikupolekwa.

Kwa upande wa Singida ambao ameulizia hapa, tumekubaliana na hili ninamwambia ili aende kufuatilia kwa sababu yeye ni Mbunge wa Singida na Manispaa ya Singida ni ya kwake; waweke milioni 250 kutoka kwenye *own source* zao kuanzia mwezi Julai. Kwa hiyo, hiki ndiyo kitakachofanyika hapa.

Sasa amezungumza zaidi ya hapo na ninataka tuelewane vizuri hapa, anauliza huoni kama kuna haja ya kuwagawia vijana viwanja ili viwanja vile sasa vitumike. Hili litakuwa ni habari ya Manispaa ya kule Singida, wao ndiyo watakaogawa. Anachozungumza hapa ni habari ya *collateral*. Sisi tunachozungumza, tunasema utaunda vikundi, utaunda SACCOS, SACCOS zile zikienda pale, ndizo ambazo zitawekwa rehani ili wao sasa waweze kukopa katika

Mabenki. Hii ni habari ya *political economy*, inakuonyesha *relations of production*, mahusiano ya uzalishaji mali yatakayoengeka pale.

Hakuna mtu atakayekwenda kumkopesha mtu mmoja mmoja, unamwuliza nyumbani kwako ni wapi, anamwambia pale msikitini ukikata utaona kanisa, ukiaenda pale utakuta kichuguu, chini yake kuna mfereji, hapo ndiyo kwangu.

Atakayetaka kukopesha anataka umwambie nani Mwenyekiti wa Kikundi, nani ni Katibu wake na nani ni Mweka Hazina wake. Ukimwuliza Mkurugenzi Mtendaji anakwambia naam kikundi hiki ninakifahamu kwa sababu kimesajiliwa. Huo ndiyo utaratibu unaoweza kuufanya katika nchi zote za Kijamaa na za Kibepari, wanaamini kwamba ushirika ndiyo njia pekee ya kuwasaidia watu wanyonge na hivyo ndiyo tutakavyofanya. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Mngodo, swali la nyongeza! Nilimwona, unajua wengine hawajauliza maswali ndiyo maana ninawapa nafasi. Mheshimiwa Mngodo nilimwona hakusimama? Haya Mheshimiwa Lwanji!

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, ninadhani hili suala ni la Singida zaidi.

Kwa kuwa hata pale ambapo Halmashauri zetu hutenga fungu kwa Mfuko huu wa Akina Mama na Vijana lakini uzoefu umeonyesha kwamba sehemu kubwa ya fedha hizi huenda kwenye SACCOS au Vikundi vilivyoko Makao Makuu ya Wilaya pale na kuviacha vikundi vilivyopo vijijini au katika tarafa.

Serikali inasemaje juu ya hili kuhakikisha mgao huu wa asilimia kumi kwa wanawake na watoto unakwenda hadi Vijijini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paul Lwanji, ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI na ambaye tumekuwa tunaongea naye, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, wakati mwingine kumekuwa na hili tatizo. Mimi ninaomba nieleze, huu utaratibu niliouelezea hapa watu wamecheka, lakini ndiyo utaratibu ambao tunautumia na utasaidia.

Pale katika Halmashauri kuna kitu kinachoitwa Idara ya Ujamaa na Ushirika, *Ujamaa and Cooperatives*, ndiyo unavyoitwa, jina lake ndiyo hilo. Kwa upande wa akina mama na vijana ambao tunawasaidia, kuna Idara ya Maendeleo ya Jamii, hawa ndiyo wanatengeneza kitu kinaitwa dunduliza, ndiyo ambao wanaleta ile *revolving fund* ambayo inatoka maendeleo ya jamii na kadhalika. Fedha hizi zote zinapokuja hapa zinakwenda katika Idara mbili hizo tunazozitungumzia hapa.

Ninachotaka kusema hapa, kama hela zote zinaonekana zinaishia pale Mjini, Halmashauri hii kupitia Idara ambazo nimeieleza hapa, ndizo ambazo zinatakiwa zi-*aportion* na kuhakikisha wananchi wote kwa maana ya vijana pamoja na wanawake, waliokuwa katika Wilaya ya Singida yote kwa ujumla wake, wanapata hizi fedha tunazozitungumzia hapa.

Kwa hiyo, ni suala la kuangalia records zao, lakini hawatatoa hizi hela kama hawatakuwa wamefuata huu utaratibu tunaouzungumza hapa. Wapo wengine wamewapelekea laki mbili, laki tano, hazitasaidia kitu chochote. Wakiweka katika makundi haya, wakaweka na orodha wakafahamika, ataangalia kama wa mjini wamepata na wale wa vijijini wapate. Sasa katika Manispaa atakuwa anamaanisha Manispaa ya Singida, lakini anazungumza habari ya Manyoni, Manyoni maana yake aangalie mpaka vijijini.

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opolukwa, atauliza swali hilo.

Na. 27

Kupeleka Umeme Kata za Jimbo la Meatu

MHE. MESHACK J. OPULUKWA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Jimbo la Meatu za Mwanjolo, Bukundi, Imalaseko, Mwamanongu, Mwamanimba, Nkoma na Mwamalole?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meshack J. Opolukwa, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Meatu ina jumla ya Miradi saba inayoendelea kutekelezwa katika Mpango wa REA Awamu ya Pili. Vijiji vinavyonufaika na Miradi hii ni Kabondo, Buliyashi, Mwambiti, Manyahina, Bulyanaga, Mwambwega na Nkoma. Miradi hiyo inatekelezwa na Mkandarasi aitwaye *M/S LTL Projects Limited*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Miradi hii katika Wilaya ya Meatu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 umbali wa kilomita 58.4; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 umbali wa kilomita 22; ufungaji wa transfoma 12 na kuwaunganisha wateja wa awali wapatao 435. Gharama za kukamilika kwa Miradi yote inayofadhiliwa na REA Awamu ya Pili katika Mkoa wa Simiyu ni shilingi bilioni 21.5.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa kazi kwa Wilaya ya Meatu umefikia asilimia 50, ambapo kazi za kusimika nguzo kwa njia ya umeme wa kilovoti 33 imekamilika kwa asilimia mia moja; kazi ya kusimika nguzo za njia ya umeme wa kilovoti 0.4 imekamilika kwa asilimia 21; na uvutaji wa nyaya kwa njia ya kilovoti 33 umefikia asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingine vya Kata za Mwanjolo, Bukundi, Imalaseko, Mwamanongu, Mwamanimba na Mwamalole, havipo katika mchakato wa utekelezaji wa REA Awamu ya Pili ila vinafanyiwa makisio na vitawekwa katika Awamu ya Tatu, inayotarajia kuanza Mwaka wa Fedha wa 2015/16.

SPIKA: Mheshimiwa Opolukwa swali la nyongeza!

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa katika majibu ya Waziri amesema vijiji ambavyo nimevitaja vinafanyiwa makisio na vitaingizwa kwenye utekelezaji wa Mwaka wa Fedha 2015/16; na kwa

kuwa sasa hivi tupo katika bajeti za Wizara mbalimbali ina maana na makisio mengi yamekwishafanyika. Je, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba vijiji hivi vitaingizwa kwenye utekelezaji wa mwaka 2015/16 badala ya 2016/17 kwa sababu tayari bajeti tunaindaa hivi sasa na mambo mengi yamekwishafanyika?

(ii) Jimbo zima la Meatu lina vijiji 57 na vinavyopata umeme ni vijiji vitano tu kwa Jimbo zima la Meatu. Tunaposema mazingira magumu ni pamoja na wananchi kutokuwa na umeme wa uhakika. Je, Serikali ipo tayari sasa kutoa kipaumbele kwa Meatu ili angalau kuweza kuondokana na haya mazingira mgumu kwa watumishi na watu mbalimbali kuweza kuvipa kipaumbele vijiji hivi viweze kupata umeme kwa haraka zaidi?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri majibu!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Opolukwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika bajeti ya mwaka 2015/16 ambayo tutaipitisha, tutakuwa na *package* ambayo inatekeleza baadhi ya vijiji. Kama nilivyosema, tumepanga hivyo kwa sababu upatikanaji wa fedha ya REA hauingiliani, pamoja na kwamba zinatengwa katika bajeti lakini kadiri fedha zinavyozidi kupatikana kutokana na vyanzo vinavyofahamika vya Mfuko wa REA, tunaendelea kutekeleza Miradi zaidi. Ndiyo maana utaona katika vijiji tulivyokuwa tumevipitisha kwa mwaka 2014/15, bado kuna baadhi ya maeneo tumeongeza kutokana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, nipende kusema tu kwamba, siyo rahisi kabisa kuweza kupeleka umeme vijijini kwa nchi nzima kwa mara moja. Lazima tutakwenda kwa awamu na hivi tunaandaa Awamu ya Tatu, ambayo itaanza mwaka huu wa fedha kwa sababu ile Awamu ya Pili inaisha mwezi Julai 2015.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, katika vijiji 57 vya Meatu, ni vijiji vitano tu ndiyo vyenye umeme, lakini vipotevya vinatekelezwa sasa. Ninaamini Mheshimiwa Mbunge katika hivi ambavyo anavipendekeza alivyovitaja hapa, kama anavyoviwekea kipaumbele na sisi tutajaribu kuviwekea kipaumbele, kwa hiyo, havitakuwa idadi ya vitano tena, tutaendelea na baadaye awamu nyingine inavyokwenda tutazidi kumaliza na hivyo ambavyo vimebakia. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Deo Sanga!

MHE. DEO K. SENGGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza. Swali ambalo limeulizwa Wilayani Njombe linafanana kabisa Jimbo la Njombe Kusini kwako Spika na Jimbo la Njombe Kaskazini.

Namshukuru Naibu Waziri wa Nishati na Madini, hivi karibuni alipokuja Njombe, tulitembelea Njombe Kusini na Njombe Kaskazini. Kwa kuwa Mradi huu wa REA, Njombe Kusini na Njombe Kaskazini hatujaupata kuna Mradi mkubwa wa kutoka Makambako kwenda Songea na ndiyo tupo kwenye Mradi huo. Tuna maombi maalum ambayo tumeomba Njombe Kusini Kata ya Kobi, Kifanya na baadhi ya vijiji na Njombe Kaskazini, Kata ya Mlowa na Kata ya Utengule ambapo kijiji kimoja kinachopakana pale, Kijiji cha Mawande na Kijiji cha Mlowa.

Waziri anatuambia nini; walituhidi katika Majimbo haya vijiji hivi ambavyo tumeomba rasmi kwamba tunaomba na sisi tupatiwe umeme katika awamu hii wanayoendelea nayo na aliahidi? Naomba atamke hapa ili wananchi kule wasikie kama ambavyo aliahidi; ni lini sasa na sisi tutapata umeme katika Mpango huu wa Awamu ya Pili?

SPIKA: Kule Njombe Kusini Waziri ana barua toka alipokuwa Naibu Waziri mpaka sasa Waziri. Anayo barua na vijiji anavyo. (Kicheko)

Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kutoka Makambako, Njombe kuelekea hadi Songea, watanufaika na Mradi wa Makambako Songea, ambao pamoja na usafirishaji wa umeme wa njia kubwa, lakini pia Mradi huu unahusisha uteremshaji wa umeme kwenye vijiji ambavyo utapita. Hata hivyo, nakumbuka kutoka kwako wewe mwenyewe juu ya ombi la Miradi ya REA katika vijiji kadhaa ambavyo kama alivyovitaja Mheshimiwa Deo Sanga katika Kata ya Kobi, Kifanya na kwake kule Mlowa na Utengule.

Mheshimiwa Spika, tutajitahidi kuona ni namna gani tunaweza kufanya, lakini *the only option* tuliyonayo sasa ni kuunganisha kutoka kwenye bajeti hii ambayo tutaianza kwa Mwaka wa Fedha unaokuja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tatizo tulilionalo ni muda. Hapa tumejibu maswali matatu tu na zimeshapita dakika kumi. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli aulize swali linalofuata.

Na. 28

Tatizo la Kukatika Umeme Mara kwa Mara

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI aliuliza:-

Hivi karibuni kumekuwa na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika Wilaya ya Rufiji:-

Je, Serikali imeshughulikia tatizo hilo kwa kiasi gani?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la umeme lililoikumba Wilaya ya Rufiji hivi karibuni limetokana na zoezi la kuifanyia matengenezo makubwa mitambo ya kufua umeme kwenye Kituo cha Somanga. Zoezi hili tayari limekamilika.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine inayosababisha umeme kukatika mara kwa mara ni uharibifu wa miundombinu ulioanza kujitokeza kwenye njia ya umeme ya kuelekea Nyamisati, pamoja na uwepo wa komba wengi kwenye maeneo hayo, wanaoleta shoti kwenye laini za umeme. TANESCO Mkoa wa Pwani wameandaa mipango ya kutembelea maeneo yaliyopitiwa na njia ya umeme kuelekea Nyamisati ili kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya kuharibu miundombinu ya umeme.

SPIKA: Mheshimiwa Kuruthum maswali ya nyongeza!

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, tunaishukuru Serikali kwa kuwa suala hilo wamelifanyia kazi na sasa kidogo hali imetulia, watu wanapata umeme na huduma inaendelea kama kawaida.

Maswali yangu mawili madogo ya nyongeza ni yafuatayo:-

Mheshimiwa Waziri kumekuwa na malalamiko mengi kwa wateja wa umeme Wilayani Rufiji, ambao wanatumia zile mita za luku. Wengine wanawekewa luku za matumizi ya viwanda na siyo kwenye majumba, kwa hiyo, wanapata tabu katika bila zao. Luku inapoharibika pia ikija kutengenezwa hata kama ulikuwa na *units* zako hamsini au mia moja, zinakuwa zimepotea na wanapozidai hawarudishiwi tena.

(i) Je, tatizo hili linaweza likaondolewa namna gani?

(ii) Katika Mradi wa REA mliahidi Wananchi wa Kata ya Chumbi, Nambunji, Mbwala, Mkongo mpaka Mloka kwamba, watapata umeme katika awamu hii lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua sana. Je, Mheshimiwa Waziri anawaeleza nini Wakazi wa Rufiji ambao wanasubiri umeme kwa ajili ya maendeleo?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kuwaomba radhi wateja mbalimbali wa TANESCO, ambao walipata kadhia ya kushindwa kununua umeme vizuri kupitia mitandao ya simu wiki mbili zilizopita.

Mheshimiwa Spika, mita za luku kwa sasa zote kwa wanaotaka kununua umeme, umeme unanunulika vizuri na hakuna tatizo tena na lile tatizo limekwisha. Sasa upo usumbufu ambao unatokana na wateja hasa wa kawaida, kutoridhika na gharama wanazozilipia kwa umeme wanaonunua kupitia luku.

Mheshimiwa Spika, pengine unapotokea usumbufu wa uharibifu wowote ule katika matengenezo yake panatokea usumbufu wa *units* zile kupotea kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Nichukue nafasi hii kuwaomba sana, kwa wale wote ambao wamekumbwa na matatizo haya, kwa sababu matatizo ya kimtandao ni ya kawaida, tunanunua vocha za simu nadhani tunajua, ni sawasawa na hiki kinachofanyika hapa; basi walete malalamiko yao na kuonyesha vielelezo au ushahidi. Nawaagiza TANESCO kuhakikisha Wilaya zote na vituo vyote wanawahudumia wateja hawa bila kupoteza fedha zao kupitia kwenye *units* ambazo zinapotea. Vilevile wasiwawekee mita au *grade* ambazo ni za kibiashara wakati ni makazi au za viwanda wakati ni biashara ndogo. Hii inaleta usumbufu na ni kweli nikiri kwamba, baadhi ya maeneo hilo linatokea.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba, REA kulikuwa na Mradi wa Rufiji Kata ya Chumbi, Nambunji, Mbwala, utekelezaji unaendelea na wakati wowote wananchi wataona shughuli zikiwa zinaendelea, kwa sababu kadiri tunavyopata fedha ndivyo tunavyozidi kutekeleza miradi hii. Miradi hii ni mingi na ipo kwa nchi nzima.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Desderius John Mipata atauliza swali!

Na. 29

Hitaji la Mawasiliano ya Simu Nkasi

MHE. DESDERIUS J. MIPATA aliuliza:-

Vijiji vilivyoko kwenye Kata ya Kate na vile vilivyoko Kata ya Isale havina mawasiliano ya simu ya kuaminika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia vijiji hivyo vyote mawasiliano ya uhakika?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata za Kate na Kisale katika Wilaya ya Nkasi Mkoani Rukwa, zimejumuishwa katika Mradi wa Mawasiliano Vijijini Awamu ya Pili (Phase 2A), unaosimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (Universal Communication Services Access Fund), ambapo Kampuni ya Mawasiliano ya Mic ya TIGO, imeshinda zabuni ya kupeleka mawasiliano katika Kata hizo.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 21 Januari, 2016.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mipata, swali la nyongeza!

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Umuhimu wa mawasiliano ni mkubwa kiuchumi na kijamii na kwamba maeneo ambayo yanakosa huduma hii hayana ushindani kabisa kimaendeleo na maeneo yenye huduma hii. Kata ya Ninde, Wampembe na Kala hazina kabisa huduma hii. Nimetumia muda mwingi sana katika Ubunge wangu kuzielezea. Mheshimiwa Waziri, wamekuwa kila mara wanaahidi na kunipa nyaraka mbalimbali ambazo ninapeleka pia kwa wananchi kuwahakikishia kwamba watapata huduma hiyo na sasa ni hukumu kwangu.

Nataka leo wawaambie wananchi hawa nini kilichotokea; ni mimi nilizembea au wao ndiyo wamechelewa kwenda kupeleka mawasiliano? Na hii ni kwa Wabunge wote.

(ii) Kwa kuwa sasa hivi Kampuni ya Vietel inashughulika sana kupeleka mawasiliano sehemu mbalimbali vijijini; na kwa kuwa Kampuni hii katika maeneo ya kwangu naona badala ya kwenda kwenye changamoto ambazo mawasiliano hasa yanatakiwa bado wanaendelea kupeleka mawasiliano sehemu ambazo hazina shida kubwa ya mawasiliano. Mkataba wa Serikali ukoje ili watu waelewe? (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba niwahakikishie Wananchi wa Nkasi Kusini kwamba, Mbunge wao hakuzembea na wala Serikali haikuzembea. Naomba niwaambie kwamba, Mheshimiwa Mbunge Mipata anafanya kazi vizuri

na katika Sekta ya Mawasiliano amewawakilisha vizuri sana Wananchi wa Jimbo lake la Nkasi Kusini.

Mheshimiwa Spika, nasema Serikali haikuzembea kwa sababu Serikali kama Serikali haipeleki mawasiliano vijijini moja kwa moja ila inafanya kazi na makampuni ya simu. Makampuni haya yana bajeti zake pia, hayawezi kwenda nchi nzima kwa mara moja, yanakwenda hatua kwa hatua. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na aende kuwaeleza wananchi kwamba, Kata za Ninde, Kala na Wampembe alizozitaja, zimejumuishwa kwenye Mpango wa Vietel; yaani Kampuni Vietel kutoka Vietnam ambayo inapeleka mawasiliano vijijini, itapeleka pia mawasiliano katika Kata hizo alizozitaja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu kwamba Vietel inafanya nini; naomba nimhakikishie kwamba, mpaka hivi sasa tumeshavitambua vijiji karibu 4,000 nchini kote, ambavyo Kampuni ya Vietel itapeleka mawasiliano na itapeleka mawasiliano hayo katika awamu tatu. Awamu ya kwanza, ambayo imeanza Oktoba 2014 mpaka Oktoba mwaka 2015 na awamu nyingine itaanza Oktoba 2015 mpaka Oktoba 2016 na nyingine itaanza Oktoba 2016 mpaka 2017 Novemba. Kwa hiyo, Serikali imejipanga vizuri sana kuhakikisha Makampuni haya ya Simu pamoja na Vietel, inapeleka mawasiliano nchini kote na hasa yale maeneo ya mipakani ambayo pia siyo ya kibiashara, tunatumia sana Mfuko ule wa UCAF kama nilivyosema, kuhakikisha maeneo haya yote yanaweza yakapata mawasiliano ya Makampuni ya Simu.

SPIKA: Hotuba ya Wizara itakuja hapa, sasa ninaenda Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma atauliza swali hilo!

Na. 30

Tatizo la Watoto wa Mitaani

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA aliuliza:-

Ni haki ya mtoto kupata makuzi na malezi mazuri kutokana na hali iliyopo sasa:-

(a) Je, ni lini tatizo la watoto wa mitaani wanaopata tabu katika maisha yao litakwisha?

(b) Je, ni mkakati gani uliopo kwa sasa wa kukomesha tatizo hili la watoto wa mitaani?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, kuhusu tatizo la watoto wa mitaani, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ya motto, imekuwa ikifanya jitihada kubwa kukabiliana na tatizo la watoto wa mitaani hapa nchini ili kupata suluhisho la kudumu la tatizo hili. Jitihada hizo ni pamoja na kutunga na kutekeleza Sera, Sheria, Mikakati na Mipango mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kushughulikia tatizo hili ili kupata ufumbuzi wa kudumu, unajikita zaidi katika uimarishaji wa mifumo ya kijamii inayoambatana na mabadiliko ya kifikra kwa jamii, mambo ambayo Serikali imekuwa ikiyafanya kwa muda mrefu.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, TAMISEMI, ambao ndiyo wenye watoto na wadau wengine wa maendeleo ya motto, tumeandaa na kutekeleza Mkakati na Mipango mbalimbali ya kukabiliana na tatizo hili. Kwa mfano, Mpango Kazi wa Jamii wa Kudhibiti Tatizo la Watoto Wanaoishi Kufanya Kazi Mitaani wa Mwaka 2014 hadi 2017 na Mpango Kazi wa Pili wa Taifa wa Huduma kwa Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Hatarishi wa Mwaka 2013 hadi 2017. Jana tarehe 14 Mei, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, amezindua zana za mawasiliano za kuzuia ukatili dhidi ya watoto Tanzania katika Ukumbi wa Dodoma Hotel Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mipango hii umejikita zaidi katika kuweka na kuimarisha mifumo iliyopo ya malezi, matunzo na ulinzi kwa watoto katika ngazi za Taifa na Serikali za Mitaa. Pamoja na kuimarisha mifumo ya utoaji huduma, mkazo mkubwa umewekwa katika kujenga uwezo wa kiuchumi wa familia na kaya ili ziweze kujitegemea na kutoa huduma bora na endelevu kwa watoto wao. Mfano, utekelezaji wa masuala ya *TASAF III*, Mikopo kupitia Benki ya Wanawake, Mifuko ya Maendeleo ya Wanawake na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwarejesha watoto hao katika familia zao. Pia ili kupata ufumbuzi wa kudumu, Serikali imeandaa utaratibu wa kukusanya takwimu za watoto katika ngazi za kijiji, mitaa, kwa kuwatumia Maafisa Maendeleo na Ustawi wa Jamii na ikiwa mtoto ataacha kwenda shule au kutoonekana kijijini hapo, inabidi mzazi au Mwalimu Mkuu atoe taarifa kwa uongozi ili mtoto huyo aweze kufuatiliwa na kufahamika alipo.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa Mipango hii yote ikitekelezwa kikamilifu, tatizo la watoto wa mitaani litakwisha.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, swali la nyongeza!

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(i) Tatizo hili limekuwa kubwa sana hasa kwenye Miji mikubwa na limekuwepo kwa muda mrefu. Je, kwa nini usiwepo mpango ambao ni endelevu wa kuwarudisha watoto hawa wa mitaani majumbani kwao, kwa wazazi wao au kwa ndugu zao mara tu tatizo linapotokea?

(ii) Kwa wale watoto ambao hawana wazazi au ndugu zao kwa nini usiwepo mpango wa kuwarudisha na kuwapeleka kwenye vituo vinavyohudumia hawa watoto wa mitaani?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSI NA WATOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niungane na Dkt. Ishengoma kwamba, tatizo hili lipo katika miji mikubwa. Utafiti uliofanyika hivi karibuni, ulibaini zaidi ya watoto 5,000 kwa wastani wa watoto sitini katika kila Kata, wanaishi na kufanya kazi mitaani na sehemu kubwa ya watoto hawa wapo katika miji kama Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, tunayo mipango thabiti kabisa ya kuhakikisha watoto hawa ambao wanakwenda mitaani wanarudishwa makwao. Mipango hii endelevu ipo katika Halmashauri zetu na ninaomba nitoe mfano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ambako

nimefanya ziara hivi karibuni na niliwasiliana na RAS wa Dar es Salaam, ambako alituthibitisha mipango hiyo katika Halmashauri ya kuchukua takwimu na kuwarudisha makwao.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo wakati mwingine wanaporudishwa makwao, wanarudi tena wale wale au wanarudi wengine Dar es Salaam wakiamini kwamba wanapoombaomba wanapata chochote, lakini mipango ipo. Mipango mingine ni kuhakikisha ada zinafutwa katika shule za msingi. Kuna mpango wa kuimarisha kaya maskini, masuala la *TASAF*, ada zinapofutwa maana yake tunatarajia watoto hawa wasiwe mitaani wawe madarasani, kuliko kuwa mitaani. Kwa hiyo, mipango hiyo endelevu ipo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, vivyo hivyo kwa wale watoto ambao hawana wazazi, tunavyo vituo. Nichukue nafasi hii kupongeza sana Sekta Binafsi, NGOs na Mashirika na Dini, ambayo huchukua watoto hawa inapoonekana hawana wazazi. Kwa maeneo kama Dar es Salaam tuna Kituo cha Watoto Kurasini, SOS, Dogodogo Center na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana mwuliza swali kwa kujali haki za watoto nchini na nimthibitishie kwamba mipango hiyo endelevu ipo.

SPIKA: Haya subirini Wizara yake itakapokuja, maana muda wangu umeisha. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, aulize swali hilo!

Na. 31

Utoaji wa Hati Miliki za Kimila

MHE. MOZ A. SAIDY aliuliza:-

Serikali ilianzisha mpango wa utoaji wa Hati Miliki za Kimila kwa madhumuni ya kuwanufaisha wananchi wa vijijini kupata mikopo:-

(a) Je, utaratibu huu umefikia wapi?

(b) Je, ni lini Mikoa mingine kama Dodoma itanufaika na mpango huu kwa kuwa Mikoa mingine imeshaanza kutekeleza utoaji wa Hati Miliki za Kimila?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2001. Utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila ulianza mwaka 2004 Wilayani Mbozi na baadaye uliendelea katika Wilaya zingine, ambapo hadi Machi 2015, takribani Hati za Hakimiliki ya Kimila 349,000 zimekwishatolewa kwa wananchi. Hati ya Hakimiliki ya Kimila si tu humwezesha mwananchi kuweza kuitumia kama dhamana ya mkopo, bali inahakikisha usalama wa miliki ya mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu au taasisi. *(Makofi)*

Kwa upande mwingine, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali, imeweza kutekeleza Miradi ya Mfano ya Utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila katika Wilaya ya Mbozi, Namtumbo, Manyoni, Babati na Bariadi. Hivyo basi, kila Halmashauri ya Wilaya inatakiwa kutekeleza Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999 kwa kutoa Hati za Hakimiliki ya Kimila kwa wananchi vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, mikoa yote nchini inaendelea na utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999 kwa kutoa Hati za Hakimiliki ya Kimila katika Halmashauri zilizo katika Mikoa yao. Aidha, kwa Mkoa wa Dodoma, utoaji wa Hati za Hakimiliki ya Kimila unaendelea katika Vijiji vya Halmashauri za Wilaya ya Kongwa, Mpwapwa, Bahi na Kondo kuanzia mwaka 2009 hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, ninaziagiza Halmashauri zote nchini, kutenga fedha katika bajeti zao ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999 na kutoa Hati za Hakimiliki ya Kimila kwa wananchi.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa makusanyo ya Halmashauri za Wilaya zetu nchini hayatoshi kufanya kazi hiyo; na kwa kuwa Serikali Kuu haileti ruzuku kwa mtiririko; je, Serikali ina mpango gani mbadala wa utekelezaji wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya Mwaka 1999?

(ii) Kwa kuwa Halmashauri kuna makusanyo ya kodi ya ardhi; na kwa kuwa Serikali Kuu mnachukua fedha hizo hamrudishi asilimia inayotakiwa; hamwoni sasa ni wakati mwafaka kuwaachia Halmashauri waondoe asilimia zao kwanza ndipo na ninyi mchukue za kwenu?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, kuhusiana na Serikali ina mpango gani mbadala wa kuziwezesha Halmashauri zetu ili ziweze kufanya kazi hii ya utoaji wa hati za kimila.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia gharama yenyewe tu kwanza, mwananchi ni lazima achangie na ni gharama ndogo sana. Ukiikokotoa katika suala zima la usajili kwa mujibu wa Kanuni ya 81 katika Jedwali la Pili la Sheria ya Ardhi ya Vijiji ni shilingi 2,750. Vilevile kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Vijijini, imeziachia Halmashauri husika za vijiji kuweza kujipangia kiasi cha tozo ambacho zinaona kinafaa kwa ajili ya kuwezesha shughuli hii maalum.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia sisi kama Serikali kwenye Miradi ya Mifano ambayo tulikuwa tukiitekeleza, sehemu kubwa ya gharama tulikuwa tukizigharamia, lakini bado ukiangalia kwa vijiji vilivyo vingi itakuwa ni ngumu kwa Serikali yenyewe kuachia hivi hivi bila mwananchi kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia gharama za Halmashauri bado siyo nyingi hivyo, kimsingi, sisi tungependa wao wajikite zaidi katika kuhakikisha kunakuwa na Watendaji wa kutosha wa Ardhi, kujikita katika ujenzi wa masjala za ardhi na vilevile kujikita katika kuziwezesha Kamati za Maamuzi, ambazo ndiyo zitaangalia masilahi mbalimbali ya mipaka ili waweze kufanya jukumu hili la kuweza kuwezesha utoaji wa hati miliki za kimila.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu rai kwa Halmashauri zetu kuhakikisha kwamba, zinawezesha Halmashauri za Vijiji. Vilevile nitoe rai kwa wananchi wetu wachangie, kwani watakapokuwa na usalama wa miliki itaweza kuwasaidia kuitumia katika matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika suala la pili kuhusiana na makusanyo ya kodi ya ardhi kuiachia asilimia 30 Halmashauri. Kwanza, suala hili tumekuwa tukilitekeleza vizuri sana, lakini kuna maamuzi ya kisera ambayo tunayafanyia kazi na baadaye wakati wa bajeti yetu tutaweza kuangalia ni jambo gani tutaweza kulitekeleza. Kwa hivi sasa makusanyo haya hatuwezi kuyaacha moja kwa moja kwanza tunapotekeleza, kwa sababu ni lazima watuletee return Wizara ya Ardhi, tuone ni kwa namna gani walikusanya kodi hii ya ardhi ndipo baadaye inaweza kurudishwa, lakini tumekuwa tukirudisha katika Halmashauri zote ambazo zimekuwa zikikusanya tozo hii.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

SPIKA: Ahsante. Twende Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ignas Malocha!

Na. 32

Jengo kwa Ajili ya Mahakama ya Mwanzo - Mtowisa

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Majengo ya Mahakama ya Mwanzo iliyoko Tarafa ya Mtowisa, Kijiji cha Mtowisa ni ya muda mrefu sana toka enzi za Mkoloni, yamechakaa sana na yanavuja; hali inayohatarisha maisha ya wananchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga jengo jipya ili kunusuru ajali inayoweza kutokea?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Sika, Mahakama inatekeleza mpango wa kujenga na kukarabati majengo ya Mahakama nchini kulingana na upatikanaji wa fedha ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Mahakama ilipanga kujenga Mahakama ya Mwanzo iliyopo Tarafa ya Mtowisa. Hata hivyo, Mradi huu haujatekelezwa kutokana na ukosefu wa fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2015/16, Mahakama itaendelea kutekeleza Mpango wa Kujenga na Kukarabati Majengo ya Mahakama nchini, ikiwemo Mahakama ya Mwanzo ya Tarafa ya Mtowisa.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, tatizo la ubovu wa Jengo la Mahakama ya mwanzo Mtowisa ni kubwa sana, tofauti na ambavyo Serikali inavyolitazama.

(i) Je, kwa nini Serikali isilione kwamba ni suala la dharura ikaweka mkakati wa kuliboresha hilo jengo ili kuzuia maafa yanayoweza kujitokeza baadaye?

(ii) Mahakama hiyo ni tegemeo la watu wengi takribani Kata saba na watu zaidi ya laki moja na nusu, lakini inalo tatizo kubwa la upungufu wa Watumishi, ina Hakimu mmoja, kiasi kwamba inasababisha msongamano wa kesi na kesi nyingi kuahirishwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Hakimu mwingine katika Mahakama hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niweke wazi kwamba, Serikali tunatambua umuhimu wa Mahakama kama Mhimili wenye dhamana ya kutoa haki katika nchi yetu na dhamira yetu hii inaonekana katika ongezeko la bajeti ya Mahakama mwaka hadi mwaka. Tumetoka kwenye bajeti ya bilioni mia moja, sasa hivi tunazungumzia bajeti ya zaidi ya bilioni mia moja sitini na sita.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba, katika mwaka huu wa fedha ambao unamalizika Juni, hatukuweza kupata fedha katika bajeti ya maendeleo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametuahidi kabla ya tarehe 30 Juni, angalau watatoa hata asilimia 30 ya Bajeti ya *Development* kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya Mahakama ya Tanzania. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Malocha, naomba niahidi, *commitment*, tutakapopata fedha yoyote katika *Development Budget* kabla ya kumaliza mwaka huu, basi Mahakama ya Tarafa ya Mtasiwa tutaipa kipaumbele kwa sababu kama ulivyosema, hali yake ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumeweka pia mpango wa kukarabati Mahakama zaidi ya 165 na kujenga Mahakama mpya zaidi ya 100 katika mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Spika, swali la pili suala la upungufu wa Watumishi, nikiri kwamba, tumefanya jitihada mbalimbali za kukabiliana na upungufu wa Watumishi katika Mahakama. Nitaenda kuangalia kumbukumbu zetu ni kwa nini Mahakama ya Tarafa ya Mtowisa haikupata Watumishi. Tangu Bunge lako lilipopitisha Sheria ya *Judicial Administration Act* ya kuwa na Mahakimu na kuwa na Watendaji wa Mahakama, tumeweza kutatua tatizo la watumishi kwa kiasi kikubwa. Mheshimiwa Mbunge, nitakuthibitishia kwamba, tutataua tatizo hili la Mahakama ya Mtowisa na ninaamini unasema kweli kwamba haina Watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Makazi na Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Ikungi ni chakavu kwani lilijengwa tangu wakati wa ukoloni na Ikungi sasa ni Wilaya. Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha makazi na Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Ikungi ili lifae sasa kama Mahakama ya Wilaya badala ya kuendelea kutumia jengo ambalo lilijengwa tangu ukoloni? *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Christina Mughwai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia kwamba, katika mwaka huu wa fedha ambao unamalizika Juni 2015, katika mpango wetu zipo Mahakama za Wilaya zaidi ya 43, ambazo

hazikuweza kufanyiwa ukarabati. Kwa hiyo, ninachoweza kumuahidi Mheshimiwa Lissu, katika Mpango wa Ukarabati wa Miundombinu ya Mahakama wa Mwaka 2015/2016, basi tutaweza kuhakikisha Majengo ya Mahakama ya Wilaya ya Ikungi nayo yanaingia katika mpango wa ujenzi. Kwa hiyo, tutakapoleta bajeti yetu wiki ijayo, nitaomba uipitishie kwa nguvu zote na asilimia zote, ili kuhakikisha tunaboresha miundombinu ya Mahakama ya Wilaya ya Ikungi, ili iweze kufanya kazi yake kikamilifu ya kutoa haki.

Na. 33

Kutumia Ardhi kwa Ajili ya Kumaliza Tatizo la Ajira

MHE. AMINA M. MWIDAU aliuliza:-

Suala la ajira hapa nchini ni tatizo kubwa sana kwa sasa na katika nchi yetu Mungu ametujalia kuwa na ardhi kubwa na yenye hali ya hewa nzuri:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia ardhi tuliyonayo kimkakati, ili kukwamua tatizo hili la ajira lililopo nchini?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kilimo ndiyo sekta muhimu inayoweza kuajiri vijana wengi nchini, ndiyo maana juhudi kubwa imeelekezwa katika kukuza kilimo. Katika kutekeleza Sera ya Kilimo ya Taifa, Serikali imelenga kujenga mazingira wezeshi, ili kukuza uzalishaji na hatimaye kupunguza umaskini nchini. Jitihada mbalimbali za kuboresha na kuongeza uzalishaji katika kilimo zinafanyika, ili kuwezesha vijana wengi kujijiri kwenye sekta hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali imeanza kutekeleza Mradi mkubwa wa miaka mitano wa kuwezesha vijana, unaolenga kukuza uzalishaji katika kilimo na kuongeza kipato cha vijana waishio vijijini. Mradi unajulikana kama *Empowering Youth in Agricultural Investment Through Establishment of Village Agricultural Youth Clubs (A Pathway Towards Economic Liberalization for Rural Youth in Tanzania)*. Mradi unatarajiwa kuunganisha vijana na mabweni, ili waweze kukopeshwa kwa urahisi na kuimarisha usindikaji mazao ili kuongeza thamani ya mazao.

Pili, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na Wadau wengine, inatekeleza mkakati mkubwa wa kuleta Mapinduzi Makubwa ya Kilimo (KILIMO KWANZA) na imeainisha maeneo kumi ya utekelezaji ambayo yameongeza kasi ya uwekezaji binafsi kwa vijana katika uzalishaji na usindikaji mazao (*10 Pillars*).

Tatu, Serikali kupitia Halmashauri nchini imetenga maeneo kwa ajili ya shughuli za vijana za uzalishaji mali na kufanya biashara. Wastani wa ekari 870 kwa kila Mkoa zimetengwa kwa ajili ya shughuli za vijana, ikiwa ni pamoja na kilimo na ufugaji.

Nne, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na Wadau wengine, imejenga na kukarabati miundombinu ya kilimo kama umwagiliaji, barabara, masoko na maghala ya kuhifadha nafaka, ili kuendeleza kilimo na kuvutia vijana wengi kujijiri katika sekta hii.

Tano, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na Wadau wengine, imewapatia wakulima wa kati mikopo nafuu ya kununulia pembejeo za kilimo kama matrekta makubwa na madogo (*Power Tillers*), huduma za kilimo zimesogezwa kwa wakulima kama mbolea na mbegu bora kupitia mawakala wa kilimo waliopo katika vijiji.

Sita, Serikali imeanzisha Vyuo vya Kilimo vya Kati na Vikuu na inashirikiana na Sekta Binafsi na Wadau wengine, kutoa mafunzo ya kilimo na ujasiriamali kwa vijana, ili waweze kuendesha kilimo cha kibiashara.

MHE. AMINA M. MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri, pamoja na jitihada zote na juhudi mlizozieleza humu haziwezi kufanyika kama vijana hawa hawana ardhi. Katika Tanzania maeneo ambayo yameathirika sana na ardhi kutokana na mashambapori ya mkonge ni Tanga hususan Pangani. Kuna vijiji ambavyo ni kama visiwa, hawana kabisa maeneo ya kulima kutokana na haya mashambapori; kama Mwera, Langoni, Ushongo pamoja na maeneo mengine. Mheshimiwa Waziri analifahamu hili, Mheshimiwa Lukuvi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Angella Kairuki.

(i) Je, Mheshimiwa Waziri unawaambia nini wananchi hawa ambao wameathirika; unawasaidiaje?

(ii) Kwa kuwa nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria na Taratibu tulizojiwekea. Naomba Mheshimiwa Waziri awaambie Watanzania kupitia Bunge hili, ili waweze kujua; Sheria ya Ardhi inasemaje kwenye mashambapori yaliyokaa muda mrefu, kuna mengine yamekaa zaidi ya miaka 20; Sheria ya Ardhi inasemaje ili wananchi wasije wakajichukulia hatua mikononi mwao? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amina Mwidau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuhusiana na mashambapori yaliyoko Tanga, napenda tu kusema kwamba, tayari mchakato umekwishanza na yapo mengi ambayo tayari Mheshimiwa Rais alisharidhia ubatilisho wake. Kama ambavyo nimekuwa nikijibu humu ndani Bungeni, ametoa sharti kwa Halmashauri mbalimbali Tanga na kwingineko, ni lazima tupate Mpango wa Ugawaji. Kwa Tanga mpaka leo hii hatujaupata Mpango huo wa Ugawaji! Tunahofia yasije yakarudi mashamba haya na baadaye kwa ujanjaujanja tu, watu wakagawana mashamba na mwisho wa siku wanavijiji wa sehemu ile, wazawa wa pale, wakajikuta hawana ardhi. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Amina Mwidau pamoja na Wabunge wote wa Tanga na kwingineko, muendeele kufuatilia, zihimizeni Halmashauri zenu za Wilaya, zituletee Mpango wa Ugawaji wa Ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuongeza pia, kama ambavyo mmekuwa mkifuatilia katika vyombo vya habari, kwa mashambapori mbalimbali Mkoa wa Morogoro, kwa mashambapori mbalimbali yaliyotelekezwa Mkoa wa Pwani, tayari tumeshaanza hatua na tayari Mheshimiwa Waziri ameshapendekeza kwa Mheshimiwa Rais; mfano kwa Mkoa wa Pwani mashamba takribani 19 na tunaendelea vivyo hivyo kwa Morogoro na kwingineko, Hatutakuwa na mzaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, alitaka kujua utaratibu wa Kisheria; Sheria inasema nini kuhusiana na watu waliotelekeza mashamba hayo? Nipende tu kumwambia Mheshimiwa Amina Mwidau kwamba, moja ya sharti au moja ya kigezo cha ubatilisho, unatakiwa uwe unalipa kodi ya ardhi kila mwaka. Pili, unatakiwa uwe umeliendeleza, moja ya nane ya shamba husika ni lazima liwe limeendelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa swali la pili, nadhani ndiyo nimeshalijibia, niombe sana kupitia Bunge hili vilevile Wabunge wenzetu, wako wengine wana mashambapori humuhumu ndani, tunaomba sisi wenyewe tuwe mfano, tuhakikishe sisi wenyewe tunayaendeleza mashamba haya na tuhakikishe sisi wenyewe tunalipa kodi ya ardhi ndipo tuweze kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda nijibu sehemu ya kwanza ya swali la nyongeza la Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumekuwa tukisema, jukumu la kuainisha maeneo kwa ajili ya vijana kufanyia biashara, kufanyia kilimo, ni la Halmashauri. Niseme tu hapa na bahati nzuri Wakuu wa Mikoa wako hapa Dodoma wote; mwaka jana tuliwekeana Mkataba ambao ulisainiwa na Wakuu wa Mikoa wote. Moja katika mambo ambayo walitakiwa kwenda kufanya ni kuhakikisha kwamba, Halmashauri ambazo ziko kwenye Mikoa yao, zinatenga maeneo kwa ajili ya vijana kufanyia biashara, kwa ajili ya vijana kufanyia kilimo, ufugaji na uvuvi. Nina hakika suala hili linaendelea kutekelezwa na Mikoa na Halmashauri zetu.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tumekula muda ambao siyo wetu. Sasa naomba kwanza niwatambue baadhi ya wageni walioko humu ndani.

Tunao wageni wa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, ambao ni Ndugu Mhache Paulo na Ndugu Lundgrean Mcharo, akiambatana na familia yake. Naomba ndugu zetu hawa wasimame walipo kama wapo humu ndani! Ahsante. Karibuni sana, nawatakia maisha mazuri. *(Makofi)*

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Jasson Rweikiza, ambao ni wafugaji wa nyuki kutoka Bukoba Vijijini wakiongozwa na Ndugu Sadick Muganyizi. Naomba hawa Wataalamu wa Nyuki wasimame walipo! Ahaa! Wako sehemu hii hapa; ahsanteni sana, tunawatakia kazi njema hiyo ya ufugaji wa nyuki. Hili ni zao jipya katika jamii.

Tuna wageni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji ambao ni Ndugu Ahmed Othman, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Itigi na Ndugu Michael Mnyabai, Katibu wa Jimbo. Naomba hawa nao wasimame walipo! Ahaa, wako sehemu hii hapa. Ahsante, karibuni sana na kazi njema. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, ambao ni Wanafunzi na Walimu 28 wa Chuo cha Azania kutoka Dar es Salaam. Hawa Wanachuo wa Azania wasimame kwanza na Walimu wao! Ahsante sana. Azania ni shule kongwe yenye sifa zake siku za nyuma zile. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wengine wa Mheshimiwa Zungu, ambao ni Ndugu Mwinyi Maulidi, Ndugu Amina Iddi na Ndugu Hamis Kinye. Wako wapi hawa?

Ahaa, mwingine yuko pale na wengine wawili wako hapa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni, hawa ni Wanafunzi 80 na Walimu 6 kutoka St. Peter Claver School ya Morogoro. Hawa nao wasimame wa Claver! Ahsanteni sana, someni kwa bidii. *(Makofi)*

Tuna Wanafunzi 33 na Walimu 4 kutoka Shule ya Msingi ya Feza ya Dar es Salaam; na hawa pia wasimame walipo! Ahaa, ahsanteni sana, tunawataki masomo mema na msome kwa bidii. Elimu ndiyo ufunguo wa maisha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kipindi cha maswali, naomba Wenyeviti wote, Kamati ya Uongozi tunataka ikae sasa hivi tuweze kuangalia ile ratiba yetu. Kwa hiyo, ni Wenyeviti wote na kama hakuna Mwenyekiti, Makamu wake, katika Ukumbi wa Spika, baada ya maswali, kipindi hiki.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, saa nane watakuwa na Kikao chao katika Ukumbi Namba 231.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mnisikilize; katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa, Bunge lilipitisha Miswada ya Sheria ya Serikali 14. Kwa Taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba, tayari Miswada tisa imekwishapata Kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria za Nchi zifuatazo:-

Sheria ya Udhhibiti wa Ajira kwa Wageni ya Mwaka 2016 *(The Non Citizens' Employment Regulations Act, 2015, No. 1, 2015)*; Sheria ya Kudhibiti Silaha ya Mwaka 2015 *(The Firearms and Ammunition Control Act, 2015, No. 2, 2015)*; Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Stakabadhi Ghalani ya Mwaka 2015 *(The Warehouse Receipts (Amendment) Act, 2015, No. 3, 2015)*; Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya Mwaka 2015 *(The National Payment System Act, 2015, No. 4, 2015)*; Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI ya Mwaka 2015 *(The Tanzania Commission for AIDS (Amendment) Act, 2015, No. 6, 2015)*; Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2015 *(The Statistics Act, 2015, No. 9, 2015)*; Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania ya Mwaka 2015 *(The Youth Council of Tanzania Act, 2015, No. 12, 2015)*; Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015 *(The Cybercrimes Act, 2015, No. 14, 2015)*; na Sheria ya Miamala ya Kielektroniki ya Mwaka 2015 *(The Electronic Transaction Act, 2015, No. 15, 2015)*. *(Makofi)*

Miswada mitano iliyobaki, nitaitolea Taarifa mara tu baada ya kupata Kibali cha Mheshimiwa Rais.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, Kamati ya Uongozi tukakae sasa tuweze kuirusha ratiba yetu kabla hatujaendelea nayo. Kwa hiyo, namwomba Mwenyekiti aje anipokee kazi hii.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2015/2016 Ofisi ya Waziri Mkuu na TAMISEMI

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Hoja ya Waziri Mkuu. Tunaanza na Mheshimiwa Moshi Kakoso, ajiandae Mheshimiwa Vick Kamata.

Mheshimiwa Kakoso? Mheshimiwa Vick Kamata? Mheshimiwa William Ngeleja? Mheshimiwa Gosbert Blandes? Mheshimiwa Gosbert!

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Karagwe, kwa kunipa ushirikiano, kwa kunichagua na kuniadini. Namshukuru sana Mkuu wetu wa Mkoa. Nawashukuru sana DSO wa Karagwe, OCD wa Karagwe, Waheshimiwa Madiwani wote, Mkurugenzi Mtendaji na Watendaji wake wote; kwa kunipa ushirikiano katika kipindi changu hiki cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa leo kifua mbele, kwa sababu katika Bunge letu hili humu ndani, hakuna Mbunge hata mmoja anayeweza kusimama akatamba kwamba, ananizidi umeme vijijini Karagwe. Mimi ndiyo wa kwanza kupewa umeme mwingi, nashukuru sana. Wananchi wa Karagwe naomba wajipange kuingiza umeme majumbani mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitano hii kwa Karagwe wameshuhudia maendeleo ya ajabu, siwezi kuyataja katika hizi dakika 10 ambazo umenipa. Wanafahamu kwamba, tumeongeza zahanati za kutosha, tumejenga vyumba vya madarasa kwenye shule sekondari na msingi na tumejenga maabara na mambo mengine mengi sana pamoja na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomaliza miaka mitano ninajivunia barabara ya lami ya kutoka Kyaka mpaka Bugene, barabara hiyo imeisha na wananchi wameanza kuitumia. Wananchi wa Karagwe wafahamu kwamba, kuna barabara inaendelea kutoka Bugene kwenda Nyaishozi mpaka Benako, ya lami inajengwa. Vilevile kuna barabara nyingine ya lami inajengwa kutoka Mgakorongo, Kituntu hadi Mrongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo ni faida kubwa sana. Anayesema hakuna maendeleo Karagwe, huyo anajidanganya na anapoteza muda wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii, kuna watu wanapitapita Jimboni Karagwe wanasema Blandes safari hii anaondoka, siyo kweli! Wananchi wa Karagwe wanajua kujipanga na kupiga kura vizuri sana. Ninakuja kugombea Wananchi wa Karagwe, ninajua mtanichagua kama ilivyo kawaida na ndivyo tunavyowashinda Wapinzani wetu siku zote, *nikwetu bhasinga!* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze mawili, matatu; tuna tatizo kubwa sana katika Ziwa Viktoria. Mwenzangu Rweikiza alizungumza jana kuhusiana na meli katika Ziwa Viktoria; ahadi ya Mheshimiwa Rais ni ya siku nyingi, tunahitaji kuona meli hiyo katika bajeti hii inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo la maji. Maji ya kutoka Rwakajunju kwenda mpaka Mrushaka, kwenda mpaka Kayanga. Mheshimiwa Waziri wa Maji atakapokuja hapa, ningetaka

atueleze shilingi ngapi wametenga. Najua tayari wameshapima Mradi huo, tunataka kuona unafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Karagwe nilitaka niwafahamisha kwamba, tumepata Baraza la Ardhi na Nyumba katika Wilaya ya Karagwe limeanza. Tunaishukuru sana Serikali; wananchi walikuwa wanasafiri kutoka mbali kwenda Bukoba, sasa hivi huduma hiyo iko Jimboni kwangu Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiomba sana hapa Serikali itupatie hifadhi ya Akiba ya Pori la Kimisi na hapa ninamwomba Mheshimiwa Nyalandu anisikilize kwa makini. Pori la Kimisi limekuwa sehemu ya kulishia ng'ombe, siyo tena hifadhi ya maliasili. Kwa hiyo, naiomba Serikali irudishe kwa wananchi hifadhi hiyo, ili Wananchi wa Karagwe na sehemu zingine, waweze kulima na kufuga na kufaidi rasilimali yao ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba Chuo cha VETA hapa ndani ya Bunge, kwa ajili ya Mkoa wa Kagera. Nataka nipate majibu kwamba, VETA Kagera imefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba sana kwa muda mrefu iletwe Sheria ya kuifanya Dodoma iwe Makao Makuu. Sheria hiyo haijaja hapa ndani ya Bunge mpaka tunamaliza; ni kwa nini haiji? Nataka nipate majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hapa nilimwona Mheshimiwa Waziri Mkuu, ningomba Mheshimiwa Hawa Ghasia anisikilize; Mheshimiwa Rais alipokuja Karagwe alikutana na Masista wa Parokia ya Nyakaiga, Karagwe, aliwaahidi kuwapatia trekta, na jembe na *harrow*. Tunashukuru sana trekta limekuja na majembe yamekuja. Tunaomba umfikishie Mheshimiwa Rais shukrani zetu kutoka kwa Masista. *(Makofi)*

Kitu ambacho hakikufika kwa bahati mbaya ni ile *harrow* ya kuweza kuvunjavunja udongo. Naomba sana safari hii niondoke nayo nikawapelekee Masista wa Nyakaiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Karagwe tuna tatizo, tumepata maendeleo, lakini pia tumepata matatizo; barabara ya lami imevunja nyumba za maaskari na maofisi; maaskari wetu, OCD na watu wake hawana mahali pa kukaa. Naomba nijue ni lini zitajengwa nyumba hizo zikamilike ili maaskari wetu wapate mahali pa kukaa?

Sambamba na hilo, nyumba za askari magereza, nyumba za walimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nakupongeza, lakini kuna moja nilitaka niliseme ambalo ni sikitiko kubwa sana katika Jimbo langu la Karagwe na ambalo ni tatizo kubwa sana. Kazi ya Bunge ni kusimamia Serikali, sasa kuna baadhi ya Wakuu wa Wilaya, Mheshimiwa Ghasia na Mheshimiwa Mwanri nisikilizeni kwa makini, kuna baadhi ya Wakuu wa Wilaya wanadhani Mbunge ni Mtumishi katika ofisi yake ya Wilaya. Mojawapo wa Wakuu wa Wilaya hao ni Mkuu wa Wilaya ya Karagwe, Darry Rwegasira. Tumepata bomu la Mkuu wa Wilaya huyo, hajui kama Mbunge anamsimamia yeye, anadhani yeye anamsimamia Mbunge. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme hilo kwa sababu tumepata shida, Mkuu wa Wilaya yetu huyo Darry Rwegasira, ameacha kufanya kazi kwa manufaa ya Watanzania, sasa hivi anafanya kazi kwa manufaa ya wahamiaji haramu kutoka nchi ya Rwanda. Nitatoa mfano mmoja, mifano ni mingi lakini kwa sababu ya muda nitatoa mmoja. Huyu Mkuu wa Wilaya ameandika barua kwenda kwenye kijiji kinaitwa Kanogo, Kata ya Nyakabanga, ambacho kipo

mpakani mwa Tanzania na Rwanda, akiwataka Wakulima ambao ni Watanzania waondoke ili Wanyarwanda na mifugo yao walishe mifugo yao hapo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelipinga kwa nguvu zote na nitaendelea kulipinga na nitapambana naye. Mheshimiwa Mwanri unakumbuka, nilikuja hapa nikakupa taarifa ukaunda Tume, Tume hiyo ulipoiunda ukapeleka kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa alimteua Mkuu wa Wilaya ya Missenyi, Mkuu wa Wilaya ya Missenyi akajumuishwa na DAS wa Wilaya ya Karagwe ambaye ndiyo aliandika barua kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, ulitegemea hawa watu wakupe matokeo gani? Mkuu wa Wilaya bado yuko anatamba hapo, anafukuza wananchi wangu kwenye ardhi yao kwa manufaa ya wageni. Yule Mkuu wa Wilaya Darry Rwegasira, kimwili yuko Tanzania lakini kiroho yuko Rwanda na huyu hatufai hata kidogo.

Nilitaka niseme kuwa, Mheshimiwa Mwanri tuondolee ule mzigo Karagwe, hatumhitaji, Karagwe siyo mahali pa kupeleka watu waliochoka, yule mama amebakiza miezi kama miwili ya kustaafu. Ningeomba sana tena narudia hili, Wilaya ya Karagwe siyo ya kutuletea watu wamechoka kivile, yule mama anajiandaa kustaafu muda wowote, ndiyo maana anachukua chake mapema. Wananchi wa Karagwe wamenituma hasa wa kijiji cha Kanogo, juzi amekwenda ana bunduki na maaskari kwenda kuwafukuza wananchi, nimewaambia wananchi wajandae, wamdhibiti kwa nguvu zote kwa sababu ile ni haki yao. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pamoja na Diwani wa Kata ya Nyakabanga, Mheshimiwa Justine Fidelis, tumepinga yule mama kwa nguvu zote. Kwa kuwa Diwani ni mtu mdogo, amemkamata tarehe 20 Aprili, 2015 akamuweka ndani, amemtoa tarehe 22 Aprili, 2015 kinyume cha sheria amekaa siku tatu ndani, kwa sababu anapinga ardhi ya wananchi isiende kwa wahamiaji haramu Wanyarwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi hawezi kunikamata kwa sababu ananiogopa sana. Nilitaka niseme kwamba, kama Serikali haitachukua hatua za haraka kumtoa pale, kuna mambo ambayo sisi tumejipanga Karagwe, mtasikia ambacho tatakifanya kwa mara ya kwanza na hamtasahau. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nimalizie kwa kusema kwamba, tulipanga bajeti ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Mpiga Chapa wa Serikali ilikuwa apewe shilingi bilioni moja mwaka mwaka wa fedha uliopita, lakini kwa masikitiko amepewa asilimia sifuri, hakupewa hata shilingi moja. Ninasikia kuna watu wanamlaumu kwamba hajui kufanya kazi, atafanyaje kazi katika mazingira kama haya ambapo hapewi fedha hata kidogo?

Tuna Hospitali ya Wilaya ya Nyakanga DDH; Hospitali hii imekuwepo kwa muda mrefu, inafanya kazi na imekuwa ikipelekewa ruzuku, lakini sasa hivi ruzuku haiendi na ikienda inakuwa ni kidogo sana na haitoshelezi, wananchi wanateseka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni ya wazee imezungumzwa sana ndani ya Bunge; ni lini Serikali itawapatia wazee wetu pensheni? Sisi sote hapa ni wazee watarajiwa, ningetamani nipate majibu pensheni ya wazee ni lini na matibabu ya uhakika ya wazee. Kwa nini wazee wetu hawapewi matibabu ya uhakika na ya bure?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna watu wetu wanaofanya kazi vijijini, wakiwemo Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Waheshimiwa Madiwani, posho wanazopewa ni kichekesho kikubwa sana. Mimi ningependa Serikali ilianganalie hili, Watendaji wetu wazuri hawa ni lini posho zao zitakuwa za uhakika na kuridhisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kuhusiana na pango la ardhi (*land rent*). Pango la ardhi siyo rafiki kwa Watanzania wote, limekuwa juu kiasi kwamba watu wameshindwa kulipia viwanja vyao, viwanja vingine vitachukuliwa kama Naibu Waziri alivyosema. Ninapendekeza sana hiyo ishushwe ili Wananchi wa Tanzania wamiliki viwanja viweze kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mimi niendeleo kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa kuniadini, ninakuja jipangeni na watu tutawapiga kama kawa. Ahsanteni kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa leo. Ninaelewa kabisa kuwa, ataendelea kuniwezesha mpaka pale tutakapofika mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda kuishukuru Serikali yangu, kwa namna ambavyo imekuwa ikifanya kazi kwa bidii kuhakikisha inawapatia Watanzania maisha bora. Ninaomba niwashukuru ndugu zangu Wanakatavi, kwa kuwa wasikivu, watulivu na wenye upendo, kwa kuwa tumekuwa tukifanya nao kazi kwa karibu na kuweza kuisukuma Katavi yetu kwa ajili ya maendeleo. Pamoja na kwamba wengine wanabeza kwamba ni Mkoa wenye watu 500,000, lakini ukweli ndiyo huo umeshakuwa Mkoa, hatuwezi kuurudisha nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze moja kwa moja kuhusiana na masuala yanayohusu Wanakatavi. Napenda nianze kuongelea masuala ya maendeleo. Mkoa wetu wa Katavi ni mpya, pamoja na Mkoa wa Simiyu, Geita na Njombe.

Kwanza kabisa, napenda kuiomba Serikali pamoja na kazi zake nzuri inayofanya kwa ajili ya wananchi, iingalie hii mikoa kwa jicho la pekee. Itenge bajeti kwa ajili ya kuharakisha maendeleo katika hiyo mikoa. Mikoa ile haina huduma nyingi za kibenki, wananchi ni wachapakazi, wana mazao yao kule, wana biashara zao za kiuchumi, lakini wanatabika sana na huduma za kibenki. Sambamba na huduma za TRA, tunaomba Serikali ianze mchakato na itenge bajeti ya pekee ijenge Ofisi za Mikoa za TRA, kuondoa usumbufu kwenda katika mikoa mingine. (*Makofi*)

Lingine, Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiyo mwenye Jimbo la Mlele hayupo lakini najua ananisikiliza na wananchi wake waliniagiza na nilikwishaongea naye, sasa nataka waelewe kwamba, nimeongea na Mbunge wao Jimbo na kilio chao ninawafikishia. Wananchi wake wa Jimbo lake wana kilio cha hospitali ambacho kilikuwa Kituo cha Afya cha Inyonga, ambacho kilikuwa kwenye harakati ya kupandishwa daraja kuwa Hospitali ya Wilaya. Wananchi wa Katavi na Wananchi wa Mlele, ninaomba niwaambie, Mbunge wenu ambaye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameahidi kuwamalizia hospitali yenu ile pamoja na kwamba wao kwa juhudi zao waliweza kuchangia maendeleo kwa ajili ya kumaliza jengo la *theatre* na *mortuary*.

Lingine, napenda niishukuru Serikali kwa namna pekee kwani sasa kupitia Kampuni ya *Vitel* tuna uhakika Wananchi wa Mkoa wa Katavi na Simiyu tunaweza tukafanya mawasiliano kwa ajili ya kutafuta masoko. Kwa sababu sasa hivi nimetoka kule, mitaro imeanza kuchimbwa na wananchi nimefanya nao mikutano, wameiona na wameniambia wanaishukuru sana Serikali kwa kuwa sasa hivi watapata mawasiliano ya uhakika ili waweze kujitafutia soko la mazao yao.

Ninapenda niishukuru Serikali kwa namna ya pekee inavyotengeneza barabara, lakini Wananchi wa Katavi wamenituma nimwulize Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete pamoja na Waziri Mkuu kwamba; wanawaachaje na barabara ya kutoka Mpanda mpaka Tabora?

Walipenda wasikie majibu kwamba; wanawaachaje maana ile barabara tumeiongelea sana na lengo la Serikali ni kuunganisha barabara za mikoa? Sasa tunataka tuunganishwe na sisi, miezi miwili wanasema michache, lakini ukiamua ukiweka mawazo yako kwenye vitendo now, tunaweza. Kwa hiyo, mimi ninaamini kabisa kutoka Mpanda, Inyonga, Koga, Sikonge na Tabora, tutapata lami mpaka mwezi wa kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Katavi wa upande wa CHADEMA; Mheshimiwa Arfi na ndugu yangu Mama Mallac, tumekuwa mstari wa mbele kwa kuweka maendeleo mbele; na ndiyo maana michango yao ya jana ilikuwa mizuri. Sana sana nilikuwa naogopa tu, Mama Mallac aliposema anaipongeza Serikali, nikasema Mungu wangu wee leo wanamwita kwenye kikao kumtukana, nilijua watamwita kumtukana; lakini ameipongeza Serikali kwa kujua Katavi ilivyo. Ameipongeza Serikali kwa kuona inavyowasaidia Wanakatavi, kwa hiyo, mimi nakushukuru sana kwa sababu tumekuwa kitu kimoja kuangalia mbele masilahi ya wananchi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Arfi, mchango wako ulikuwa mzuri, Mheshimiwa Mama Mallac mchango wako ulikuwa mzuri, inaonyesha jinsi gani Wanakatavi tulivyo na upendo na umoja. CCM oyee! *(Makofi)*

Wameongelea masuala ya reli na mimi naongezea hapo; ndugu zangu wa Ugala wamenituma kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu baba yao wa Jimbo, ndugu zake wa Kambuzi, Katumba, Shankala na wajasiriamali kwa ujumla wa Mkoa wa Katavi, angalau na ndugu zangu shemeji zangu Wasukuma walioko kule, angalau

MHE. ANNAMARSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Pamoja na kwamba...

T A A R I F A

MHE. ANNAMARSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nirekebishe mchango wa Mheshimiwa Mbunge mwenzangu, amesema kwamba, ananishukuru kwa kuwa niliipongeza Serikali kwa maendeleo ambayo nimeyasifia Mkoani Katavi. Nirekebishe kwamba, nilisifia Serikali kwa kuunga mkono Mfuko wa UKIMWI wa Taifa, lakini sikupongeza maendeleo kwa sababu nililalamika barabara tulizonazo pamoja na reli, ila niliipongeza kwa Mfuko wa UKIMWI wa Taifa. *(Makofi)*

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, la msingi ni kwamba hoja inayoongelewa ni ile ile ya maendeleo na pongezi ilikuwepo. *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ndiyo tunaendelea kupongeza.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba, wananchi niliowataja wa kutoka Tabora, kupitia Kaliuwa Uramba, Ugala, Kambuzi, Shankala, Katumba mpaka Mpanda, takribani kwa miezi mitatu walikuwa hawana usafiri wa reli na ndiyo reli tunayoitegemea. Tatizo niliambiwa ni vichwa, wengine wakasema ni reli. Serikali ninaiomba sasa ifuatilie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu uulinde. Matatizo mengi, napenda niongelee suala la posho kwa Wenyevidi wa Vitongoji na Vijiji. Hawa ndiyo watu wetu watendaji kule, tusipowalipa posho ndiyo wanaowaambia wachungaji ingizeni ng'ombe Katavi, ingizeni ng'ombe mbugani, kafanye hivi, anapewa mbuga wawili wale watu ng'ombe wao wanapigwa

mnasema Serikali! Tunaomba muwaangalie hawa watu, tusipowawezesha ni matatizo, wao ndiyo wenye kujua mipaka ya ardhi, wao ndiyo wenye kusimamia ardhi kule, wao ndiyo wenye kusimamia maendeleo. Kwa hiyo, tunaomba kabisa muangalie posho zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, napenda nitoe pole za pekee kwa watu wangu wa Mamba; kuna mlemavu mmoja ambaye kuamkia jana amekatwa mkono. Nawaomba ndugu zangu Watanzania, hili suala kwa kweli ni baya, katika suala la Utawala Bora linatushusha hadhi Kimataifa. Unaenda nje *sometimes* unaogopa kusema unatoka Tanzania wanauliza ninyi ndiyo mnauwa walemavu na wazee na nini, unajisikia vibaya. Ndugu zangu tuwalinde hawa watu kwa umoja wetu, ni rai ninaomba, tunakolala inaonyesha kabisa hawa walemavu wanalala peke yao kwenye vyumba, sehemu ya familia, baba, mama, tukae nao hawa watoto usiku, tulale nao.

Hii ni rai ninawaomba Watanzania ambao tuna familia za watoto hawa, maana yake na wao tutawaita *endangered species* sasa hatufiki huko, hawa ni binadamu wenzetu, ni ndugu zetu, ni watoto wetu, wana haki sawa ya kuishi kama sisi. *(Makofi)*

Ninatoa raia kwa Watanzania, tuondoke na hizi imani, tufanye kazi kwa bidii kama alivyosema Mheshimiwa mmoja jana alipokuwa anachangia. Ukifanya kazi kwa bidii utapata. Usikae tu, nakwambia nenda kaoge pale uchi, wewe unasema hawakuoni, wamwulize yule nani aliyenda Sumbawanga akadanganywa, yule aliyepora hela, alikuwa anaitwa Kasusura; akaambiwa nenda wewe hawakuoni akaenda kum-*approach* mwanamke akifikiri hawamwoni! Sasa tuache hayo, twende na sayansi na teknolojia, tufanye kazi kwa bidii, hata maandiko yanasema fanya kazi kwa bidii. Tuachane na hayo kabisa.

Sasa hawasemi wao wafanyabiashara, tunaambiwa wanasiasa ndiyo tunaofanya hayo. Tufike mahali na sisi wanasiasa tusimame majukwaani tukemee hayo na tuwaeleweshe wananchi wetu. Tusifike mahali tunaangalia watu, jamani mkono wewe yaani *imagine*, panga lile mtu ukakate; unajisikiaje? *(Makofi)*

Hebu tufike mahali tujaribu kuliangalia hili ni janga, ni janga linatushushia hadhi na linatushushia heshima Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwanjale, ajiandae Mheshimiwa Kakoso!

MHE. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu na mimi katika Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amenipa uzima, nipo hapa leo, maana lolote lingeweza kutokea.

Pili, naishukuru Serikali, kwa kazi nzuri hasa kwa miaka hii mitano ambayo nimekuwa madarakani nimeona mabadiliko makubwa sana na maendeleo makubwa katika Jimbo langu la Mbeya Vijijini. Naishukuru Serikali kwa kutupatia Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, ambapo wiki iliyopita tulikuwa tunafanya uchaguzi pale na bahati nzuri CCM imepata ushindi pale. *(Makofi)*

Suala la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ni la muda mrefu, iliombwa tangu 2004 lakini mwaka huu ndiyo tumepewa kuwa Mji Mdogo. Mji Mdogo unahitaji kuboreshwa pia na tumejaribu kuomba hapa katika Bunge uboreshaji wa Mji hasa katika miundombinu ya maji.

Ninaiomba Serikali katika eneo hilo ijaribu kutenga pesa ya kutosha kwa ajili ya kuhakikisha Miradi ya Maji ambayo ni muda mrefu sana inabadilishwa inaboreshwa. Kwa sababu maji ambayo tunapata sasa hivi yanatoka mjini lakini hayatoshelezi mahitaji ya wananchi walioko katika mji ule. Kwa hiyo, naomba TAMISEMI waliangalie hilo.

Nashukuru pia kwa ujenzi wa barabara pamoja na lami, ambayo ni sehemu ya ahadi ya Rais. Rais wakati amekuja katika kampuni za mwaka 2010, aliahidi kwamba, Stendi ya Mbalizi na barabara zake zitaboreshwa. Bajeti ambayo ilitengwa kwa ajili ya kuboresha barabara na stendi ilikuwa bilioni 1.3, lakini fedha ambayo imefikia Halmashauri ilikuwa milioni 525.

Kwa hiyo, barabara iliyotengenezwa pale bado haijaboreka na bado imesababisha usumbufu mkubwa sana kwa wananchi wa mji ule kwa sababu ile lami walioiweka haipitishi magari yenye uzito mkubwa.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hiyo bajeti ya Shilingi bilioni 1.3 ikamilishwe. Bado Shilingi milioni 800, nilikuwa naomba hizo katika bajeti hii zikamilishwe ili barabara itengenezwe. Ilikuwa ni sehemu ya ahadi ya Rais hiyo, naomba TAMISEMI waliangalie hilo. Lakini miradi ya maji pia kama nilivyosema inazidi kuboreshwa; maji ambayo tunapata sasa hivi bado miundombinu yake ni ya miaka mingi ya nyuma, tangu 1970 na kitu, kwa hiyo haitoshelezi, watu wengi wanakosa maji pale. Ule mji ni mkubwa sasa hivi, watu karibu 60,000 wako pale wanahitaji kupata huduma hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hapa Serikali ilikuwa imeahidi kwamba itapima viwanja kwa ajili ya watu kujenga katika mpangilio mzuri. Niliuliza swali hili, wakasema, tutapima viwanja karibu 2000 na kitu, lakini mpaka leo hii miaka karibu miwili imepita, sijaona jitihada yoyote ya Serikali ya kuboresha upimaji wa viwanja pale. Naomba Serikali pia ilichukue hilo iliangalie isijekuwa watu wanajenga kiholela tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilikuwa naomba kulisema ni suala la umeme. Naishukuru Serikali, hasa REA pamoja na Wizara ya Nishati. Waziri na Watendaji wake wote wamefanya kazi nzuri sana. Kusambaza umeme katika vijiji vingi nchi hii, siyo kazi ndogo. Hata Ulaya nchi zilizoendelea, kuna maeneo mengine umeme hakuna katika vijiji. Wala siyo uongo!

Kwa hiyo, ina maana kwamba kazi ambayo inafanywa na Serikali hii ni nzuri na ya pekee. Nafikiri itakuwa ni kazi ya pekee katika nchi nyingi za Afrika. Siyo rahisi kusambaza umeme kila mahali vijijini, lakini kazi hii imefanywa kwa umakini mkubwa sana. Ninachoomba hapa, katika kusambaza umeme vijijini, huwa mara nyingine, kwa mfano kule kwangu wanachukua umeme kutoka Mbalizi naupelekwa lrembo kilometa karibu 60 au 40, unakipatia Kijiji kimoja cha lrembo umeme, lakini vijiji karibu kumi na kitu hapo katikati hakuna umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetuhidi italeti *transformer*, lakini ahadi hiyo naona imechukua muda mrefu sasa, sijui! Wale wananchi wanalalamika kwa sababu nguzo zimepita katika maeneo yao na vijiji vyao lakini umeme unaenda kwa kijiji kimoja tu, lakini vijiji kumi na kitu au kumi na tano hapo katikati hakuna. Nilikuwa naomba hilo lichukuliwe kwa makini kwa sababu ni muhimu hawa wananchi ambao umeme umepita kwao pia wapate huduma hii ya umeme kwa sababu lengo ni kusambaza umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Sekondari, naomba Sekondari zote ambazo zinapitiwa na umeme zipelekewe umeme. Kwa mfano, Sekondari ya Iyalawe pale, Sekondari ya wapi kule, Itundu pale naomba umeme upelekwe. Kwa hiyo, hizo ndiyo hatua mabazo kwa kweli naisifu Serikali ya CCM kwa kazi yake nzuri, kwamba imeweza kufanya kazi hiyo, kusambaza umeme katika vijiji vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nje ya umeme, hata maji pia wamejitahidi, pamoja na kwamba bado hawapati bajeti ya kutosha. Naomba hapa tuisaidie Wizara ya Maji wapate fedha ya kutosha. Tuliishauri Serikali hapa, kama inawezakana kwa nini kusiwe na Wakala wa Maji kama ilivyo kwa umeme ili speed ya kusambaza maji katika vijiji pia iwe haraka kama inavyofanya kwa umeme. Kwa sababu maji ni uhai na ndiyo kitu kikubwa sana.

Kwa hiyo, kwa sababu ni uhai ni vibaya sana kuchezea maisha ya watu kwa kutowapelekea maji ambayo ni safi na salama. Naomba Serikali itenge hela ya kutosha katika Wizara ya Maji maana ni muhimu kweli kweli, kwa sababu watu wanahangaika maji, wanatembea Kilometa nyingi; Kilometa 20, Kilometa 10 kutafuta maji. Fedha itengwe ya kutosha. Tumepiga kelele suala la maji hapa kwa muda mrefu sana, lakini nimeona kwamba halifanyiki vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa naomba hii miradi ya ujenzi wa Zahanati; wananchi wamejenga Zahanati. Kule kwangu tumejenga Zahanati zaidi ya 80 au 100, lakini Serikali inashindwa kupeleka fungu la kumalizia. Naomba TAMISEMI waliangalie suala hili. Nataka tujue ni shilingi ngapi imetengwa hasa kwangu kule Mbeya Vijijini kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Zahanati. Wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anamalizia naomba ajibu hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni Shamba la *Tanganyika Packers*. Shamba hili tumepiga kelele mara nyingi, lakini hatuoni muafaka wake. Naomba hili nalo mlilibu, kuna nini kilichopo mbele yenu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naomba kuzungumzia kuhusu madawa ya kulevya. Jamani madawa ya kulevya yapo tu kwa maeneo ya mijini. Yapo kidogo, lakini itakuwa sawa na UKIMWI. UKIMWI ulianza kidogo, lakini baada ya miaka michache ukalipuka nchi nzima. Hakuna mahali hapakuwa na msiba. Kwa hiyo, naomba suala hili la madawa ya kulevya Serikali ihakikishe kwamba inaweka udhibiti wa kutosha kabisa ili kuhakikisha kwamba tunakomesha.

Bahati mbaya siku hizi vijana wengi wamemaliza Vyuho Vikuu na Mashule, hawana mahali pa kwenda, kwa hiyo, wanakimbilia kwenda kunywa madawa. Naomba tuliangalie kwa kutenga hela ya kutosha kuhakikisha kwamba tunadhibiti na kuongeza hata Watumishi katika kitengo hicho au katika Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naishukuru Serikali na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Kakoso, ajiandae Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Mkosamali na Mheshimiwa Sendeka.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote naishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanyika hasa katika kusukuma maendeleo ya Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi sana ambayo yamefanyika ambayo yamesukumwa na Serikali; na kwa ukaribu sana wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ikiwa ni chachu ya kusukuma maendeleo ndani ya Mkoa wa Katavi. Mkoa wa Katavi tulikuwa na vitu vingi sana ambavyo havipo. Mkoa huu ulikuwa haujafunguka kabisa hasa kwenye Sekta wa Barabara. Sasa hivi kuna ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Sumbawanga kuja Mpanda, lakini tuna kilometa karibu 100 zinaanza kujengwa katika mwaka wa fedha kwenda Mkoa wa

Kigoma. Kwa hiyo, tutakuwa tumefungua mawasiliano kati ya Mikoa ambayo kimsingi ilisahaulika sana Ukanda wa Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Ujenzi wa uwanja wa ndege ambao umekamilika, zimejengwa sekondari katika maeneo mengi ndani ya Mkoa, tumekamilisha maabara karibu sehemu kubwa ndani ya Mkoa wetu, lakini bado changamoto zinazohitajika kufanywa na Serikali katika kipindi hiki. Tunahitaji kukamilisha ujenzi wa barabara ambayo ilianza kujengwa muda hasa barabara ya kutoka Sumbawanga kuja Mpanda ambayo inaunganisha Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imeanza muda mrefu kujengwa, tunaomba sasa Serikali ifike mahali ikamilishe ujenzi wa barabara hii. Barabara hii ikikamilika itasaidia sana wananchi wa Mikoa ya Rukwa na Katavi, lakini bado ujenzi wa barabara ya kwenda Kigoma ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa huu ili iweze kuwasaidia kiuchumi, kwani kutoka Kigoma kuja Mpanda karibu kilometa 196 zinahitajika zijengwe ili zitoe mawasiliano yatakasaidia wananchi kwa maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na barabara ya kutoka Mpanda kwenda Tabora, Serikali imeshaahidi kujenga na Mheshimiwa Waziri Mkuu kafanya jitihada za dhati kupata fedha kupitia Benki ya Afrika. Tuna imani kubwa sana kwamba sasa hiyo barabara inahitaji ijengwe ili iweze kusaidia wananchi wa Mikoa hii na siyo tu Mikoa ya Tabora na Katavi, ni pamoja na Mikoa yote ya Kanda ya Zawa ambako kimsingi mahitaji yao makubwa hasa ya chakula wanategemea sana barabara hii ambayo ni kunganishi katika Kanda ya Ziwa. Tunaomba Serikali ielekeze nguvu katika maeneo hayo ili iweze kusaidia kukamilisha miradi ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika barabara zinazounganisha Wilaya, kuna barabara ya kutoka Mpanda kwenda Karema ambako ni Ukanda wa Ziwa na kunaunganisha wananchi wa nchi mbili. Nchi ya Kongo na nchi ya Tanzania, barabara hii siyo nzuri. Naiomba sana Serikali iweze kukarabati barabara hasa katika kipindi cha mvua nyingi zilizonyesha, zimeharibu barabara hii na tunaomba Serikali ielekeze nguvu na ifanye matengenezo ya dharura ili waweze kusaidia wananchi kupata huduma katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo barabara nyingine inayounganisha Wilaya, barabara ya Kibo-Mwese. Barabara hii inaunganisha kati ya Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma Kusini kwenye Jimbo la Mheshimiwa Kafulila. Tunahitaji barabara hii iweze kutengenezwa ili iweze kuwasaidia wananchi hawa na iweze kutoa mwanya wa kiuchumi katika maeneo ambayo yana shughuli za kiuchumi ukanda wa Ziwa Tanganyika na ukanda wa huku juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ishughulikie suala la wananchi waliopata uraia hasa wa makazi ya Mishamo na Katumba. Serikali kwa nia njema iliweza kuwasaidia wananchi ikatoa uraia, bahati mbaya sana kuna kasoro zilizojitokeza. Wapo wananchi ambao wameanza kutenganishwa na familia zao; unakuta kwenye mji mmoja, baba anapata uraia, mama anakosa. Kwa hiyo, badala ya kuwasaidia hawa wananchi, sasa tunaanza kuchangia kuwatenganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana, wakati fulani unakuta mtoto wa miaka mitano ananyimwa uraia kwa kigezo kwamba hana sifa, yeye ni jambazi. Sasa unashangaa, miaka mitano, mashine inamkataa yule mtoto ili atenganishwe na familia ya kwao. Naomba sana Serikali iangalie na ichukue hatua za dharura ili kuwasaidia hawa wananchi wasije wakawa na manung'uniko wakati ilikuwa imetoa nia njema kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, wananchi hawa wanahitaji kushiriki shughuli zote kwa sababu tayari ni wapiga kura na ni raia wa Tanzania. Naomba sana Serikali ishughulikie vituo vya wapiga kura ili waweze kushiriki shughuli zote kama Watanzania ambao wamepewa uraia kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo naomba kuchangia zaidi ni suala la mawasiliano. Kwenye suala la mawasiliano bado jitihada za Serikali zilizofanywa zinahitajika sana maradufu kuliko ilivyofanya mapema. Eneo hili tuna Kata ambazo kwenye Mkoa wa Katavi bado tunahitaji huduma ya mawasiliano. Mfano, Kata ya Katuma, Sibwesa na Kubungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali imeleta Kampuni ya *Viatel*, bado kasi ya ujenzi siyo nzuri. Kwenye Kata ya Katuma ambako kuliwekezwa na Serikali kiasi cha fedha karibu Shilingi milioni 160 kama ruzuku ya kusaidia Kampuni ya *Vodacom* ijenge mnara utakaosaidia Kata ya Katuma na Sibwesa, mpaka sasa bado haujajengwa. Naomba Waziri mwenye dhamana aweze kutoa majibu ya msingi ni lini mradi ule utakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la kilimo, tunaiomba sana Serikali iwajengee mazingira mazuri wananchi hasa wakulima wadogo wadogo ambao kimsingi mwaka 2014 walipata shida sana kwa kukosa masoko na ambayo imepelekea mwaka huu wakulima hao wakakosa hamu kubwa ya uzalishaji kiasi kwamba kuna dalili za kuwa na njaa.

Naiomba sana Serikali iweke huduma hasa kwenye pembejeo, iweke ruzuku za pembejeo za mbolea ili ziweze kuwasaidia wananchi wazalishwa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwenye zao la biashara ya tumbaku, ni vyema sana Serikali ikaangalie wakuma wa tumbaku nchini kuwapunguzia gharama za uzalishaji hasa kwa kupanda bei za pembejeo.

Serikali kama itawasaidia ikaweka ruzuku kwenye pembejeo, itawasaidia sana wakulima hao waweze kuzalisha kwa tija, sambamba na kuwatafutia masoko ya nje, kwani sasa hivi wanunzi ambao wanunua zao hili wameanza kuwa na uchambuzi wa kutoa kilo chache sana za kununua kuliko ilivyokuwa mwanzo. Ni vyema Serikali ikachunguza kwamba zao hili ni zao ambalo linawasaidia sana wananchi na linatoa kipato kikubwa sana kwa Taifa. Ni vyema Serikali ikaliangalia hili na ilichukule umuhimu kuwasaidia wakulima wote wa nchi hii wanaolima zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya jambo zuri sana kwa Mkoa wetu kupeleka Walimu, lakini bahati mbaya sana mwaka huu hatujapata mgao wa Walimu wa Shule za Msingi. Kwa Shule ya Sekondari, tunaishukuru sana Serikali, imefanya kazi nzuri na imeongeza Walimu wa kutosha; bado tunaiomba sana Serikali iendee kuleta Walimu hasa kwenye Sekta ya Elimu ya msingi. Ikifanya hivi, itatusaidia sana kupunguza tatizo la uhaba wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee suala la vituo vya kupiga kura kwenye maeneo ya Jimbo la Mpanda Vijijini. Eneo la Mpanda vijijini lina ukubwa wa kilometa 16,900. Vituo vilivyopo ni vichache sana ambavyo vinasababisha wananchi wengi washindwe kupiga kura, kwani ukiangalia hata uchaguzi uliofanyika mwaka 2010, waliojiandikisha walikuwa 37,000 waliopiga kura walikuwa watu 8,000 ni kwa sababu wengi wanashindwa kwenda kupiga kura kwa sababu vituo vyao viko mbali mno. Naiomba Serikali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Mkosamali jiandae.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia fursa hii ili nami niweze kuchangia katika hoja muhimu sana ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda wa siku tatu nimekuwa nikifuatilia kwa umakini sana mazungumzo yanayoendelea humu ndani na ikaonyesha wazi kwamba kuna tatizo. Haiwezekani jambo moja upande mmoja useme Serikali imeshindwa na upande mwingine useme Serikali imeshinda. Kisaikolojia tunasema hilo ni tatizo na lazima kuna mmoja anasema uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kila mahali alikuwa anasema kwamba mafanikio haya yote ni kwa sababu ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, imetekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwa bahati mbaya kwa sababu nina *allergy* na rangi za kijani imebidi ni-*print*. Najaribu kuangalia, nimesoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi na naomba wananchi waelewe; kinachoongolewa hapa ndani ni utapeli mtupu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la kilimo. Hotuba ya Waziri Mkuu inaeleza vizuri kwamba kilimo kinaenda vizuri; idadi ya Watanzania zaidi ya asilimia 75 wanategemea kilimo.

Kimsingi kuna tatizo kubwa sana na ukiangalia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 - 2015 katika suala la kilimo wamesema jambo la kwanza ni kuhakikisha kwamba wanaanzisha Benki ya Kilimo yenye uwezo mkubwa ili ianze kuwakopesha wakulima wakubwa na wadogo kwa masharti nafuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki hiyo iko wapi? Nimeongea na Naibu Waziri wa Kilimo leo, anasema Bodi imeanza. Bodi ndiyo imeanzishwa, hakuna chochote. Huo ndiyo utapeli tunaousema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunasema kilimo ndiyo uti wa mgogo wa Tanzania, kwa bajeti ya mwaka 2014, fedha za ndani za kilimo ilikuwa Shilingi bilioni 25 wakati Kitengo cha *Protocol* cha mambo ya nje...

MWENYEKITI: Subiri Mheshimiwa, kuna Naibu Waziri wa Kilimo hapa!

TAARIFA

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Suzan Lyimo ni *collage mate* wangu na ninamheshimu sana. Ni kweli, nimezungumza asubuhi, alikuja hapa. Aliuliza Benki ya Kilimo imefikia wapi?

Nikamwambia Benki ya Kilimo inaanza rasmi tarehe 1 mwezi wa Saba na kwamba taratibu zote za kuanzisha zimeshakamilika na kwamba *top management* imeshaajiriwa, wafanyakazi wameshaajiliwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya kwetu Kilimo, Chakula na Ushirika alishaizindua Bodi yenyewe ya Wakurungezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wote tunajua kupitia Dirisha la Kilimo la *TIB*, mikopo imekuwa inatolewa na zaidi ya Shilingi bilioni 40 zimetolewa karibu katika kipindi kilichopita. Sasa

asiseme uongo kwamba Benki yenyewe iko wapi; wakati taratibu zote kimsingi zilishakamilika na mikopo inatolewa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Pokea taarifa.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo jadi ya wana CCM kuongea mambo ambayo hayapo. Mimi nimesema Ilani inasema kwamba Benki iwe imeanza na imeshaanza kuwakopesha. Hiyo Benki ya Kilimo ipo? Imeshaanza kukopesha? Ndiyo hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni jadi ya wana CCM, kuongea mambo ambayo hayapo. Mimi nimesema ilani inasema kwamba benki iwe imeanza na imeshaanza kuwakopesha wananchi. Hiyo benki ipo ya kilimo? Imeshaanza kukopesha? Ndiyo hoja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa nazungumzia suala la kilimo, mwaka 2014 fedha za ndani za kilimo zilikuwa Shilingi bilioni 25 za fedha za maendeleo. Wakati Kitengo cha *protocol* cha Mambo ya Nje ni Shilingi bilioni 50, lakini safari za nje peke yake ni Shilingi bilioni 24; na hapo bado suala la tezi dume lilikuwa halijaanza. Kwa hiyo, uniona ni jinsi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi isivyo na mipango thabiti!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuna janga kubwa sana la hali ya hewa, tukasema kilimo cha umwagiliaji ndiyo kitakuwa suluhisho. Tuna ekari milioni 29.4 za umwagiliaji; katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inasema kwamba katika hekta 300,000 ambazo mwaka 2010 walikuwa nazo, wataongeza zifike ekari milioni moja. Lakini tunavyoongea leo, hata ekari 600,000 za umwagiliaji hazijafika! Sasa huo kama siyo utapeli ni nini? Naomba Mheshimiwa Zambi asimame tena anipe taarifa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapozungumzia suala la kilimo, ni lazima Serikali ya Chama cha Mapinduzi itekeleze ilani yake! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda; hotuba ya Waziri Mkuu inaelezea, lakini Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilisema kwamba, ikifika mwaka 2015 viwanda vitachangia pato la Taifa kwa asilimia 15. Leo viwanda vina asilimia ngapi? Hata asilimia 10 haijafika, viwanda vyote vimeuawa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunategemea *general tyre* sasa hivi Watanzania wengi wana magari, kwa hiyo, kile kiwanda kingesaidia sana. Kiwanda kimekufa, ndiyo wanajidai sasa hivi wanakifufua. Tanzania ilikuwa namba mbili kwa *textile* ukiondoa *Egypt*. Sasa hivi Tanzania mtu akipata Shilingi milioni 10 anakimbilia China kwenda kuleta khanga na vitenge, wakati viwanda vyetu hapa vimekufa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza halafu Wabunge wa CCM, wanasema kwamba sisi tumechoka. Ninyi mmechoka! Tunasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni, lakini nyinyi ni kwa kunyongwa moja kwa moja. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua elimu ni uti wa mgongo wa nchi hii na Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikitamba kwa majengo, lakini nataka nikuhakikishie hakuna jambo baya kama kutowatimizia Walimu mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MEM2 na MES, ilikuwa kila mwanafunzi wa Shule ya Msingi apate Sh. 10,000/=, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari apate Sh. 25,000/=. Lakini leo tunavyozungumza, wastani wa Shule za Sekondari unakuta mwanafunzi mmoja hata Sh. 1,000/= haifiki. Wanafunzi wa *Primary* ndiyo hatusemi! Sasa mnategemea elimu ya nchi hii itakwenda vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni Mwalimu. Kwa mara ya kwanza katika nchi hii inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi, Walimu wetu wameshindwa kwenye *block teaching*. *Block teaching* kwa kawaida; najua wewe siyo Mwalimu, lakini mimi kama Mwalimu, tunatakiwa twende kwa wiki nane kwa mwaka na kwa miaka miwili wiki 16. *This time* wamekwenda kwa wiki mbili! Walikuwa wametengewa Shilingi bilioni saba, wamepewa Shilingi bilioni mbili, sawa na asilimia 28. Haya hapa majibu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa Walimu tunawapeleka wapi! Hili ni tatizo. Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inasema kwamba kufikia mwaka 2015 angalau kila Wilaya iwe na Chuo cha VETA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii, nadhani mwaka huu ndiyo Mkoa wa Kagera ambao ulikuwa umebaki ndiyo unajenga sasa Chuo chake; Mkoa huo! Wilaya, hazina! Lakini hii ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi! Sasa tusiposema mmechoka, tutasemaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wazee, hapa wametuambia, kufikia mwaka 2015 vituo 10 vya wazee vitapata magari 10, hebu niambieni, kuna kituo gani cha wazee kimepata gari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda na *data*, kwa sababu *no research no information, no data, no right to speak*. Kwa hiyo, naombeni mkija, mje na *research*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hotuba ya Waziri Mkuu, anasema vijijini asilimai 71, mjini 86; lakini katika ilani, naomba nisome; kutekeleza mradi mkubwa kufikisha maji katika mji wa Igunga, Nzega hadi Tabora kutoka Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana wakati Mheshimiwa Rage anauliza swali hapa, Waziri alijibu kwamba, naomba ninukuu, jana Waziri wa Maji anasema: "mkataba ndiyo utasainiwa, tarehe 15, Juni, halafu mchakato utanza mwezi wa Septemba." Lakini ilani yenu ilikuwa inasema maji yawepo tayari. Sasa tukisema ninyi ni matapeli, ni waongo, tunakosea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, naendelea na wazee. Mlisema kwamba hawa wazee watapata vitambulisho, watapata matibabu bure. Hivi kweli, kuna mzee amepata kitambulisho? Sasa hivi tuna wazee milioni mbili laki tano, wanatibiwa...

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Muda umekwisha!

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Na wewe Mshama, nyamaza wewe! *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante, muda wako umekwisha. Kengele ya pili Mheshimiwa Susan! Mheshimiwa Mkosamali! Mheshimiwa Sendeka, jandae.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nampongeza Mheshimiwa Susan hapa, ameeleza mambo ambayo ndiyo uhalisia, ndiyo ukweli na hakuna mtu wa kupinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza, kitu tunachofanya humu Bungeni ni kitu gani? Bajeti za ndani; fedha za ndani zinazokwenda kwenye Halmashauri kwa mijibu wa randama hii, asilimia 28; fedha za nje zimekwenda asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, tunakaa hapa, miaka mitatu minne, kila mwaka tunapitisha bajeti ambayo hamwezi kuitekeleza. Hivi mnadhani hata hao Wakurugenzi wa Halmashauri wanawaonaje ninyi! Hawa Watendaji wenu mliowaajiri ambao mnaitisha vikao hapa tunakaa, mkijua kabisa hamna uwezo wa kupeleka hizo fedha, mnataka Watanzania wawaelewe vipi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnatuita sisi hapa, tunatoka Majimboni tuje tupitishie bajeti ambayo mnafahamu hamna uwezo wa kuitekeleza. Hivi ni viini macho! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wakichagua CCM mwaka huu, nashauri tutafute *consultant*, tutafute *consultant* wa kupima uwezo wa kufikiri wa Watanzania. Kwa sababu mme-*fail everywhere!* Hakuna sehemu hata moja katika miaka yenu hii mnaweza kusimama hapa mkasema jambo hili tumelifanya vizuri kwa asilimia 100. Hili tumefavya vizuri! Hakuna hata moja! Mtasema barabara, lakini barabara ni mbovu. Mnatumia rushwa, nini, barabara miaka miwili imekwisha. Hakuna kitu! Mtasema maabara, sijui nini! Ninyi hamna uwezo wa kukamilisha maabara! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kupata shida nchi hii *deal* na mambo ya Serikali! *Deal* na Ofisi za Serikali, utapata matatizo makubwa sana! Ukitaka shida kwenye nchi hii, somesha mtoto wako kwenye shule ya Serikali! Ukitaka kupata shida nchi hii, nenda katibiwe kwenye hospitali ya Serikali! Ukitaka kupata shida nchi hii, panda ndege za Serikali! Nchi hii, wewe panda ATC uone kama hudondoki nayo! Mheshimiwa Buyogera alidondoka nayo juzi hapa, Kigoma! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yote ya Serikali, wakianzisha jambo, hakuna jambo hata moja, ninyi mnaweza mkafanya mkazidi *private sector!* Haipo! Maana yake ninyi ni kwamba Wizara ya Uchukuzi, mnazidiwa na Makampuni; maana yake Wakurugenzi wa *Precisions* na *Fast Jet*, wana akili kuliko ninyi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Serikali mshindwe kila kitu! Hapa mkisema ardhi mmeshindwa kupima; tumewaambia wapeni sekta binafsi, watapima. Hakuna kitu hata kimoja mnachoweza kusimamia. Haiwezekani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwanri, hapa nimekusikia asubuhi, unatuambia kwamba fedha za vijana na wanawake, unawakumbusha kwenye majibu yako kwamba Halmashauri ziendeleo kupeleka hizi fedha wakati ulishajibu hapo hapo Bungeni, ukasema Mkurugenzi ambaye hatapeleka hizi fedha tutamchukulia hatua. Ehee! Tuambie umeshachukua hatua gani? Huwezi kuwa ni Serikali, unatunga sheria, unapeleka miongozo, haifuatwi halafu unasema wewe ni Serikali! Serikali gani? *You guys!* Hawa watu jamani, nchi hii, Watanzania tunaomba mtuelewe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi wametudanganya hapa, wakati wanaanzisha haya mambo ya *Big Results Now* haya, wakatuambia kwamba hii *Big Results Now* kazi yake itakuwa ni

kufuatilia utendaji wa Mawaziri, tutakuwa na *performance contract* na nini. Sasa hii imekuwa ni *the Big Problem Now*. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mmetuambia Wizara ya Elimu ndiyo imekuwa namba moja; haiwezekani Wizara ya Fedha iwe ya mwisho, halafu kuwe na Wizara nyingine zimefanya vizuri. Huo ni uongo! Hizo Shilingi bilioni 29 ambazo mmezitumia kuazisha hiyo *Big Results Now*, kajengeni barabara. Jenga barabara! Huwezi kuanzisha kitu! Hii shida ni *unfunded budget!* Shida siyo kuanzisha vitu vya ovyo ovyo! Wizara ya Fedha mnatuambia mnakusanya fedha, kuna rushwa kwenye ukusanyaji wa fedha. Ninyi hamna uwezo wa kukusanya fedha vizuri bandarini, ndiyo maana akina Kagame wanawadharau, wanawaambia mkiwapa bandari wataongoza nchi na Tanzania itakuwa ni nchi ya mfano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmetudanganya, kule Kigoma mwaka huu ndiyo tunamalizia yale Majimbo matatu yaliyobaki. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara ya Nyakanazi kwenda Kigoma mmedanganya wananchi wa Kigoma toka mwaka 2005. Mkapa amedanganya, Kikwete amedanganya; sasa mwaka huu kule ndiyo hamlambi Jimbo hata moja! Hao akina Chiza muage! Muanze kuaga kabisa! Haiwezekani miaka hamsini na ngapi, sisi, eeh, ageni wazee! Wananchi kule hawataelewa! Haiwezekani miaka 50 mikoa yote mmekamilisha ujenzi wa barabara za lami, sisi mnatuletea hadithi! Mwaka huu kule Kigoma lazima kitaeleweka! Mtaishia kule! Yaani UKAWA kule ndiyo mpango mzima! Tunawakamua, mpaka mtajuta! (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili, tunafanya kazi ya kulidhalilisha! Huwezi kuja hapa unafanya kitu ambacho unajua ni *impossible*. Jana nimemshangaa sana hata Mheshimiwa Rais, anapita anakagua mafuriko; madaraja yaliyobomoka mwaka jana hayajajengwa mpaka leo. Hivi shida ni kukagua mafuriko au kazi ya Rais ni kupanga mipango kabla ya hivi vitu kutokea! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile siyo mvua! Majiji kama Dar es Salaam mlishindwa ku-*plan* toka miaka ya 1960, hakuna barabara mnazoweza kujenga pale lile likaonekana ni Jiji, haiwezekani! Mnatudanganya! Mliwaahidi watu wa Dar es Salaam mtajenga *flyovers* na nini, mmeweka wapi? Mmejenga wapi? Hii ni *total failure!* Mabasi yaendayo kasi; zile ni barabara! Mmejenga madaraja mabovu! Yaani ninyi kila kitu hakijakamilika! Hivi mnapata *consultant* wapi? Mnashauriwa na akina nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tuko na Waziri wa Utumishi, anatuambia nchi hii sasa hivi Watendaji wa Serikali uadilifu umeongezeka. Eeh, kutoka asilimia tisa kwenda asilimia 14.

Nikamwambia hivi wewe na hao Watendaji, sasa hivi haijulikani muda wa Wakurugenzi wa Halmashauri wa kukaa Ofisini ni upi. Ma-DC unakuta wanazunguka zunguka; wako kwenye vikao, wako huku wako huku; hivi hayo maadili, watu wanacheza na *Facebook* na *Twitter* Ofisini, muda wa kazi. Foleni imezidi, watu Dar es Salaam wanafika kazini saa 5.00 asubuhi, wanaondoka saa 7.00 mchana ili kuwahi foleni. Huo uadilifu, hivi ninyi mko *serious!* Mkoa okay! Mko sawa sawa? (Makofio/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Wagombea Urais wa CCM, hii Serikali imewamaliza. Acheni kugombea! Huwezi kugombea kwa Chama ambacho kimefeli, utajieleza nini? Utasimulia nini? Makatibu Wakuu Viongozi hawa, kazi yao ni kusafishana. Mtu hawezi kujiuzulu hapa; hawezi kufukuzwa na Bunge, halafu yule Katibu Mkuu anajifanya anajua, sijui nini, anakuja kusafisha watu hapa! Watu wetu wamekufa, wamenyanyaswa anakuja kusafisha watu. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wote waliojiuzulu, wote wana makosa. Huwezi kujiuzulu, hiyo ndiyo *principle!* Hamwezi kusafishana; mnasafishana nini? Kuna watu hapa walichangia jana, eti usafishe watu; hivi hapa utamsafisha nani? Hivi...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sendeka! Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya jiandae.

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya njema na kuliongoza Taifa letu hili kwa miaka 10 ya awamu ya nne ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kazi kubwa waliyoifanya kuliongoza Taifa hili katika awamu hii ya mwisho ya uongozi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakuwa mwizi wa fadhila pia kwamba unapozungumza mafanikio ya Serikali ya awamu ya nne, usipolitaja jina la aliyekuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Serikali ya awamu ya nne, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa kazi nzuri aliyofanya kwa miaka miwili ya Uwaziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mwenye akili timamu asiyekubali, labda uwe mwizi wa fadhila kwamba kazi aliyofanya Mheshimiwa Edward Lowassa kwa miaka miwili ni ya kiwango cha kupigiwa mfano na kwa maana hiyo na yeye ni sehemu ya mafanikio haya tunayoyaeleza kwa leo ambao baadhi ya watu hawataki kuyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuingia kwenye malumbano ya nani ambaye amesema vyema zaidi, iwe ni Kambi ya Upinzani au CCM, pale ambapo mambo yako dhahiri. Ni katika awamu hii tumeshukudia Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni - Mheshimiwa Mbowe, akisimama na kuiambia dunia na kuiambia Tanzania kwamba kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, katika uimarishaji wa miundombinu ya barabara ni kazi ya kupigiwa mfano na akampongeza Mheshimiwa Rais hazarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika Bunge hili tulishuhudia Wasemaji wa Kambi ya upinzani, wakati wa kujadili hoja ya Muswada wa Mabadiliko ya Katiba, wakisema hawajawahi kumwona Rais bora na makini kama Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Wakati huo kama mtakumbuka, wale wenye akili timamu na ambao hawasukumwi na msukumo tu wa utashi wa vyama, nilisimama hapa nikayashanga mapenzi haya ya dharura ambayo yaliibuka; nikasema, sifa moja ya mapenzi ya dharura, yana mchecheto lakini yana tabia ya kuchuja mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo wenzetu hawa walimsifia Mheshimiwa Dkt. Kikwete na mimi nilisema wakati huo Roho mwema aliwashukia, bahati mbaya sana sijajua roho wa leo ni wa aina gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema ueleze mafanikio ya Serikali ya awamu ya nne, ambayo kwa hakika sisi wote tumechangia, Wabunge wa CCM na Wabunge wa Upinzani tumechangia, kazi kubwa tuliyoifanya ya kuisimamia na kuishauri Serikali, hakuna anayekataa kwamba Mawaziri kedekede hapa wameachia ngazi kutokana na usimamizi mahiri wa Bunge

hili la awamu ya nne ya nchi yetu. Kazi hii haikufanywa na CCM peke yao; ina mchango wa kambi ya upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewaondoa Mawaziri madarakani, hatuwezi kusema tumewaondoa wenyewe. Wamewaondolewa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, tukiwa na Wabunge wa CCM na tukiwa na Wabunge wa Upinzani. Katika hili, tumefanikisha pia kupeleka fedha mikoani, katika Majimbo; kwa kutengeneza barabara, kujenga shule na kupeleka umeme vijijini. Imepitishwa na Bunge lenye Wabunge wa CCM na Wabunge wa Upinzani, hata pale siku nyingine walipoamua kunyosha miguu kutoka nje kwa kile kilichokuwa kinaonekana kama kususia. Lakini wao nao watakapokwenda kwenye Majimbo yao, wataeleza wamejenga hosptali, wamejenga barabara, wamejenga shule, lakini hayo tulipitisha katika Bunge ambalo takribani asilimia zaidi ya 78 wanatokana na Chama cha CCM. Hakuna namna ambayo ninyi sio sehemu ya mafaniko haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonishangaza ni pale ambapo ninyi wenyewe mnaonea haya yale mliyoyafanya na mnageuka kuwa wasanii wa leo kusema hamkufanya kitu, lakini kesho mnapokwenda kuomba kura, ninyi hawa hawa mtakwenda kusema nimefanya. Nataka kati yenu asimame mtu aseme kwa miaka mitano ya Ubunge wake, kwa miaka kumi ya Ubunge wake alikuja kupoteza muda hapa na kwamba kile kilichofanyika yeye sio sehemu ya mafaniko haya. Kama atatokea mtu mwaminifu wa kiasi hicho, itapendeza sana na Watanzania watakuheshimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu unahitimisha ngwe ya pili ya uongozi wa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na kuanzisha awamu nyingine ya tano ya Uongozi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika na Tanzania tuna changamoto nyingi na ambazo sote lazima tufikirie kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata viongozi wanaoweza kutusukuma katika kipindi hiki kingine. Changamoto kubwa tuliyonayo, Afrika na Tanzania ni kuhakikisha kwamba rasilimali za Afrika, rasilimali za Tanzania zinakuwa mikononi mwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais tunayemtarajia atakayepatikana, mgombea yeyote wa Chama chochote anayeota ndoto za kuliongoza Taifa hili, lazima awaeleze Watanzania kwamba rasilimali ni za Tanzania; Watanzania wanadai ukombozi wa uchumi, utakaoweka uchumi mikononi mwa Watanzania, utakaohakikisha gesi ni kwa Watanzania, madini yote yanakuwa kwa faida ya Watanzania na ukombozi utakaoweka misingi yote ya uchumi mikononi mwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue nafasi hii kuwaomba sana, kuikumbusha Serikali juu ya ahadi ya Shilingi bilioni 1.8 ambayo Mheshimiwa Rais aliahidi kuileta pale Orkesmet au Simanjiro kwa ajili ya maji ya vijiji vinavyozunguka Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro. Ahadi hiyo ni ya muda mrefu na leo nataka Waziri Mkuu atoe kauli juu ya hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia nitumie nafasi hii kueleza njaa iliyoko katika Jimbo langu, hali ya ukame ni kubwa, mvua haikunyeshwa, tunahitaji chakula haraka na kwa bei nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara ya KIA - Mererani iliyokuwa imepewa Mkandarasi asiyekuwa na sifa. Tunataka sasa Mkandarasi mpya aliyepewa, akafanye kazi ili barabara ya KIA - Mererani ijengwe kwa kiwango cha lami. Tunataka barabara inayotoka Arusha kupitia Mbauda, kupitia Komolo kuingia Orkesmet kuja Kibaya, kuja Kongwa ijengwe sasa kwa kiwango cha lami kama ambavyo iliahidiwa kwamba itajengwa kwa fedha za MCC II. Wananchi hawa wanasubiri barabara hiyo ijengwe haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme vijijini kuna maeneo ambayo kwa upande wa Kaskazini tulikopakana na Wilaya ya Monduli pale Lolkisale. Umeme umefika Lolkisale, nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba umeme ule uingie sasa katika Kijiji cha Nyorii, Emborei na Kijiji cha Leborsoi ili eneo la Simanjiro proper inayopaka na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire iweze kupata umeme huo wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuishukuru Serikali kwamba siwezi kuelezea vijiji ambavyo vimepata umeme; nataka kuelezea vile ambavyo havijapata umeme, kwa sababu vilivyopata umeme na ambavyo mkandarasi yupo site ni vijiji vingi. Kwa kweli kuelezea mafanikio ya Chama cha Mapinduzi kwa miaka kumi katika Jimbo la Simanjiro ni sawa sawa na kutakiwa kusoma Biblia kutoka Agano la Kale hadi Agano Jipya kwa muda wa saa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambieni, Chama cha Mapinduzi katika Wilaya ya Simanjiro imeshinda kwa asilimia 97, mmepata kijiji kimoja ninyi Wapinzani. Kuwaza kwamba mnaweza kuchukua Jimbo lile ni sawa sawa na kufikiria kuuangusha mgunga kwa kisu cha kukatia nyanya sokoni.

MHE. HALIMA J. MDEE: Baada ya kuengua!

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima anadai kwamba baada ya kuengua. Kuengua bado kutaendelea, lakini kura za CCM Simanjiro ile ni ngome ya Chama chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwahakikishieni kwamba watu wanaofikiri kwamba Majimbo...

WAHESHIMIWA WABUNGE: *(Waliongea nje ya microphone)*

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Achene kelele, ninyi ni watu wazima! Mtu mzima hovyoy! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ni chombo cha heshima sana. Unapona Mbunge anayepewa Jimbo ana-rap wakati Mbunge mwingine anajijuliza, hao ndio unatakiwa utafute washauri waelekezi wa kupima akili zao. Hao huwezi kutafuta washauri waelekezi wa kuja kupima akili za Watanzania; hilo ni tusi kwa Watanzania!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mhonga! Mheshimiwa Moza Abedi ajiandae.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Kwanza natoa pole sana kwa wananchi wa Mkoa wa Kigoma, nawaomba tu waendeleo kuwa watulivu na wavumilivu katika kipindi hiki kigumu cha kupokea wakimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba rai kidogo kwa Serikali, iziangalie sana Hospitali zetu, hospitali ile ya Mkoa, Hospitali ya Wilaya ya Kasulu na Kibondo na Vituo vya Afya mahali ambapo wale wakimbizi wanafikia kama Kagunga na maeneo ya Mwamgongo, tuongezewe

vifaa tiba na Wauguzi, kwa sababu kuna kipindi milipuko ya magonjwa ikitokea kwa wale wakimbizi wenyewe, yale mashirika ambayo huwa yanasaidia wakimbizi, ambayo yanatoa huduma za afya huwa wanalemewa, wanawakimbiza katika hospitali zetu. Kwa hiyo, naomba sana hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango wa kujenga hospitali ya Wilaya katika kituo kidogo cha Bitale pale, imemuliwa kwamba itajengwa hospitali ya Wilaya baada ya kugawanyisha hii Wilaya yetu ya Kigoma ambapo sasa hivi kunakuwa na Wilaya ya Uvinza. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali itupe utaratibu tumefikia hatua gani mpaka sasa? Kwa sababu michoro tayari na jengo la *OPD* limeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda harakahara kwa sababu nina mambo mengi kidogo. Nimeona hapa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu anasema kwamba asilimia 86 ya maeneo ya mijini yatakata maji na asilimia 71. Nadhani katika Mkoa wa Kigoma hiyo asilimia hatutaifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji ni kubwa na pale tunalo Ziwa Tanganyika. Kuna kampuni ambayo imepewa kazi ya ukandarasi inaitwa *SPECON* ilisaini mkataba toka mwaka 2013 mwezi Machi na walitakiwa wakabidhi kazi hiyo kwamba tayari iwe imeshakamilika kwa asilimia mia moja Machi, 2015.

Mpaka sasa hivi kazi iliyofanyika ni kujenga matenki peke yake. Yaani wako katika *thirty percent*, kwa hiyo, maana yake ni kwamba *70 percent* haijafanyika. Sasa tunataka kujua utaratibu mpaka sasa hivi ukoje na wanaamujaje kuhusu huyo Mkandarasi? Sasa hivi anasema anaji-*commit* kwamba atamaliza Novemba. Kwa hali ya kawaida hawezi kumaliza kwa sababu ameshindwa kufanya kazi hii katika kipindi chamiaka hii miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Kigoma Mjini, Ujiji, Igungu, maeneo ya Kisangani, Hospitali ya Mkoa kule, maeneo ya Meti, maji yanatoka mara moja kwa wiki na kuna maeneo mengine maji hayatoki kabisa; na bei ya maji kwa wale wanaouza wanapandisha kulingana na umbali wa sehemu. Kwa hiyo, tunaomba sana Serikali iangalie hilo na ituambie itafanyaje kuhakikisha kwamba na sisi tunakuwa katika watu wa mijini ambao wanapata maji kwa hiyo asilimia 86.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kwenda haraka tena, kuna tatizo la fidia. Kuna wananchi ambao waliondolewa katika eneo la Katosha ili *PTA* wajenge Bandari Kavuu. Najua kuna baadhi ya watu wameshalipwa ambao maeneo yao yalikuwa madogo. Kwa hiyo, kama asilimia 60 ya wananchi wamelipwa. Lakini wale wenye maeneo makubwa bado hawajalipwa, ni kama asilimia 40. Kwa hiyo, naomba nao walipwe haraka sana, *cheque* zao zitoke ili waweze kufanya maendeleo mengine kwa sababu wamesubiri kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna mpango wa *Kigoma Special Economic Zone* ambao ulipigiwa chapuo sana na Mkuu wa Mkoa aliyekuwepo Mheshimiwa Simbakalia. Maeneo yale watu walishaondoka na walilipwa japo kidogo, lakini yale maeneo yameachwa wazi, hakuna shughuli yoyote ambayo inafanyika. Kwa hiyo, kuna hatari kwamba inawezekana wananchi wakavamia yale maeneo na matatizo yakatokea. Kama mipango, imepangwa itekelezwe kwa wakati ili kuondoa matatizo ambayo yanaweza kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo lingine nyuma ya *Airport*, Rwanda, Ujiji eneo la *EPZ*, wananchi wanaendelea na shughuli zao pale, hawatakiwi kuendeleza lile eneo kwa kiwango kikubwa kwa sababu wanatakiwa watoke ili eneo hilo liweze kuchukuliwa na Serikali. Mpaka sasa hivi watu hawajalipwa. Wanauliza, watalipwa lini? Kwa sababu wameshaka muda mrefu wanasubiri! Bado kuna malalamiko ya watu waliotolewa pale eneo la *Airport*, wamelipwa fidia kidogo na madai yao Serikali nayo ilifanyie kazi hilo suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kwenye suala la barabara ya Kigoma – Nyakanazi. Nilikuwa Mbunge mwaka 2005 - 2010 nimelisemea sana suala hili; nimekuwa Mbunge tena mwaka 2010 - 2015 naendelea kulisemea hili suala. Inasikitisha sana! Mkoa wa Kigoma ni watu wachapakazi, hakuna hata siku moja tulishapelekewa chakula cha njaa. Tuna hali ya hewa nzuri! Sasa nashindwa kuelewa, kwa nini hamtaki kutuunganisha na Mikoa mingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kila mwaka huwa tunapangiwa pesa lakini huwa hazitolewi toka mwaka 2005 – 2010, hii ni kawaida. Mwaka 2010/2011 ilitengwa Shilingi bilioni sita, haikutolewa hata Shilingi. Mwaka 2011/2012 walitenga shilingi bilioni 2.3 haikutolewa hata sumni. Mwaka 2013/2014 tumetengewa Shilingi bilioni 3.5, haikutolewa, wakatoa Shilingi milioni 101. Mwaka 2014/2015 imetengwa Shilingi bilioni kumi, wanasema kwamba ni ya kutangazia. Inabidi tupewe *status*, imetolewa kiasi gani mpaka sasa baada ya miaka miwili ya bajeti kukamilika? Mwaka 2015/2016 naona kuna Shilingi bilioni 7.86.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua, kwa nini mnatuchezea akili wananchi wa Kigoma? Nakubaliana na maneno ya kama yangu hapa anavyosema kwamba mwaka huu hamtapata kitu kweli; na kweli hamtapata kitu! Tumechoka na tunasikitika sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo ninayosemea ni kama kilometa 300 tu kuanzia eneo la Kidahwe mpaka kufika Nyakanazi; ni kama kilometa 300 ndiyo ninayoisemea na nimekuwa nikiisemea muda mrefu sana.

Sasa pamoja na hilo, kuna barabara ambayo tunaweza tukaunganisha; ikiwa hii barabara ya Kigoma – Kidahwe - Nyakanazi ina matatizo, kuna barabara nyingine unaweza kupitia Kigoma – Manyovu; kuna mchepuko pale Manyovu – Buhigwe – Kasulu. Ie barabara tunaomba sana na yenyewe itiliwe lami kwa sababu itakuwa inatusaidia pale inapotokea matatizo katika barabara hii ambayo inatuunganisha sisi wote wa Wilaya zote tatu Kigoma, Kasulu na Kibondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwasemee kidogo wafanyakazi wa Reli, Maofisa na Maaskari. Wafanyakazi hawa wanaitunza reli siku zote na kwa sababu ndiyo usafiri ambao tunaategemea sisi wananchi masikini wa mikoa ya Kigoma. Wafanyakazi hawa wanadai nyongeza ya mishahara toka mwaka wa 2014 na pesa za masaa ya ziada na pesa za uhamisho na wengine wanadai hadi pesa za matibabu. Naomba kujua Serikali imefikia wapi kuwasaidia watu hawa ambao wamekuwa wakifanya kazi katika nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameongea pia suala la ajira kwa vijana; na akasema kwamba wametoa elimu kwa vijana 20,000. Vijana wa Tanzania tuko karibu milioni 16.5, unatoa elimu kwa vijana 20,000 halafu unatangaza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kwamba Serikali siku zote inaangalia wajasiriamali kwa kuwakopesha ndogo ndogo. Mimi naomba leo niongelee vijana waliosoma. Msomi hawezi kwenda dirishani kupewa mkopo wa Sh. 15,000/= maana mikopo inayotolewa ni midogo midogo, halafu akauze maandazi. Hebu tufikirie nje ya boksi. Tuangalie utaratibu mpya wa kusaidia vijana pia waliosoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mfano kada mbalimbali kama labda tuseme waliosoma sheria, *engineering* au kazi yoyote ambayo mtu anaweza akajijiri. Mfano *lawyers*, uwekwe utaratibu, vijana ambao watakuwa na *interest* ya kuanzisha *law firms* wapewe mikopo ya kuanzisha ofisi, ikiwepo na *grace period* kwamba labda ni miaka mitatu au minne ndiyo

waanze kulipa na *guarantee* itoke Serikalini, kwa sababu Serikali imekuwa ikitoa *guarantee* kwa wafanyabiashara. Hebu tuangalie pia na kwa wasomi ili tuweze kuwasaidia waweze kujijiri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, pia *engineers* wanaweza nao wakawa kwenye makundi, wakaweza kufungua ofisi wakafanya kazi za *private* labda katika suala la umeme, uhandisi labda wa majumba, magari na uchoraji. Inawezekana kabisa! Tuache kuwapa hiyo mikopo midogo midogo; hebu tuwafungue mawazo pia vijana ambao ni wasomi waweze kujiunga pamoja na kufanya vitu ambavyo vinaweza vikawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mengi, mengine nitachangia katika hotuba zinazofuata, lakini naomba nimalizie kwa kusema kwamba Ilani ya CCM namba 226 wanasema kwamba, "kimsingi utekelezaji wa ilani hii utafanikiwa kama Chama kitatekeleza jukumu lake la kusamamia kwa kuhakikisha kuwa programu ya utekelezaji inaandaliwa na kusimamiwa ipasavyo. Inawezekana kujenga maisha bora kwa kila Mtanzania; na Tanzania ni yenye neema tele kama uongozi wa sasa wa Chama utabadilika kiutendaji, kimsimamo na kintazamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamjabadilika na ndiyo maana matatizo ni mengi, mapato ni kidogo, matumizi ya anasa ni makubwa, tuna njaa inatukabili kila sehemu, wakati tunalima. Katika ukanda wa Kusini, mfano mikoa ya kusini mpaka kushuka huku kusini Katavi, kuna mahindi mengi sana lakini kuna maeneo mengine yana njaa, lakini kufikisha kule inakuwa ni tatizo kwa sababu hatuna hata miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshiwa Moza Said! Ajiandae Mheshimiwa Ngeleja.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la siasa katika nchi yetu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema katika nchi yetu, siasa ni safi. Nami nakiri kwamba siasa ya Watanzania waliokuwa wengi, wana imani na wana demokrasia iliyo ya ukweli kwamba wana imani, hakuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya hewa inazidi kuendelea mbele na kuendelea kuchafuka kwa sababu Chama kilichoko madarakani hakiamini kwamba kuna Vyama ambavyo vimekubaliana na vikakaa kwa pamoja vikasajiliwa na vikawa viko halali. Lakini leo hii tunashuhudia Serikali inatumikia siasa kwa kushirikisha vyombo vya dola kufanya vurugu kwenye mikutano ya wanasiasa. Vitu...

MBUNGE FULANI: *(Aliiongea nje ya microphone)*

MHE. MOZA A. SAIDY: Aah, we peleka huko! *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu kwenye Bunge. *(Kicheko)*

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde muda wangu. Naona watu wengine wanapenda siasa za ajabu ajabu! Sina vijembe mimi, nataka kusema ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapoleta Vyama vya Siasa, ujue vimeshirikiana kwa pamoja. Kwa hiyo, maana ya kuwa pamoja ni lazima tuaminiane na tupendane. Tusitumie vyombo vya dola kushirikisha kwenye mambo ya siasa. Tusidhalilisha Vyama vingine kwamba havifai, vyenyewe ndiyo vinafaa.

Sasa nataka kusema kwamba, huu ni wakati wa uchaguzi, kesho kutwa tunaendea huko mbele; naomba vijana wote na wazee na ndugu zangu wote wajandikishe kwenye daftari la kudumu. Mkoa wa Dodoma linaanza hivi leo, wajandikishe kesho linaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kucheza na siasa ni sawa na kucheza na maisha ya mwanadamu. Tunapoitumia siasa vibaya, itatuchezea vibaya sisi wenyewe. Nawaambia Chama Tawala kiache desturi hiyo, kwamba siyo nzuri, tutavuruga nchi yetu!

Mheshimiwa mwenyekiti, nije kwenye suala la usalama wa raia na mali zao. Tumeshuhudia mambo mengi katika nchi yetu. Ni kitu gani kinachosababisha vurugu na matukio mbalimbali ya wananchi kuporwa mali zao katika maeneo mbalimbali? Tunashuhudia mpaka hata benki; ina maana benki ikienda kuporwa iliyoporwa ni mali za wananchi. Vyombo vyetu wa dola vinashindwa kulinda mali za wananchi, vinashindwa kuwalinda hata Askari wao wenyewe. Sasa suala kama hili, tunaposema raia na mali zao na wakati huo huo bado kuna mauaji ambayo yanaendelea; mauaji ya *Albino*, tunawaona; tunashuhudia na hata ambao sio walemavu wa ngozi wanauawa, wanachinjwa, lakini Serikali inakuwa iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna vyombo vya dola vilivyopo, kuna mbwa hata wale wa kunusa wakatambua nani kaondoka na kiungo cha mtu au nani kashika damu ya mtu? Hivi vinakuwa viko wapi? Hao mbwa waliokuwa wanaotumikishwa hapa nchini, wanalishwa na wanatengewa gharama ya fedha, wanakuwa wapi kuwalinda wananchi wanaofanyiwa matukio mabaya katika nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la ajali za barabarani. Ajali za barabarani tutawalaumu sana Madereva, lakini hebu tuangalie miundombinu ya barabara zetu, ziko sahihi? Tutoke barabara hii ya Dodoma mpaka Dar es Salaam, ndipo palipokuwa na maafa makubwa yanatokea kule, mashimo utafikiri mtu kachimba chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapolaumu kwamba ajali za barabarani zinatokea kwa ajili ya madereva, nakataa; wakati mwingine dereva hawezi kusababisha. Je, tunaangalia vipuri vinavyoletwa, viko sahihi? Vinaletwa vipuri kutoka nje, nani anayevipima? Tunapima vyakula tu, *TBS*, sijui nini, lakini hivi vipuri, nani anavishughulikia kama viko sahihi? Leo unafunga kwenye gari na kesho unafika hapa na pale vinakongoroka, vinaharibika, ajali. Kisha mnasema dereva mzembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo, ajali hizi hizi za barabarani tunazosema, leo mmewawekea madereva *guarantee* wakalipie kila mmoja Shilingi milioni moja sijui kwa ajili ya kwenda kusoma, hapo hapo mnasema kwamba ajira kwa vijana mnaziongeza. Mnaziongezaje hizi ajira? Kama mnataka vijana hawa wajajiri wenyewe, ajira ambayo wanaweza kujajiri, toeni masomo haya bure, wakasome muwape vyeti ili waweze kwenda kujajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mtu anaendesha gari la *day worker* analipwa kutwa nzima Sh. 10,000/=, wewe uende ukamwambie akasomee alipe Shilingi milioni moja, atazitoa wapi? Hata hiyo Sh. 100,000/= ataitoa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihame kwenye suala hilo, nije kwenye suala la ajira kwa vijana. Serikali imetenga fungu la kusema, sasa tunaweza kuwawezesha vijana ili wajiwezeshe wao wenyewe. Lakini fedha zinazotengwa siyo kweli, mnaleta uchonganishi kwenye Wilaya zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tu katika Wilaya yangu ya Kondo, wanasema kwamba vijana wa bodaboda wamepewa Shilingi milioni tano, *Ukombozi Group SACCOS* wamepewa Shilingi milioni 4,420. Hivi kweli, Wilaya kama Wilaya ina watoto zaidi ya wanaozaliwa leo, wamemaliza shule, *Form Four* kesho, wanajijiri kwenye bodaboda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mmefikiri bodaboda ndiyo ajira? Au mnataka kutumaliza vijana wetu? Tengenezeni miundombinu mipya! Hebu njooni na mikakati mipya ya kiuchumi ili tuwawezeshe vijana wetu na kuwapangia programu iliyokuwa sahihi. Tuache kudanganya na kuuza roho za vijana wetu. Tusiwafanye ndiyo wingu kubwa la wapiga kura kwa kuwahadaa na kuwadanganya. Hata fedha hizi zinazosemwa hazijafika Wilayani kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la wanyamapori. Hivi tunasema tuna wanyamapori, hawa wanyamapori wanawafaidisha nini wananchi katika nchi yao ya Tanzania, au inawafaidisha wao wakubwa tu? Kumetokea matatizo makubwa kwamba Pembe za Ndovu zinabebwa, zinakamatwa. Zikifikishwa zinakofikishwa, hazijulikani zinapokwenda. Hatuambiwi zina gharama ya Shilingi ngapi, hatuambiwi zimekwenda wapi na hata ndani ya Vituo vyenyewe vya Polisi tunaambiwa zimepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tunaposema kwamba tuna wanyamapori, ndiyo tunaowatumikia basi angalau tupate fedha nyingi za kigeni. Lakini leo hii tunashindwa kujiendesha sisi wenyewe, matokeo yake tunaona fedha zinazokusanywa ndizo mnazokusanya ki-group cha watu wachache baadaye mnakuja kujigawia keshokutwa kwenye uchaguzi mwafanye wananchi kama kuku wa kienyeji. Naomba wananchi na Watanzania wote waanze kufikiria hilo na kugeuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye viwanja vya ndege...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngeleja! Jiandae Mheshimiwa Kheri Ameir.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wengine waliotayarisha bajeti hii ambayo mjadala wake unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja kwa sababu za msingi tu kama ambavyo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakizieleza. Moja, ni kuhusu mafanikio yaliyopo, pamoja na kwamba tunafahamu zipo baadhi ya changamoto ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuzamia kwenye bajeti hii, naomba kusema mambo machache ambayo namkumbusha tu Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wengine wanaohusika.

La kwanza, wiki mbili zilizopita Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema tulikuwa na Baraza la Madiwani. Katika mambo ambayo tuliyajadili na mimi mwenyewe nikatumwa kuja kumkumbusha Mheshimiwa Waziri Mkuu ikiwa ni sehemu ya utimizaji wa wajibu wangu, ilikuwa ni ombi letu la mji mdogo wa Sengerema kuwa Halmashauri ya Mji. Nimeteta naye jana, nimeongea na wataalamu, wameniahidi lakini naweka kumbukumbu wazi kwamba jambo hili tungependa Wanasengerema kupitia ufafanuzi utakaotolewa baadaye walisikie ili kuona hatua iliyofikiwa kuhusu ombi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kwa kuridhia Jimbo la Buchosa kuwa na Halmashauri yake siku chache zijazo. Hili ni jambo zuri na sisi kwa niaba ya Baraza la Madiwani la Wilaya ya Sengerema, tunaishukuru sana Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna ahadi ya miaka mingi kidogo ambayo aliahidi kutusaidia kutoka kwenye mfuko wake na kadri atakavyoona, Serikali kutuongezea uwezekano wa kuimarisha barabara zetu za mji mdogo wa Sengerema kwa urefu wa kilometa nne. Sasa ni ahadi aliyonayo, anaifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mambo tuliyozungumza kwenye Baraza letu la Madiwani ni ombi ambalo pia lipo Serikalini linafanyiwa kazi. Sisi pale Hospitali ya Wilaya ni hospitali ya Wamishenari, inamilikiwa na Kanisa Katoliki, lakini imepewa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya na sasa tunaambiwa kwa ngazi ya Mkoa imekuwa ni Hospitali ya Rufaa. Wataalamu wanajua hili jambo. Sasa tunafahamu utaratibu wa Serikali ni kuchangia kupitia ruzuku kwa kuwezesha *operations* za hospitali ambazo zinamilikiwa na watu binafsi, lakini zinapewa hadhi ya kuwa Hospitali za Wilaya.

Makubaliano ya awali ilikuwa ni kwamba, ruzuku iliyokuwa inatolewa ilikuwa inategemea vitanda 150 vilivyokuwepo katika Hospitali ya Wilaya ya Sengereza, lakini sasa vitanda vimeongezeka vipo 300, ndiyo maana tunaiomba Serikali izingatie kwamba inapofanya *calculations* zake kuhusu ruzuku ya Hospitali ya Sengerema, basi izingatie katika uwiano huo wa vitanda 300 na wala siyo 150. Haya ni makumbusho kwa sababu jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi na taarifa ninazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ziara zangu kule Jimboni, limekuwa likijitokeza swali, kwa sababu sehemu kubwa ya Wilaya au Jimbo la Sengerema ni ziwa. Sasa shughuli kubwa za kiuchumi mojawapo ni uvuvi unaofanyika katika Ziwa Victoria.

Moja ya kero ambayo imekuwa ikiwasumbua wananchi wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi ni kwamba zipo ndoano ambazo zinatumiwa kuvua Samaki, lakini mara kadhaa zimekuwa zikitamkwa na baadhi ya Watendaji wa Serikali kwamba ni haramu na mwananchi anapokutwa nazo anachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali limekuwa, hizi ndoani zinafikaje? Kwa sababu nyingi zinatoka nje ya nchi. Sasa Wanasengerema tunauliza, hivi ndoano zinazotumiwa kuvua Samaki, kama siyo halali kwa nini Serikali imekuwa ikiziruhusu ziletwe ndani lakini pia zilipiwe kodi? Haya ni mambo ambayo napenda kupata ufafanuzi.

Mwisho kutoka Jimboni ni kuishukuru Serikali, katika mgawo huu wa Walimu wapya Sengerema tumeletewa Walimu 463, ambapo Walimu 360 ni kwa ajili ya Shule za Sekondari na Walimu 103 ni kwa ajili ya Shule za Msingi. Tunaishukuru sana Serikali na haya ni majibu pia kwa kero ambayo imekuwa ikilalamikiwa na Watanzania wengi na hasa tunapokuwa tunajadili maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye kwenye bajeti, nizamie kwenye mafanikio, ni kwa nini naiunga mkono bajeti hii? Moja, Serikali ya Chama cha Mapinduzi siku zote imekuwa ikijielekeza na ina shauku kubwa ya kutatua kero za wananchi. Tunafahamu kwamba katika Ilani ya Uchaguzi kero namba moja kwenye Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni maji. Lakini tunafahamu pia juhudi ambazo zimekuwa zikifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sengerema tuna mradi mkubwa sana wa maji unatekelezwa wenye thamani ya Shilingi bilioni 23 na hii *figure* siyo ya bahati mbaya. Mimi natoa mfano kwa niaba ya wananchi wa Sengerema, kubeba hoja hii ambayo imekuwa ikisemwa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haizingatii kero za wananchi, hapana!

Kuna mradi mkubwa unatekelezwa wenye thamani ya Shilingi bilioni 23, tunaamini kwamba ni mradi mkubwa kuliko Halmashauri yoyote na ngazi ya Wilaya katika nchi hii, lakini hii inaashiria kwamba muda wote Serikali imekuwa ikihangaika kutafuta raslimali fedha kuwezesha utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule unakamilika mwishoni mwa mwaka huu na hatua zinaendelea kwa uzuri kwa sababu una hatua mbalimbali, lakini uboreshaji wa maji unatarajiwa kuwa umefikia mahali pazuri katikati ya mwaka huu. Sasa hili ni jibu kwa wale ambao wamekuwa wakihoji kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona upande wa elimu; hii ni mojawapo ya pongezi kwamba Serikali imefanya kazi kubwa. Mwaka 2005 wanafunzi waliokuwa wanakwenda Shule za Sekondari kati ya *form one* mpaka *form six* walikuwa ni 500,000 tu, leo tuna zaidi ya 1,700,000. Sasa haya ni mafanikio makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme, mwaka 2005 tulikuwa hatuzidi asilimia 10, lakini leo ni zaidi ya asilimia 30; na miradi mikubwa ya awamu ya pili itakapokamilika tutakuwa kwenye asilimia 40 na kitu kuelekea 50. Sasa hayo ni mambo makubwa yanayofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuzungumzia mitandao ya barabara za lami na hata zile za Mikoa ambazo hazijawekewa lami, lakini zilivyoboreshwa. Yote haya yanafahamika! Tumejimarisha kuona na hifadhi ya chakula ambayo ni jambo kubwa sana. Nchi yoyote inapokuwa na njaa, ni matatizo makubwa na mipango mingi ya maendeleo haiwezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia habari za mawasiliano kwamba leo Watanzania zaidi ya 32,000,000 wanatumia mitandao na matokeo yake tunaona kwenye miamala mbalimbali ambayo wanaitumia, inaboresha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia pia habari ya madini kwamba ushuru wa huduma unaanza kutozwa kwenye migodi ambayo tumeihangaikia toka miaka ya 2000 mwanzoni, lakini sasa hivi jambo hili limekuwa la kweli, Halmashauri sasa zinaongezewa uwezo kwa mapato yake. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba juhudi zinazofanyika zinazijengea Halmashauri zetu uwezo wa kuwa na raslimali nyingi za fedha na hivyo kuwaongeza kasi ya kuwahudumia Watanzania waliopo katika maeneo haya, lakini na ruzuku na mikopo nafuu kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri ni kwamba ajira kubwa katika nchi yetu inatokana na Sekta ya Kilimo. Mimi naungana na mikakati iliyosemwa na Serikali lakini tuendeleo kujikita katika hii ili tuliimarisha hili eneo. Reli na uwanja wa ndege Mwanza, tunafahamu umuhimu wa Mji wa Mwanza lakini pia ni kwa sababu ya eneo la kikanda jinsi lilivyo na vile vile mikakati ya kuboresha ajira. Nakubaliana na mikakati ya Serikali na hasa katika eneo linalohusu Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, ni jambo muhimu sana tujijimarisha. Mikopo ya wanafunzi ya elimu ya juu, ni jambo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Idd Azzan, wakati anachangia jana alisema kwamba Dar es Salaam sasa haipumui. Nilishawahi kuchangia na ninawakumbusha tena Watanzania wenzangu na naomba Bunge hili lizingatie kwamba Dar es Salaam inahitaji kupewa heshima na hadhi ya aina yake. Kama uchumi wa nchi yetu uko kati ya asilimia 60 karibia 70 uko pale Dar es Salaam, ni muhimu sana Jiji la Dar es Salaam likapewa hadhi ya kuwa Wizara, vinginevyo Watanzania wataendelea kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti uliyofanyika miaka miwili au mitatu iliyopita tunaambiwa kwamba mabilioni ya fedha yanapotea kwa Watanzania wengi wanaoishi Dar es Salaam kwa sababu ya foleni. Sasa katika mazingira haya ambapo mvua ikinyesha siku moja watu wanatumia masaa saba kwenda maafisini, tutafika wapi? Kwa hiyo, ombi langu ni hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma hotuba za Wapinzani, zimekuwa zikilalamika sana. Nasema niseme kwamba maelezo yanayotolewa ni kama vile nchi hii imesimama. Mheshimiwa Ole-Sendeka amesema, yote yanayofanyika sisi Wabunge tunahusika; lakini kubwa ni kwamba Benki ya Dunia mwaka huu mwezi wa Pili wametoa taarifa kwamba Taifa la Tanzania lipo kwenye mwendo, linatembea, halijasimama. Ndiyo maana leo Tanzania toka awamu ya nne ianze, wakati tunaanza sisi tulikuwa miongoni mwa nchi masikini sana duniani, yaani zile *top ten* masikini za nchi; lakini leo Tanzania siyo miongoni mwa nchi kumi masikini katika dunia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini? Ni ujumla wa mafanikio ambayo yamepatikana katika juhudi ambazo zimefanywa kupitia sekta mbalimbali likiwemo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, nawaomba wenzangu wanapozungumzia maendeleo yanayofanyika, tunafahamu kwamba changamoto hazuwezi kwisha ni kama kwenye familia, lakini ukweli ni kwamba Taifa la Tanzania linatembea na viashiria vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia habari ya uchumi kukua, lakini pato la Taifa linakua, umaskini unapungua, mfumuko wa bei unapungua na hata kiwango cha maisha, yaani namna ya kuishi (*Life Expectance*) imeongezeka; kwamba sasa hivi tuna miaka 61 siyo jambo dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wenzangu, Watanzania wanaendelea kusoma taarifa hizi zinazotolewa hapa Bungeni. Wenzetu wanavyolalamika ni kama vile Serikali ya Chama cha Mapinduzi haifanyi kitu. Lakini pia ukisoma hotuba za wenzetu, nami sitaki kupiga vijembe kwa sababu hapa tunabishana kwa hoja na kuangalia kama kuna mawazo mbadala. Kwa hiyo, naendelea kuwaomba Watanzania waendeleo kuiamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu wanachokiomba, wanataka Serikali ifafanue. Ukisoma hotuba za Upinzani hata Kiongozi wa Upinzani, anasema baadaye Waziri Mkuu atoe ufafanuzi wa hoja ambazo ameziulizia; lakini hakuna mawazo mbadala ya kusema katika changamoto zinazolikabili Taifa, wana mawazo gani mbadala ya kuisaidia nchi hii isonge mbele? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Watanzania wazidi kuiamini Serikali na Chama chake kwa sababu ina shauku kubwa, lakini kikubwa tunachowaomba wenzetu, kama kweli wana

dhamira ya dhati na wanadhani kwamba kinachofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi hakikidhi matarajio ya Watanzania, watuambie mbadala wake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo narudia tena... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Kheri Ameir.

Waheshimiwa Wabunge, inaelekea Wajumbe wengi wako nje, labda niwataje kabisa wachangiaji ambao watachangia mchana ambao ni Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Kheri Ameir, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Salim Turkey, Mheshimiwa Mtutura, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Highness Kiwia, Mheshimiwa Joyce Mukya, Mheshimiwa Prof. Kahigi na Mheshimiwa Christowaja Mtinda. Naomba kama wapo nje waingie ndani ili wapate nafasi za kuchangia.

Kama Mheshimiwa Ameir hayupo, basi namwita Mheshimiwa Akunaay!

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia nisimame leo kujadili hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kabla sijaanza, napenda kutuma salamu kwa wapiga kura wangu kwamba huu ni mwaka 2015 na ni mwaka wa uchaguzi na bado nipo imara na wanaopitapita katika sehemu hizo ni changamoto tu za Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kumpongeza Mheshimiwa Susan Lyimo kuonyesha namna ambayo Bunge linajadili Serikali iliyopo madarakani. Nimeshangazwa sana na Waheshimiwa Wabunge wa CCM kushindwa kufuatilia jinsi alivyozungumza Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba Wapinzani wamechambua Serikali imefanyaje kwa kutumia ilani yake. Sasa hiyo ni *yardstick* ya majadiliano na ndivyo inavyosema Katiba yetu Ibara ya 63(2)(a), (b) kwamba Waheshimiwa Wabunge kazi yao ni kuishauri Serikali, kuisimamia na kujadili bajeti yake. Sasa nashangaa Wabunge wa CCM wamechukua nafasi ya Serikali, badala ya kuihoji, wenyewe wanaitetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa sababu ya muda naomba niendeleo na kuunga mkono hotuba ya Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni na hotuba zake zote pamoja na hotuba ya Kamati ya TAMISEMI ambayo imechambua jinsi bajeti yetu ilivyokaa. Kwa hiyo, naungana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo kwa haraka haraka nitamke kwamba kuhusiana na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 hali halisi inaonyesha kwamba uandishi wa wapiga kura au kuboresha daftari la wapigakura hautaweza kumalizika kabla ya mwezi labda wa Tisa au wa Kumi. Kwa ajili hiyo, iwapo Serikali itang'ang'ania kutumia jinsi inavyofanya sasa hivi, tutakuwa na hali ngumu ya kwenda kwenye uchaguzi na itakuwa ni machafuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangazwa sana kuona Serikali inaagiza magari 777 ya Polisi na magari ya washawasha na mabomu badala ya kuweka hizo fedha katika utayarishaji wa uchaguzi wa mwaka 2015. Serikali hii ambayo tumesema kwamba imechoka, lakini siyo kuchoka tu, pia ina roho mbaya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014 Desemba, ilikuwa watu wakisimama tu wanapigwa bomu na kukamatwa, lakini tunaelewa kwamba ni maagizo yametoka Serikalini kwamba kikundi hicho ni cha upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niiambie Serikali kwamba mwaka huu yakiwepo mabomu kama hayo, wananchi wa nchi hii watafanya kitu ambacho siyo cha kawaida. Kwa hiyo, naishauri Serikali muwajali watu, kwani watu siyo ndege wala wanyama, haifai kuwapiga mabomu na risasi na kuwaua hovyoy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwenye uchaguzi, labda nigusie pia kura ya maoni kuhusu Katiba inayopendekezwa. Iwapo Uchaguzi Mkuu matayarisho yake yanademadema hivi: Je, hiyo kura ya maoni ya Katiba itasaidia nini? Naishauri Serikali iachane nayo mpaka huko baadaye Uchaguzi Mkuu utakapofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imesema imefanikiwa katika kutengeneza ajira. Ajira katika nchi hii haiwezi kutengenezwa kwa sababu hakuna viwanda. Kwa hiyo, wanafunzi au watu wanaotoka vyuoni waliosoma *faculty* zao mbalimbali hawawezi kuajiriwa kwa sababu hakuna viwanda. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba iangalie viwanda kwanza, viwanda vianzishwe, hata wawekezaji wanaokuja wachambuliwe wale ambao wanaleta viwanda ili tupate ajira. Ajira ikipatikana, ndiyo pato la Taifa litakua na TRA kodi zake zitapatikana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *deficit* ya bajeti, nakisi ipungue au iondolewe kabisa ikiwezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie juu ya watumishi wa Halmashauri. Mwaka 2014 au 2013 tulirekebisha Sheria ya Utumishi ya mwaka 2002 tukaruhusiwa tuajiri katika Wilaya watu wa kada ya chini yaani VEOs, Madereva na Watumishi wa Ofisini. Sasa ile sheria imetuletea tatizo kwa sababu nia yake ilikuwa ni kutafuta wafanyakazi wa Halmashauri wa daraja la chini katika eneo husika. Lakini sheria imeleta kikwazo kwamba lazima ajiriwe mtu yeyote anayetoka mahali popote Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kama pale Mbulu tunataka kuwajiri watu walio karibu, tutakuwa tunafanya ukabila. Sasa tumefanya nini na tunafanya nini? Iwapo wakati ule tulikuwa tunaondoa gharama za kumleta mtumishi kutoka mbali wa kum-*reallocate* kwa ajili ya *leave*, tunaomba Ofisi ya Waziri Mkuu itoe maelezo kwamba ile sheria inatumaje? Sisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu tulitangaza ajira ya Watendaji wa Vijiji 20 lakini baada tukashindwa kuajiri kwa sababu sheria inasema wale wanaotoka mbali na Baraza la Madiwani wanataka kwamba wale waliokuwepo pale wajiriwe. Tunaomba tupate maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa Serikali za Mitaa hasa Wenyevitwa wa Vitongoji na Vijiji ni taabu katika sehemu mbalimbali hapa nchini kwa sababu hakuna fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Madiwani wetu watastaafu kama Waheshimiwa Wabunge, watamaliza muda wao; Serikali imetaka Halmashauri ilipe *gratuity* kwenye fedha za ndani. Hii tunaona itakuwa ni ngumu, tunaomba Serikali Kuu iwalipie *gratuity* Madiwani wetu kama wanavyolipwa watu wengine *gratuity* na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie ahadi ya Rais aliyoitoa katika Wilaya ya Mbulu. Rais Jakaya Kikwete mwaka 2005 aliahidi kwamba Serikali itajenga daraja moja linaloitwa Daraja la Magara, ikatoa fedha, Shilingi milioni 600 lakini fedha ile ikapigwa juu kwa juu haijafika kwenye lile daraja. Mpaka leo hilo daraja ni matatizo, daraja ambalo linaunganisha

Tarangire na *Lake Manyara*. Kwa hiyo, tunaomba Serikali basi kama hamna fedha watuletee daraja la *barrier bridge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia wakati anafungua Barabara ya Minjingu – Singida, alitangza kwamba barabara ya Karatu – Mbulu – Haidom itawekewa lami na Serikali yake kabla hajamaliza muda. Sasa imebaki miezi michache kabla ya muda wa Serikali hiyo kumalizika. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awaambie watu wa Mbulu, Karatu, Haidom mpaka Meatu kwamba hiyo barabara itakuwapo au ni hadithi ya Alinacha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji katika Wilaya ya Mbulu katika vile visima kumi imekwama kutokana na fedha za *World Bank* kutopatikana, hasa miradi ya Tumati Mongai, Harsha na Haidom, tunaomba Serikali ituambie kama hayo maji yatapatikana au hayatapatikana.

Jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni bajeti. Bajeti hii ambayo inaisha mwezi wa Juni, TAMISEMI mpaka sasa Wilaya yangu imepata asilimia 18 kwa *release* ya Desemba, 2014. Mwaka huu inaonesha kwamba bajeti ya maendeleo nayo itakuwa kwenye asilimia 20 na kitu. Sasa iwapo itakuwa kwenye kiwango hicho, wananchi wetu watakuwa wanaumia sana kwa sababu wanabuni miradi, wanaanzisha lakini Serikali haileti fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, miaka mingi tumepewa fedha za bajeti kwa ajili ya maabara, hazikuonekana mpaka Mheshimiwa Rais akaja akasema na yeye kwamba mpaka wa Sita maabara ziwe zimejengwa. Sasa hizo maabara zimeleta balaa kwa sababu Wakuu wa Wilaya wanakamata Watendaji wanawaweka ndani kwa sababu fedha hazipatikani. Sasa kama wananchi ndiyo hawana fedha, ni kwanini hao Watumishi watishiwe na Wakuu wa Wilaya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inadai kwamba ina *rule of law*, hakuna chochote, kwa sababu Mkuu wa Wilaya anatoa amri zake, Waziri anatoa amri yake, Rais anatoa amri yake yote ni mchanganyiko. Sasa tunaomba kama nchi inatumia *rule of law* basi itumike.

(Hapa kengele ya pili ililia)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Rebecca Mngodo na ajiandae Mheshimiwa Godfrey Mngimwa.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa muda nami niweze kuzungumza. Kwanza kabisa, nataka kusema kwamba nimesoma kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa kusema kweli ni hotuba nzuri sana, sijawahi kuona hotuba nzuri kama hii. Lakini ukiondoa macho katika hotuba, ukaiangalia nchi katika hali halisi, ni vitu viwili tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kabla sijaendelea sana, niongezee pale alizpozungumzia Mheshimiwa Susan Lyimo kuhusu Ilani ya CCM. Ilani ya CCM ilisema kwamba, ili kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, mtajenga *flyovers* katika makutano ya Ubungo na pale TAZARA. Sasa nata kujua, hizo *flyovers* ziko wapi? Mimi niko katika Kamati ya Miundombinu; ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa nyumba mlisema kwamba mtajenga nyumba 15,000 kwa maana ya nyumba 3,000 kila mwaka ili wananchi waweze kuwa na nyumba za kuishi. Lakini ukweli ni kwamba mpaka sasa ni *fifty percent* tu ndiyo imeshakamilika, nikimaanisha kwamba ni jumla ya nyumba 7,547. Hata hivyo, nyuma hizo zinajengwa kwa gharama ya juu sana kiasi kwamba kunakuwa na matabaka ya watu; wanaoweza kuishi

kwenye hizo nyumba ni wachache na wengine hawawezi ku-afford hizo nyumba. Sasa tungependa kujua, ziko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuendelea nizungumzie kuhusu tabaka. Tunaposema CCM imeshindwa jamani, haijaanza leo. Ni process, ilianza kushindwa zamani, isipokuwa katika awamu hii ya nne huko kushindwa kumejidhihirisha zaidi. Kwa kutumia ujanja ujanja wametengeneza matabaka katika nchi yetu. Tabaka ni mfumo mbaya sana wa kibepari ambao mabepari walikuwa wanautumia kututenga sisi wananchi; walio nacho na wasio nacho ili waendeleo kututawala. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianza na upande wa ardhi. Tarehe 25 Juni, 2014 Mheshimiwa Waziri Mkuu hayuko hapa, lakini ningependa kusema kwamba niliingia Ofisini kwake hapa Dodoma na hiyo ni baada ya kupigiwa simu na wananchi kutoka Kikuletwa Shambarai Burka na kuletwa Msitu wa Mbogo kwamba wangukuja kumwona kuhusu shamba la *Karangai Sugar Estate* ambalo lilikuwa limefutiwa umiliki na Mheshimiwa Rais Mkapa ili liingie mikononi mwa wananchi. Kwa sababu ya kutengeneza tabaka, shamba lile linamilikiwa na watu wachache na wengine wamo humu humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefika pale Kikuletwa nikaangalia, karibu ekari 500 zinamilikiwa na Mheshimiwa Lazaro Nyalandu na anawakodisha wanawake wajane kwa Sh. 250,000/= kwa kila msimu wa kulima. (Makofi)

MBUNGE FULANI: *Shame!*

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tabaka! Serikali ya CCM imetengeneza matabaka; wawekezaji uchwara wakiwatesa Watanzania waendeleo kukodisha ardhi na wao wakimiliki maeneo makubwa huku hawawezi kuyatumia. Matabaka ni mfumo mbaya sana. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri Mkuu aliniambia kwamba wewe ondoka, akanyanyua simu kumwomba *Secretary* kwamba anapiga simu Arusha ili lile shamba lirudishwe kwa wananchi mara moja. Nikaamini mia juu ya mia, nikajua kwamba wananchi wa kule Meru watarudishiwa ardhi. Mpaka sasa ninapongea hapa ndani ya Bunge, wananchi wanaendelea kuteseka, wanakodisha ardhi yao wenyewe kutoka kwa wawekezaji uchwara ambao nimewataja na baadhi yao wako humu humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, migogoro ya ardhi iko mingi na wananchi mnaonisikiliza, wote ambao mna migogoro ya ardhi, nawaombeni tarehe 25 Oktoba siyo mbali, ni lazima tui-*delete* CCM kwa sababu wametudanganya kwa muda mrefu na wametutengeneza matabaka, siyo katika ardhi tu, lakini niseme hata katika elimu. Hakuna kitu kibaya kama matabaka katika elimu. Kwa sababu unapoweka matabaka katika elimu, ndiyo pale tunapona wanafunzi wengine wanatembea kwa miguu wamebeba madumu na mifagio wanaenda mbali shuleni na wakifika kule wanakaa chini au kwenye mawe; lakini tabaka lingine linapanda basi la shule wamebeba mabegi yao mazuri mgongoni, wakifika shuleni pia kuna chakula, wanakalia madeski na wanajifunza kutumia *computer*. Lakini lile tabaka la wanaokaa kwenye mawe, wanafundishwa *computer* kwa kuonyeshwa picha tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabaka! Hakuna kitu kibaya kama tabaka katika Taifa. Mmetengeneza ubaguzi ili mwendelee kuwanyanyasa wananchi na kuendelea kuwapa vizawadi wakati wa kampeni! Nawaomba wananchi safari hii msikubali kupokea zawadi ndogo ndogo, ni udhalilishaji! Tunadhaliisha wananchi kwa kuwapa zawadi ndogo ndogo. Kwanini tusiache kabisa kuwapa watu rushwa kwa kuwapa zawadi ndogo ndogo za khanga, vitambaa

na vilemba eti kusudi wakuweke madarakani halafu baadaye unawasahau, umewawekea matabaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matabaka haya yapo hata katika mfumo mzima wa utoaji afya. Maisha ya mijini na vijijini ni kama mbingu na ardhi, hayafanani! Mwanamke anayezalia chini na mwanamke anayezalia kwenye kitanda karibu na kiyoyazi na mtungi wa oxygen uko karibu naye ili tatizo lolote likitokea aweze kuokoa maisha yake. Tanzania ya leo! Ndiyo maana CCM mkiambiwa mmeshindwa jamani, mkubali. Ni lazima muangalie alama za nyakati! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu asiyejua Chama cha Kikomunisti cha Urusi ambacho *one night* kilianguka mwanzoni mwa miaka tisini. Wala hakikuangushwa na Chama cha Upinzani, ni kwamba na chenyewe kilikuwa kimechoka kama ninyi mlivyochoka. *One night* kilisambaratika! Chama ambacho kilikuwa kinaongoza nchi kubwa kama Urusi, ilipokuwa ikijivuna kwamba iko karibu sawa na Amerika, lakini kilisambaratika *one night*. Ni vizuri mkaanza kujiandaa kisaikolojia kwa sababu tarehe 25 ndugu zangu siyo mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matabaka ya watu wanaotibiwa katika hospitali ambazo hazina dawa na wengine ambao wana tiketi mikononi wanangoja kwenda India, hao ndiyo wengi.

MBUNGE FULANI: Marekani!

MHE. REBECCA M. MNGODO: Wengine Marekani; matabaka!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika maji, nashangaa sana kwamba, CCM mmeshindwa kutumia ubunifu; nyakati kama hizi za mvua, Halmashauri zetu zingeweza kujenga matanki makubwa ya kuvunia maji ili wananchi wasiteseke kuliko kuendelea kutegemea ufadhili wa *World Bank*, ninyi wenyewe mngelitahidi kufanya ubunifu ili wananchi wavune maji, lakini hata hilo limewashinda ndugu zangu. Ni lazima mjue kwamba wananchi wa sasa hivi sio kama wale wa zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii katika ukurasa ule wa 31, nimesikitika sana kwamba Wamachinga wamesifiwa katika hiki kitabu! Eti ajira kwa vijana! Eeh! Imeandikwa kwamba hapa Tanzania vijana ni milioni 16.2 halafu milioni 15 wamejiajiri katika biashara ndogo ndogo. Machinga! Kitabu cha Waziri Mkuu kinasifia Machinga? Vijana wamekosa ajira, wanatembeza biashara ndogo ndogo mnawatangazia kwamba eti ni maendeleo! Hata mkopo watachukuaje sasa wakati biashara ndogo ndogo wanayoifanya ni ya kutembea kuanzia asubuhi mpaka jioni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmeweka matabaka na siamini kabisa kwamba kama mtaendelea kukaa madarakani baada ya tarehe 25 Oktoba, mtaweza kuleta maendeleo yoyote kwa sababu mmeshindwa kwa muda mrefu na haiwezekani kwamba sasa hivi mtaweza tena. Kwanza ninyi wenyewe mmeshaanza migogoro ninyi kwa ninyi kama ile ile iliyokuwa kule katika Chama cha Kikomunisti ambacho nimewapa mfano wake. Mfano huo naufahamu vizuri maana hiyo siku ambayo hicho Chama kinasambaratika, nilibahatika kuwepo Mjini Moscow, kwa hiyo, nilishuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna matabaka pia katika wizi. Kuna wanaoiba fedha nyingi eti wanaombwa warudishwe; tena wanabembelezwa kwamba warudishe. Lakini kuna vijana wetu wakiiba kitu kidogo, hata tunda tu, wanapigwa na kuchomwa moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza hapa mwanafunzi mmoja wa Chuo Kikuu wiki mbili zilizopita, watu wakidhani kwamba ni mwizi kumbe alikuwa na matatizo ya akili kwa kukosa mikopo, wazazi wake ni masikini akawa amechanganyikiwa akatoroka akakimbia. Hii ni habari ya kweli. Kijana huyu alipigwa mpaka akavuliwa nguo kwa kuhisiwa ni mwizi. Lakini wanaoiba fedha nyingi, hawafanywi kitu chochote...

MBUNGE FULANI: Tuko nao humu humu!

MHE. REBECCA M. MNGODO:...badala yake tuko nao humu humu ndani na wengine wanabembelezwa tu warudishe; na kusema kwamba Shilingi milioni 10 ni kama fedha ya mboga tu. Ndugu zangu, nawaambia wananchi nikijua wananisikiliza kwamba kwa kura yako wala usidanganyike safari hii kwa kupewa zawadi ndogo ndogo, ni lazima mkatae. Hamna kusema sijui... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, wajiandae Mheshimiwa Highness Kiwia, Mheshimiwa Joyce Mukya na Mheshimiwa Margareth Mkanga.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu; vilevile niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wasaidizi wake wote, Mkurugenzi wangu na Uongozi wote wa Chama na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamekuwa wakizungumza masuala ya Serikali iliyochoka ambayo haifai. Mimi niko hapa kuhakikisha kwamba wananchi na Watanzania kwa ujumla wanapata nafasi ya kuujua uongo unaoongelewa katika Bunge lako. Vilevile napenda kuwataarifu Watanzania kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inarudi tena tarehe 25 mwezi wa Kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu zifuatazo: mimi kama kijana, naongea hivi kwa sababu najua ni nini ambacho Serikali imefanya kwenye Jimbo la Kalenga na Majimbo mengine hata hayo ambayo yanashikiliwa na Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nitoe ushahidi kadhaa ambao unadhihirisha kwamba Chama cha Mapinduzi lakini vilevile Serikali kwa ujumla inarudi. Nilipokuwa naingia kwenye Jimbo la Kalenga kulikuwa na Kata 13, sasa hivi tuna Kata 15. Katika hizi Kata 15 kulikuwa na saba tu zilizokuwa na umeme. Leo hii Jimbo la Kalenga lina Kata nyingine nane ambazo zina umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata hizi nane kuna Wapinzani ambao tuko nao mle ndani, wanaangalia zile nguzo na kila kazi inayoendelea. Leo hii wanakuja wanasimama wanasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijafanya chochote. Sasa hawa watu tunawapima kwa uwezo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia mtu mwingine amekuja anasema tunahitaji *consultant*; *consultant* kwa ajili ya nini? Nadhani wao ambao wanashindwa kuangalia hata nguzo za umeme, mwanadamu ambaye anashindwa kuangalia hata nguzo za umeme, nadhani yeye ndiye anahitaji huo ushauri, tena tumkodie mshauri mzuri hasa ambaye anaweza akatazama uwezo wake wa kufikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata zifuatazo kuna nguzo ambazo tayari Serikali imeishamwaga. Kuna Kata ya Maguliwa, Lyamgungwe, Mgama, Wasa, Maboga, Ulanda na Kiwele. Bado Wapinzania wanasema nao wana uwezo wa kuchukua Serikali. Jimbo la Kalenga tumewagaragaza kwa asilimia 99 mwezi wa Kumi na Mbili na mwaka huu tunawakaribisha ili tuwagaragaze zaidi. Nadhani hiyo itakuwa inatosha. *(Makofi)*

Jambo lingine najua maendeleo ni hatua ambayo ni lazima ifuatwe, kama vile ambavyo nchi nyingine zilizotajwa zilikuwa na maendeleo. Tuna Vijiji vya Kiperu na Tagamenda ambacho tunahitaji Serikali iendelee kufanya utaratibu wa kuwaletea umeme katika vijiji hivi viwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya kwenye Jimbo langu la Kalenga, hususan kwenye masuala ya miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara ya Isakalilo kuelekea Ipamba Hospitali ambayo tayari imeishawekwa lami. Sasa hivi wananchi wa Jimbo la Kalenga tunapita pale na magari yetu vizuri, wale wanaopita na baiskeli safi, tunaendelea tu kuteleza, hamna tatizo! Sasa hawa wenzetu ambao wanapita juu na ma-chopper sijui wanaonaje chini maendeleo ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayafanya. *(Makofi)*

Vilevile ningependa tu kugusia maeneo machache ya barabara ambayo pia ningependa Serikali iendelee kuweka mkazo. Kuna Barabara ambayo inatoka Kalenga kuelekea Kiponzelo moja kwa moja mpaka Wasa. Barabara ile imekuwa ikifanyiwa utaratibu wa kutengenezwa, lakini tunaomba Serikali iendelee kufanya kazi ya ziada ili kuhakikisha kwamba barabara ile inakuwa katika hali nzuri. Pia ningependa kupiga kelele kwenye suala la barabara inayotoka pale Kalenga kuelekea Kidamale katika Kata ya Nzii. Barabara hiyo ni nzuri na Kata ile ya Nzii ina biashara nyingi na kilimo cha hali ya juu. Kwa hiyo, ningependa sana Serikali ifanye utaratibu tuweze kupata lami pale ili tuhakikishe tunaendelea kukidumisha Chama chetu na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Katika suala la miradi ya maji katika Jimbo langu la Kalenga ipo mingi na Serikali imefanikisha miradi kadhaa. Kuna miradi ya Weru, kuna mradi mwingine uko Kiwere, Mwambao na mwingine unaitwa Igangidung'u. Miradi hii tayari imekamilika na wananchi wangu wanasubiri tu bomba zifunguliwe waanze kuoga vizuri na kujimwagia maji safi. Hiyo ndiyo kazi nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaendelea kuifanya. Naomba tu labda kwa kugusia kwamba Serikali iendelee kuwaangalia na kuwatazama vizuri Wakandarasi wetu ambao bado malipo yao yamekuwa yakisuasua. Naomba sana Serikali iweze kutazama ni namna gani inaweza ikawalipa Wakandarasi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala ya mawasiliano, Serikali yetu imefanya kazi kubwa sana, siyo katika Jimbo la Kalenga tu, ila vilevile katika Majimbo mengine mengi sana. Nilikuwa nikiingea na Mheshimiwa Moses juzi tu hapa, akasema pia katika Jimbo lake mambo ni safi; sasa ninashangaa sana anaponiambia kwamba haiwezekani Chama cha Mapinduzi na Serikali yake...

TAARIFA

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulipa Bunge lako taarifa kwamba, hayo anayozungumza Mheshimiwa Mgimwa kwanza sijakutana naye nikazungumza naye.

Pili, kama ana ushahidi, namtaka athibitisha mahali hapa. Wananchi wangu wana matatizo kibao yakiwemo ya maji, barabara mbovu, Serikali imeshindwa kutekeleza na ndiyo maana tunasema Serikali imechoka.

MWENYEKITI: Ahsante. Endelea Mheshimiwa Mgimwa.

MWENYEKITI: Ahsante, endelea Mheshimiwa Mgimwa!

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hiyo taarifa siipokei lakini vile vile kuthibitisha ni kwamba, Mheshimiwa tuliongea jana na ukathibitisha hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu kwa kugusia katika masuala haya ya mawasiliano labda niendeleo kidogo, Serikali imefanya kazi kubwa sana kwenye Jimbo langu kuna mnara wa simu ambao tayari umewekwa ambao ni mnara wa Tigo kwenye Kata ya Nzii katika Kijiji cha Magubike, mnara huu unafanya kazi na ni kazi nzuri ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, hakuna mjadala hapo, wananchi wangu kule sasa hivi wanainua simu na wanapiga vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna mnara wa simu wa VODACOM ambao uko pale Kata ya Mgama unaendelea kujengwa hiyo ni kazi nzuri sana ambayo sikubaliana na masuala ambayo yanaongelewa hapa kwamba Chama na Serikali yetu imechoka, je, itachoka vipi kama minara tunayo? Pia inachoka vipi kama *Viettel* imeshapita katika sehemu mbalimbali katika Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi huo na barabara na wao wanapita pia Wapinzani. Kwa hiyo, hilo lisiwape taabu sana Watanzania, hawa ni watu ambao ni kama watoto wanaonyonya, wataendelea kuwa katika utaratibu huu mpaka baadaye watakapokuwa tutawaachia nafasi, lakini baada ya miaka mia hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya afya ni ya muhimu sana, niliongea kipindi kilichopita kuhusu hospitali ya Ipamba. Ningependa suala hili tuliangalie kwa jicho la huruma sana kuhakikisha kwamba Hospitali hii ya Ipamba ambayo inahudumia wananchi wengi sana, katika Jimbo langu na hata wengine Iringa Mjini pale ipatiwe gari la kubebea wagonjwa, tuna tatizo kubwa sana ningeiomba sana Serikali tuweze kupata gari hili ambalo litakwenda kusaidia wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa jana na Mheshimiwa Ritta na mimi naligusia tena kuweka msisitizo kwamba hata Mheshimiwa Mbunge aliyepita marehemu Dkt. William Mgimwa alilizungumzia sana hili. Nami pia nachukua nafasi hii kuendelea kuwakumbusha tu Serikali kuwa tunahitaji sana suala hili liweze kukamilika ili tuendeleo kuhakikisha kwamba Chama chetu na Serikali inaendelea kupeperusha bendera katika Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo moja ambalo nalipata kwenye Jimbo langu, tatizo hili ni la kilimo. Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu, lakini vile vile kilimo kinagusa sana wananchi wa Jimbo la Kalenga kwa sababu kwa asilimia zaidi ya 95% wanategemea kilimo.

Ningependa sana wananchi wangu waweze kupata masoko, mahindi yao mwaka jana msimu uliopita yameharibika kwa kiasi kikubwa sana kwa sababu ya ukosefu wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda sana Serikali iweze kutazama hili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata masoko ya kutosha waweze kuuza na vilevile tuweze kusaidia NFRA kuhakikisha kwamba uwezekano mkubwa wa kuhakikisha kuwa wananchi wanauza bidhaa zao na kuhakikisha kuwa wanapeleka watoto wao mashuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mkanga, wajiandae Mheshimiwa Highness Kiwia na Mheshimiwa Joyce Mukya!

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii. Kwanza niishukuru na kuipongeza Serikali kwa dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo ya nchi hii ikifuatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mpinduzi ambacho ndiyo kimeshika Serikali. Serikali hiyo kiutendaji ikiongozwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Pinda na Mawaziri wake wote kwa ujumla ndiyo katika utendaji wao wamechagua kufanikisha haya ambayo yameandikwa kwenye hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *summary* nzuri, yaani mtu ukikaa kwa makini ukaisoma kwa kweli unaona tumesonga mbele, kwa sababu kila mahali wamesema tulikuwa hivi tuko hapa, tulikuwa hivi, tumesogea hapa. Sasa nashangaa watu tunaposema kuwa hakuna chochote kwa sababu hatua hizo hata kama ni kidogo zimeoneshwa humu ndani ya Hotuba, kwamba hiki tulikuwa hapa tumesogea hapa na ndugu zangu niseme maendeleo yoyote ni hatua, siyo kitu cha kuamka leo ukasema tumeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani niseme ni mwongozo wa yale mliyodhamiria kama nchi kuyatekeleza, yanaweza yakatekelezeka kwa wakati huo na mengine ikawa ni mwendelezo. Ninachokijua sasa hivi Chama cha Mapinduzi yale ambayo bado hatujatekeleza ndiyo yanaingia kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka wa 2015/2020, kwa sababu ni mwendelezo wa mambo haiwi tu kukurupuka, ni mipango ambayo inaweza kufanikiwa kuteketeleza kwa wakati ule au baadaye kidogo. Sasa tunapolalamika kila kitu kingekuwa, jamani hata Mungu alichukua muda na mpangilio wa kutuumba, sijui alianza na nini, anajua yeye lakini kwa utaratibu wake aliouamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, wananchi hilo wala lisiwatishe kwa sababu maendeleo ni hatua, unaanza na moja, unasogea, ukirudi nyuma ndiyo usikitike, lakini kama unasonga mbele ndiyo maendeleo yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na utangulizi huo mdogo niwashukuru sana wanawake wa Morogoro Mkoa ndiyo walionileta mimi hapa kwa kutumia maarifa na utashi wa Chama cha Mapinduzi kwamba hata akinamama wenye ulemavu wanaweza kitu kwa kweli niwashukuru akinamama wale ambao wameteteleza Chama chetu kilivyofikiria kwa upande wa mambo ya kisasa kwamba tunapaswa kuwa na wawakilishi ambao watasemea mambo ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Serikali imetuunga mkono sana kusikiliza hoja na changamoto na malalamiko ya wenzetu wenye ulemavu wa aina zote. Ushahidi ni kwamba

mwaka jana Serikali na hapa niwashukuru Wabunge wote waliniunga mkono katika kurekebisha kifungu kile cha nani watakaokuja kushiriki ndani ya Bunge Maalum.

Serikali ikakubali na Wabunge mkatuunga mkono wakaja 120 humu ndani, ndiyo ninaunganisha na kilichosemwa ukurasa wa 71 mpaka 72, kuhusu nia ya Serikali kushirikisha watu wenye ulemavu kisiasa, kijamii kwa kweli pale mlionyesha nia ya dhati kabisa, kwa sababu mlitekeleza lile, nalo hilo ni baya? Nalo hilo Serikali hapo tutailaumu? Sisi tunaishukuru kwasababu walikuja na wakachangia na mlishuhudia hapa wale ambao waliamua kuwepo humu ndani hata kwa kusikia basi. mlishuhudia jinsi ambavyo walitoa michango yao ili kufanikisha Katiba pendekezwa kwa lengo kwamba baadaye nchi itaendelea kwa misingi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kuwa changamoto haziishi, lakini Chama cha Mapinduzi na Serikali yake imejitahidi kufanya mengi na yaliyobaki itaendelea kuyafanya kwa sababu mwaka huu mbona kinashinda na mbona yataendelezwa kwenye Ilani yake? Hilo wala sina wasiwasi, labda kupungukiwa, lakini kushinda Ikulu, Ikulu kinaingia Chama cha Mapinduzi, jamani tukubali tusikubali, hata kama ni Urusi imelinganishwa hapa bado hatujafikia stage ya Urusi hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa Mwalimu wa historia *Perestroika* ile imefanya kazi nikiwa nafundisha na kuelewa, haikuwa hivyo. Ukurasa wa 71 na 72 umekiri kwamba Serikali inatambua kwamba, watu wenye ulemavu ni lazima watambuliwe, waheshimiwe na nini. Niseme hivi, kwa muda huu hali hiyo nzuri imeanza kujionyesha pamoja na kwamba bado kuna changamoto na kama nilivyosema ni hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa inatia matumaini kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ina dhamira ya dhati kabisa kuendeleza kundi hili, lakini kielimu nashukuru *enrolment* ya watoto wenye ulemavu inaongezeka na kwamba kila shule sasa wamelazimishwa au wameelekezwa kuwa na vitengo vya watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali jinsi Serikali ilivyoona.

Kwa hiyo wapo wanaosoma na bado wanaendelea kujikongoja, lakini naomba juhudi za miundombinu katika maeneo haya ya shule ziongezoke, kwa mfano, pesa za chakula kwa sababu aina nyingine ya ulemavu wasipokula hawawezi hata kusikiliza kusoma, zipelekwe kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye ulemavu ni kama watu wengine na hapa tumekiri kabisa lakini bado kuna changamoto ya suala la matibabu, Serikali ilishaweka kwamba angalau watu wenye ulemavu ambao hawajiwezi kabisa waweze kutibiwa bure, hili bado halijatekelezwa naiomba Serikali na hata hiyo ijayo ya Chama cha Mapinduzi, hili tuondokane nalo liweze kutekelezeka sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujiwezesha ni muhimu na watu wenye ulemavu ni lazima wawezeshwe kwa sababu wanasadia kuchangia maendeleo ya nchi hii, lakini katika suala la mikopo bado kuna changamoto, Taasisi nyingi haziamini kwamba tunaweza kukopesheka, lakini hebu jaribuni tunaweza kukopesheka, wanajiunda kwenye vikundi lakini bado hawaaminiwi katika kukopeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hali ya uwezeshaji wa namna hii, nashauri kwamba tuna Mifuko mingi sana ya uwezeshaji wananchi hapa nchini, basi hawa wenzangu wawe *concentrated* sana kwenye ule Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Mfuko ule wa Wanawake kwa sababu huko ndiko kuna wenye ulemavu vijana na kuna wenye ulemavu akinamama, wapate kufikiwa huko. Hii Mifuko imekuwa mingi inachanganya, lakini hii miwili tukiitilia nguvu

hili kundi litaweza kufaidika humo, kwa sababu katika kukopeshwa kwake hawaambiwi sana dhamana sijui nini, hapana, hiyo mingine mara dhamana, mara nini, itaweza kuwa ngumu lakini hii miwili naomba iongezewe nguvu kusudi watu wenye ulemavu waweze kupata hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wazee, bado malalamiko yapo hasa kwenye upande wa matibabu, maeneo mengine lile dirisha lililoamriwa kuwa liwepo halitumiki vizuri, hebu hili tulirekebishe kwa sababu hawa walitumika walipokuwa vijana na sasa ndiyo wameishiwa nguvu na sisi sote tunakwenda huko huko, mradi mtu akipata uhai, unakuwa mzee na wewe. Kwa hiyo, wafikiriwe zaidi au lihimizwe zaidi hili dirisha wakati wa matibabu ili waweze kutibiwa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo niandamanishe na pensheni, pensheni ongezeeni wazee hawa jamani wanaumia. Kuna niliyekutana naye kabla sijaja hapa anasema, mimi nilikuwa mfanyakazi imara kweli, sasa pensheni yangu nilianza na shilingi 4,000 jamani, ikapanda ikawa ni 21,000, yaani inauma kwa sababu unamwona kabisa kuwa alikuwa ni mtendaji mwaminifu sana. Hili tuendeleo kulitafakari na kulfikiria na kuweza kuwawezesha wenzetu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mahakama kuna wazee wa Mahakama wanaosikiliza kesi kidogo kidogo, nako huko hatujafanya vizuri sana. Tujitahidi sana kuwalipa kwa wakati ili nao waendeleo kutoa busara zao katika utoaji wa haki pale ambapo inawabidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nilikuwa nimefikiria kukizungumzia hapa ni ajira. Ajira ni tatizo na kila Mbunge hapa tumelisema hilo, kujajiri au kuajiriwa, lakini katika kuajiriwa ni lazima usome. Hili naliomba kwa watu wangu hawa hawa wenye ulemavu, kuna ambao wameweza kusoma, mpaka siku hizi kuna wenye *degree* na *PhD* Maprofesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wale wanaokidhi vigezo tuweke kabisa utaratibu kwamba, wawe ndiyo wa kwanza kupata ajira za Serikali, maana kujajiri nako ni ngumu, kama hawapewi mkono inakuwa ni ngumu, lakini angalau tuweke utaratibu kabisa kwamba hawa ambao wanakidhi vigezo vya ajira wapewe *priority number one* kuajiriwa, ndipo wafuate wengine wenye uwezo wa miguu, macho na vitu kama hivyo. Vinginevyo hata wale waliosoma tutawaacha nyuma na hawa wakijitegemea jamani, wanasaidia familia zao. Kwa hiyo, hilo naliomba sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Kiwia, wajandae Mheshimiwa Mtutura na Mheshimiwa Turkey.

MHE. HIGHNESS S. KIWIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kwenye mjadala huu ambao unaendelea mbele yetu. Kazi yetu sisi Wabunge ni kuishauri Serikali na hasa sisi Wabunge wa Upinzani kazi yetu kubwa ni kuikosoa Serikali, kuishauri pale panapohitajika kushaurika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana kwamba yale yote yanayosemwa na Wabunge kutoka Upinzani yanaonekana kuwa hayana msingi na hayana tija. Niwashauri Wabunge wa CCM, mnaweza mkatuchukia sisi, lakini msichukie hoja za Upinzani. Hakuna namna mnavyoweza kushindana na ukweli, ukweli huwezi kupingana nao, ukweli unafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijafanya kitu, siyo kwamba haijafanya kitu kabisa, tunachosema hapa ni kwamba ukiangalia

umri wa uhuru wa Taifa letu, ukiangalia fursa tulizonazo kama Taifa na ukiangalia hali ya maisha ya Watanzania, hapo ndipo tunaposema Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijafanya kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana jioni wakati Mheshimiwa Christina Lissu anachangia alizungumzia juu ya suala la namna ambavyo chombo kikuu tunachokitegemea kusambaza (MSD) madawa nchini kinavyotetereka na kinavyodhoofika kutokana na madeni ya Serikali. Hata hivyo, jambo la kusikitisha na hapa ndipo tunaposema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni chovu na imechoka, Naibu Waziri anasimama anasema kwamba Mheshimiwa Christina Lissu analipotisha Taifa, MSD iko imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Naibu Waziri nimekuwa naye kwenye Kamati ya Huduma za Jamii kwa zaidi ya miaka miwili na nusu na mara zote MSD malalamiko yao makubwa yalikuwa ni deni la Serikali. Leo hii Waziri anasimama na kusema kwamba MSD wako imara, ni kweli wako imara, lakini wanaodhoofisha MSD, chombo kikuu cha usambazaji wa madawa nchini ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka jana MSD walikuwa wanaidai Serikali bilioni 102. Najjuliza maswali hivi huyu Naibu Waziri amepatikana vipi? Hivi wanatumia vigezo gani kuwachagua hawa watu? Nchi nzima tunafahamu changamoto kubwa tuliyokuwa nayo katika hospitali zetu ni madawa kuanzia Zahanati, Kata mpaka hospitali za Mikoa na za Rufaa, leo Waziri anasimama hapa anasema kwamba MSD wako imara tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kwenye hotuba ya Waziri tunazungumzia suala la kujenga Zahanati na vituo vya Afya nchi nzima hizo Zahanati zitatu watu vipi kama hakuna madawa? Huyu Waziri sijui amekula maharage gani huyu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nasimama kuzungumza hapa, kwenye Jimbo langu la Ilemela tuna mradi wa ujenzi wa hospitali ya Wilaya, lakini kwa miaka hii mitano, program ya bilioni tatu kiasi cha pesa ambacho kimetolewa ni shilingi milioni 300 tunakwenda wapi? Halafu tunaipongeza Serikali kwa lipi? Programu ya shilingi bilioni tatu unapeleka milioni 300 ifanye nini? Halafu tunazungumzia kujenga Zahanati na vituo vya afya nchi nzima, hii haikubaliki. Tunaposema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni wachovu ni kwa sababu tuna ushahidi na tuna vielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anakuja hapa analidanganya Taifa hata kwenye Hotuba yao watakyoileta hapa bado watalalamikia deni la MSD. Wakati Waziri anakwenda kuhitimisha, watueleza ni namna gani wanakwenda kulipa deni la MSD ili tuwe na madawa katika hospitali zetu kuanzia Zahanati mpaka hospitali za Wilaya. Naomba ku-declare kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikizungumzia juu ya suala la kusaidia vijana na wanawake na suala hili la 10% kwa ajili ya vijana na wanawake ni suala la kisheria. Tukiwa kwenye Kamati tumetembea nchi nzima katika mikoa mbalimbali, hakuna mkoa ambao umeweza kutenga 10% kwa ajili ya vijana na wanawake. Leo Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi inatuambia kwamba, ina dhamira njema kwa ajili ya vijana na wanawake wa nchi hii siyo kweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha hata ile Mikoa, hata zile Halmashauri ambazo zina Wabunge ambao ni Mawaziri, zimeshindwa kutenga 10% kwa ajili ya vijana na wanawake dhamira ya kusaidia wanawake na vijana iko wapi? Ukiangalia Bajeti hii kwa undani wake ni mwendelezo ule ule wa bajeti ya kisani, mwendelezo ule ule wa bajeti tegemezi, ni mwendelezo uleule wa bajeti feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi pesa ambazo zimekwenda katika Halmashauri zote nchini ni 23% kwa ajili ya miradi ya maendeleo, watafanya muujiza gani wa kufikia 100%? Tusidanganyane, leo hii hakuna Taifa ambalo lina mipango mingi kama Taifa la Tanzania. Nchi hii mipango tuliyonayo kama tungeifanyia kazi, tungekuwa tumefika mbali, tatizo la Serikali ya Chama cha Mapinduzi linajenga nchi hii kwa kauli mbiu, Kilimo Kwanza, Kilimo Mbili tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye taarifa ya Waziri, TAMISEMI inaonesha kwenye Mfuko wa Barabara pesa ambazo zimeshakusanywa mpaka sasa kwenye Halmashauri ni 50%. Wabunge wanasimama hapo hapo wanaipongeza Serikali. Hii asilimia 50 utafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Ilemela nimekuwa nikizungumza mara zote kwamba Halmashauri ni changa, haina uwezo wa kukarabati barabara zake kutokana na uchanga wake na nimekuwa nikiomba itengwe pesa kutoka Mfuko wa Dharura kwa ajili ya kukarabati barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyozungumza hapa, barabara zimekatika kutokana na mvua. Waziri Mkuu naomba unisikilize! Tunayo barabara ya kutoka Kiseke kwenda Buselu kwa Mkuu wa Wilaya. Barabara hiyo imekatika, ilikuwa inahudumiwa na TANROAD. TANROAD imerudisha kwenye Halmashauri ambayo haina uwezo nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikaa kikao cha Bodi ya Barabara tukakubaliana kwamba barabara hiyo iendelee kuhudumiwa na TANROAD. Naomba umwagize Meneja wa TANROAD aende akaunganishe barabara ile kuondoa adha hii kubwa ambayo wananchi wangu wa Ilemela wanaipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ya kusahau kwa umuhimu wake, naomba nimkumbushe Waziri Mkuu kwamba, ilimchukua miaka miwili kuweza kutatua migogoro ya Madiwani. Kata zangu tatu zilikosa uwakilishi wa Udiwani, kwa sababu tu Serikali ilishindwa kutangaza uchaguzi na ikashindwa kurejeshea Udiwani wao. Pamoja na kutatua mgogoro huu, naomba nimkumbushe Waziri Mkuu bado mtoto wao ambaye ni Mayor, Matata bado yupo pale.

Mheshimiwa Waziri Mkuu unafahamu kwamba Matata hakuchaguliwa kihalali na kazi anayofanya ni kuharibu maendeleo ya Halmashauri yetu ya Ilemela. Nikuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu mje Ilemela mchukue mzigo wenu, nguvu ya umma inakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wote wa Tanzania na Jimbo lako la Ilemela, nimeingia kwenye Ubunge nikiwa na Wenyeviti wa Mitaa minne, leo nimechukua Mitaa 70 ya CCM. Naomba niwaambie Watanzania, CCM tunaipa miaka 50 na hata tukiiiongeza miaka 50 mingine haiwezi kufanya kitu. Maana si tu kwamba imeshindwa na imechoka, ime-fail. Wafanya maamuzi magumu. Dawa ya nyoka si kuchuna mbuzi, dawa ya nyoka ni kupiga kichwa.

Wajitokeze kwa wingi katika zoezi la kupiga kura na katika uchaguzi ujao wapige kura za kutosha, wasiwe na wasiwasi. Chadema tunajipanga tutazidi ku...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mtutura, wajiandae Mheshimiwa Salim Turkey na Mheshimiwa Mwanjelwa!

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza kabisa nimshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyeweza kunijalia afya na kuweza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja kwamba CCM imechoka. Ninachotaka kuwaambia hao watani wetu kwamba CCM haijachoka na CCM haitachoka, sana sana ninachoweza kuwaambia kwamba hatunywi sumu, hatujinyongi, ila CCM ni mbele kwa mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi kwamba CCM haijachoka na haitachoka, nitachukua takwimu chache tu, hasa za Idara ya Elimu. Wakati Mheshimiwa Rais Kikwete anakabidhiwa madaraka kulikuwa na shule za msingi 14, 257 mwaka 2005. Mwaka huu wa 2015 shule za msingi ni 16,538. Mwaka huo udahili wa wanafunzi shule za msingi ilikuwa ni 7,541,208, wanafunzi wa msingi waliodahiliwa mwaka huu ni 8,202,892.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu mwaka 2005 walikuwa 135,000, sasa Walimu wa shule za msingi ni 190,957. Shule za sekondari udahili wa wanafunzi walikuwa 100,745, sasa hivi wameshafikia 400,753.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu wa shule za sekondari, mwaka 2005 walikuwa 20,754, sasa hivi Walimu wa sekondari ni 80,529. Nyumba pamoja na madarasa mwaka huo ilikuwa ni 5,795, sasa hivi nyumba na madarasa ni 49,882.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maabara kipindi anapokea madaraka, maabara zilikuwa 247, sasa hivi tuna maabara za sekondari 2,329, ongezeko la zaidi ya asilimia 500. Sasa unasema ongezeko la zaidi ya asilimia mia tano unasema mtu amechoka?

Ndugu zangu Watanzania tuendeleo kuiunga mkono, kukosoa ni kazi nyepesi sana na ndiyo maana kila siku huwa nasema katika nchi hii kuna haja ya kufanya *specialization*. *Specialization* ya CCM ni kuendelea kuwa madarakani, kuwatumikia Watanzania. *Specialization* ya wenzetu Wapinzani ni kuandamana, kuzomea, pamoja na kukosoa na kulaumu hata jambo ambalo na wao wenyewe wanaliona kwamba lipo dhahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi Jimboni kwangu hususan jambo la kilimo. Tumekuwa na mahitaji ya pembejeo hasa zao la korosho na mazao ya chakula, lakini kwa Wilaya yetu ya Tunduru ambayo uzalishaji wa korosho umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka, kuna haja kubwa ya kuiangalia Wilaya hii kwa macho mawili. Kwa sababu, mikorosho ya Tunduru kuna ile ambayo inafufuliwa, lakini vile vile kuna mikorosho mipya inapandwa. Kwa hiyo, ongezeko la korosho kwa hekari na mikorosho kwa idadi ni kubwa sana, kuliko maeneo mengine yote katika nchi yetu. Tunaomba Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza ruzuku katika *sulfur*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa soko la korosho. Bado naunga mkono mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani, lakini sio kama inavyoendeshwa sasa hivi. Sasa hivi mkulima analipwa nusunusu, jambo ambalo sivyo lilivyoielezwa katika stakabadhi ya mazao ghalani, haielezi hivyo.

Kwa hiyo, naomba uandaliwe mfumo ambao mkulima atalipwa fedha zake zote hata kama kupitia mfumo huu wa stakabadhi ya mazao ghalani, lakini kupewa nusunusu kwa kweli hilo sitaweza kuliunga mkono, kwa sababu sio siri, hata sisi hapa Wabunge posho zetu zikichelewa huwa inatokea sintofahamu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima anauza korosho zake, anakaa miezi mitatu, miezi minne hajalipwa. Ni kumcheleweshea maendeleo yake na kumdhalilisha kwa sababu nyumba

yoyote ambayo baba mwenye nyumba hayupo vizuri kiuchumi, heshima ya nyumba hiyo huwa inapungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wanyama waharibifu. Hivi karibuni kumekuwa na mlipuko mkubwa sana wa wanyama waharibifu hususan hawa tembo. Wanasumbua sana katika Kata ya Nemasekata, Kijiji cha Nemasakata yenyewe, Kijiji cha Amani na Kijiji cha Changamoto. Mpaka jana orodha ya wananchi ambao mashamba yao yameshashambuliwa na tembo, wanafikia arobani na nane. Sielewi mpaka leo hali itakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali, itumie nguvu zake za ziada kuhakikisha kwamba tembo wale wanafukuzwa haraka sana katika eneo lile ili tusije tukawalazimisha wananchi wakatamia ujuzi wao wa asili kujilinda wao wenyewe. Naomba sana katika hili lifanyike vizuri. Vile vile baada ya wanyama hao kufukuzwa, naomba timu ya watu wa kutathmini waende haraka wakatathmini ili wananchi hawa ambao wana tishio la njaa sasa hivi waweze kulipwa fidia haraka iwezekanavyo, ili waweze kununua chakula kutoka kwa wananchi wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais, aliyekuwa Waziri wa Nishati kipindi kile alitangaza kwamba Vijiji vyote vilivyopimwa katika Jimbo la Tunduru Kusini vitapata umeme mpaka kufikia Juni. Naomba sana Waziri aliyeshika nafasi hiyo ajaribu kuwasiliana na mimi ili tuone ni namna gani suala hili linatekelezwa haraka iwezekanavyo kabla ya mwezi huo Juni ili wananchi waendeleo kuiamini Serikali yao na kuipenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Watanzania kwamba kule Tunduru hatuna wasiwasi. CCM itashinda kwa asilimia kubwa na hizi kelele kelele zinazopigwa hapa sisi kule wala hatuhangaiki. Narudia tena, hatunywi sumu! Hatujinyongi! CCM ni mbele kwa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Turkey, wajiandae Mheshimiwa Mwanjelwa na Mheshimiwa Vicky Kamata!

MHE. SALIM ABDULLAH TURKY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunijalia mie fursa hii. Awali ya yote, nataka nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhana Wataala* kwa kutujalia sisi tuliokuwa hapa salama salmin na waliokuwa na maradhi Mwenyezi Mungu awape wepesi wa kupona na waliodharurika, Mwenyezi Mungu azijalie dharura zao ziwe nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wote kwa mafuriko yaliyotokea katika nchi yetu na hususan katika Jimbo langu la Mpendae kuna wananchi wengi wameathirika na mafuriko haya, Mwenyezi Mungu awape subira, *inshallah* muda si mrefu Mbunge wenu atakuja kukutembeleni rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake na Mawaziri kwa ujumla kwa hotuba nzuri waliyoileta hapa ni mipango waliyotoka nayo na wanayotaka kuendelea nayo. Mwenyezi Mungu awajaalie wapate *istikama* ya kuweza kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata tabu moja, mara nyingi sana hapa Bungeni mimi si mzungumzaji, lakini lugha hii ambayo inazungumzwa kwamba CCM imechoka leo imenifanya nami kidogo nikohoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wapinzani ndugu zetu, namshukuru Bwana Highness amezungumza ukweli mmoja ambao Mwenyezi Mungu amhidi awe mkweli siku zote, kwamba kazi yao kubwa ni kutukosoa, lakini unapokuta shilingi imeviringwa katika kinyesi tabu kuikota. Sasa na wao wanavyotukosoa, hawatukosoi kwa lugha za kistaarabu, lugha zao zinakuwa mbaya mno. Sasa ndiyo maana hapa panakuwa uwanja wa mapambano. Badala ya watu kutoa hoja tukajenga nchi yetu inakuwa sasa vijembe vitupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili nataka niwaambie, wao wanapenda sana kuzungumza kwamba *business as usual*, mie toka nimeingia Bunge hili, sijaona sera zao zaidi ya wao kusema CCM haiwezi! Aibu kubwa sana, wao wanatuambia hatuwezi, wameshindwa hata kusoma *order paper* ilikuwa pale wakajua kwamba nani achangie na nani asichangie. Leo mtu kama huyu ukimpa nchi si ataiweka juu chini! (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, watu hawa hawaaminiki hata siku moja, watabaki kazi yao kupiga kelele. Na toka tumeingia wao wanasema wataenda Ikulu, mtu anakwenda Ikulu mwaka wa kwanza, hebu niambie unaendaje mwaka wa kwanza Ikulu, uchaguzi miaka mitano? Sasa angalau lugha hizo wakizungumza kipindi hiki wataelewewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapiga kelele bajeti hii haijatekelezeka, haiwezi kutekelezeka, kwa sababu watu wanaopinga bajeti hii ni wao namba moja. Kwa sababu wanatafuta sababu ndogo, badala tukakaa wenyewe tukaelekezana tufanye nini humu ndani, wao watatoka wakazuie misaada ya nje, jamani mfanye hivi mfanye hivi! halafu wanazunguka wanasema hatusaidiwi. Mmeshafamu! Sasa hilo ni fitina kubwa ya nchi hii na bajeti hii haikutekelezeka kwa sababu ya Wapinzani hakuna mwingine. Hayo ndiyo yao, ukiwaambia kweli hawawezi. Uvumilivu hawana, uvumilivu hawawezi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa akili zao wanaitwa wana hamu fahamu zimeondoka. Hamu imewazidi fahamu hazifanyi kazi niwapeni hadithi. Siku moja nilikuwa timu Meneja wa Timu ya Mpira ya Shangani. Nimekaa kwenye benchi na kocha wangu wa Ujerumani tunacheza na Simba. Goli kipa kapigwa shuti katema nikamwambia kocha mtoe hafai yule. Haya baada ya dakika mbili beki kapigwa ngwala nikamwambia mtoe! Kuja kupiga tahamaki *half time!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeingia chumba cha mapumziko kocha kaja kwangu. Ananiambia Meneja nisamehe lakini watu ulioniambia niwatoe hapa wako saba na tunatakiwa tubadilisha watatu inakuwaje? Hizi ndizo akili ambazo nilikuwa nazo wakati huo sawasawa na za Wapinzani. Unakuwa na hamu, akili haifanyi kazi. (*Kicheko*)

Sasa tuje kwenye bajeti yetu jamani. Ninachosema sasa hivi *Alhamdulillah* Dar-es-Salaam inajengwa kwa kasi sana na inapendeza, majumba mengi mazuri, lakini tuna matatizo ya miundombinu nafikiri Serikali imeshapanga bajeti mambo yake yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja ambalo nataka nitahabaishe hasa Serikali hizi za Mitaa. Katika Richmond *Street*, Mindu pale kuna maghorofa mengi sana yamejengwa, lakini ukipita pale barabara ukiangalia na maghorofa yale havilingani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Halmashauri zetu zijipange, kwamba watu ambao wanajenga maghorofa basi barabara zile ziwe majukumu yao, kwa sababu kabla ya

ujenzi ule barabara zilikuwa nzuri zinapitika, lakini malori ya michanga, kokoto na vyuma, zinaharibu barabara zile. Kwa hivyo, mtu yeyote ambaye anajenga ghorofa sehemu yoyote lazima kuwe na mchango ambao unachangia kujenga barabara pamoja na mitaro ya mitaa ile. Naomba sana hilo lifanyiwe kazi katika Ofisi hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linasikitisha, kulikuwa na operesheni na bahati nzuri Mkuu wa Mkoa wa Dar-es-Salaam yupo hapa, walifanya operesheni ya kuondoa watu ambao kwakweli wanatafuta riziki zao kwa kuuza mikahawa ya jioni. Baada ya saa kumi na mbili mtu anapanga meza katika area yake, anauza kuku anachoma anapata riziki yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliingia watu wakavunja vunja wakachukua meza, vyakula vinaondosha, lakini sasa katika hili tunaona kama tunafanya sera hii kwa ubaguzi. Ukiondoka Kariakoo na Mjini ukienda huku juu unaona watu wanauza pombe kabisa na meza ziko nje hawafanywi lolote. Sasa hii *double standard* sifahamu ya kazi gani. Kwa hivyo, naamini hii sio sera ya CCM ni sera ya watendaji wabovu. Kwa hivyo, nataka tuwasimamie hawa tuweze kuwapa sera za CCM, wazifuate. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wananchi wasibughudhiwe katika shughuli zao za jioni. Hata hao Wamachinga, tunaweza tukawasaidia baada ya saa kumi na mbili tukapanga eneo kama wanataka kuuza bidhaa zao likawepo soko la jioni, hakuna tatizo, lakini wajipange vizuri bila ya kuleta *traffic jam*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu ilifikirie, nalo ni Bima ya Afya kwa wananchi wetu wote. Sasa hivi nimesoma India, Waziri Mkuu Modi ametoa sera ya karibu shilingi sitini kila siku unalipa kabla hujatoka nyumbani, kuanzia mtoto wa miaka kumi na mbili mpaka umri unaofika. Hawa wanachangia rupia moja kwa siku. Ukishachangia rupia moja kwa siku, maana yake wewe unayo *health insurance cover*. Kokote utatibiwa kwa gharama ya rupia laki mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania kama tutabadilika na sisi tukaanzisha Mfuko huo wa kuchangia shilingi ishirini kwa siku, maana yake kwa ufupi tunaweza kwa watu milioni 30, maana tupo 45 tuchukue wengine hawa 15 ni chini ya miaka kumi na mbili. Watu milioni 30 kama utawachangisha shilingi ishirini kila siku au shilingi kumi basi unapata kwa kutwa milioni 300, kwa mwezi utapata bilioni tisa, ambayo kwa kweli itatusaidia kuondoa mgogoro wa afya na Serikali na huo utakuwa Mfuko kila Mtanzania anasaidiwa kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wake hili walichukue, walibebe na walifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni muhimu sana sasa hivi tuna mfumuko wa bei...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. SALIM ABDULLAH TURKY: Kengele ya kwanza hiyo.

MWENYEKITI: Kengele ya pili. Mheshimiwa Mwanjelwa, ajiandae Mheshimiwa Kamata!

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kabisa kwa sababu hii ni bajeti ya mwisho ya Bunge lako Tukufu la Kumi, naomba nichukue fursa hii ya kipekee kabisa kuwashukuru wapiga kura wangu wote wanawake wa Mkoa wa Mbeya kupitia Chama cha Mapinduzi. Naamini kwa uwezo wa Mungu nimeitendea haki hii nafasi yangu ya awamu yangu ya kwanza katika miaka mitano sawasawa, hakika Mungu wa Mbinguni awabariki sana, niko kwenye majukumu ya Kibunge na ninaahidi baada ya hapa narudi tena kuendelea kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwanambeya naomba nichukue fursa hii kuishukuru sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutuletea uwanja mzuri kabisa wa kisasa wa Songwe Mbeya na vilevile kuturahisishia usafiri. Hata hivyo, pamoja na shukrani zangu na pongezi hizi kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, ni jambo la ajabu kidogo kwamba uwanja huu haujakamilika kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapo katika sekta ya ujenzi, kwa nini nasema hivyo? Uwanja huu pamoja na kwamba ni mzuri lakini hauna taa. Ni juzi tu hapa ndege ilishindwa kutua, jambo ambalo ni la hatari kabisa. Kwa hiyo, ni vema tukatumia ule usemi unaosema kinga ni bora kuliko tiba, kwa sababu hii inahatarisha usalama wa abiria na wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nikiwa hapo katika sekta ya ujenzi, kwa sababu haya ni mambo ambayo tumekuwa tukiyaimba mno katika Bunge lako Tukufu kwa miaka yote hii na huu ni mwaka wa tano, ni suala zima la barabara ile tunayoita *bypass* kutoka Uyole mpaka Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo Waziri Mkuu hapa ni shahidi, Bunge lako ni shahidi na kila kitu kipo kwenye *Hansard*, tumekuwa tukilipigia kelele kwa muda mrefu sana na nimekuwa nikilizungumzia kwa muda mrefu. Unatoka Uyole unakwenda Mwanjelwa kwangu hapa, kitu cha dakika tano unatumia masaa manne, kweli hii ni halali na wakati kuna hii barabara ya zamani? Serikali inashindwa nini kutuwekea *bypass* angalau tu kuweka moramu kama siyo lami, kuwe na *alternative*. Sasa hii ya kusema mpaka lami, kama pesa haipo, tuwekeeni *alternative* ili wananchi hawa wa Mbeya wasisumbuke, maana wananchi wanaanza kuilaumu Serikali yangu ya CCM kwa sababu mambo mengine ni madogo madogo tu ambayo yangeweza kufanyika lakini hayafanyiki. Jambo kama hili kwa kweli halibariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali yangu ya CCM ituwekee hiyo *bypass* kwa vitendo, hata kama siyo lami, maana haya magari makubwa yote yapite kule chini itaondoa msongamano wa hii barabara ambayo ni ya kutoka Uyole mpaka hapo Mjini. Vile vile barabara inaharibika, ajali ni nyingi. Kwa hiyo, naomba hili jambo lizingatiwe na kwenye bajeti ya ujenzi kama hili jambo sijaona chochote, naweka shilingi yangu hapa ili niweze kupata angalau *legacy* kwa wananchi wangu wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linguine, nakuja katika sekta ya elimu. Wiki iliyopita nilikuwa mgeni rasmi kwenye shule ya sekondari ya Mbeya pale, katika mahafali, baadaye nikaweza kukutana na Walimu wa shule mbalimbali katika Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba, Walimu wamesahaulika sana na sisi wote hapa huko ndiko tulikotokea. Wote tumefundishwa na Walimu, lakini Walimu hawa unakuta kwamba wanajiendeleza, wanapanda madaraja, hawapandi madaraja,

wanapandishwa mishahara hawapandishwi mishahara. Kwa hiyo walimu hawa wamekuwa *frustrated* kabisa na mpaka inafikia hatua wanaanza kuilaumu Serikali ya CCM. Sasa sisi kazi yetu ni kuwaambia Walimu Serikali ya CCM inawapenda, inawajali, wavute subira kwa sababu Serikali hii ya CCM ndiyo yenye familia na siku zote mwenye familia ndiyo mwenye uchungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wengine wanaposema Serikali imechoka ni kwa sababu inafanya kazi. Kwa hiyo, tusipende kulaumu, suala la msingi ni kwamba hata tunapotoa ushauri basi tutoe ushauri kwa busara, siyo kwa kutukana, kwa sababu unapokuwa na familia wewe ndiye mwenye watoto na wale watoto ndiyo barabara, wale watoto ndiyo mahospitali, wale watoto ndiyo mashule na sisi wote tunategemea hizo huduma, nani atakuja aweke muujiza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hata tunapotoa ushauri, tutoe ushauri kwa busara na huo ushauri utazingatiwa na kufanyiwa kazi endapo utatolewa kwa busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika sekta hii ya elimu ni nini kifanyike juu ya suala zima la Walimu. Nashauri na kupendekeza ni vema kikaundwa chombo maalum ambacho kitakuwa kinashughulikia masuala yote yanayohusu Walimu na hiki chombo ni nini? lundwe Tume ya kwao wenyewe ya masuala ya Walimu tu, kama kuna kupanda madaraja, kuna kushuka madaraja, kuna mishahara, kulalamika na mambo mengine yote waundiwe chombo chao, kuliko kila kitu kupitia katika Wizara ya Elimu, mzigo unakuwa ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kile Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha pale Mbeya. Serikali yetu inasema kwamba Walimu wa masomo ya sayansi ndiyo wanaopewa kipaumbele. Sasa pamoja na hayo kile chuo kinafundisha pia masomo ya sayansi na kuna Diploma pale. Vijana wengi wapo humo mavyuoni hawana uwezo wa kujilipia, basi wale wanafunzi wanaochukua Diploma kwa masomo ya sayansi wakumbukwe kupewa mikopo. Hiyo itapunguza *tension* na wale watoto watakuwa na imani kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho, nataka kusema kwamba Jiji letu la Mbeya limekuwa ni *squatter* na hii mimi nimekuwa nikiisema muda mrefu katika sekta ya ardhi. Kwa hiyo, suala zima la mipango miji liangalie Jiji hili la Mbeya ambalo limekuwa ni *squatter* linatumia mbinu gani katika kuhakikisha kwamba *squatter* hii haipo bila kuwabugudhi wananchi na fidia yenyewe iweze kufanyika kwa utaratibu unaotakiwa.

(Hapa kengele ya kwanza ililia)

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo kengele yangu ya ngapi?

MWENYEKITI: Ya kwanza!

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Ya kwanza, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nikirudi katika sekta ile ya ujenzi katika viwanja vya ndege. Nikiwa kama Mwanambeya kuna ule uwanja wa zamani wa *Airport* ambao sasa hivi hautumiki na nilishawahi kumuuliza hapa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, akawa amenipa jibu ambalo lilikuwa halina mwelekeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema, Wizara husika iliangukie hili jambo la uwanja ule wa zamani wa ndege ambao upo pale pale mjini. Ule uwanja sasa hivi hautumiki, ule uwanja sasa hivi umekuwa upo upo tu na yale majengo yamekuwa ni magofu. Sasa wangetupatia basi sisi Jiji la Mbeya ili tufanye kitega uchumi, kama ni kujenga pale hoteli ya

kitalii au kama pale ni kufanya stendi, lakini kuliko kuuacha vile vile hiyo ni ku-*misuse resources unnecessarily*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba niseme tena kwamba, naunga mkono hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, lakini haya tunayoyazungumza kila siku naomba sana kwa heshima na taadhima, yasiwe kwamba tunaimba wimbo tu, kwa kweli yawe yanatekelezwa, yawe yanatiliwa mkazo, kwa sababu ni kwa faida ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mchangiaji wetu wa sasa ni Mheshimiwa Vicky Kamata na tutamaliza na Mheshimiwa Kaihula!

MHE. VICKY P. KAMATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa namshukuru Mungu kwa afya njema na naanza kwa kuunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu naenda moja kwa moja ukurasa wa 21 ambapo hotuba hii inaelezea hali ya uchumi. Sitasoma tangu mwanzo kwa sababu ya muda, anasema pato la wastani la Mtanzania limeongezeka kutoka shilingi 360,865 mwaka 2005 hadi shilingi 1,725,290 mwaka 2014. Kwa hiyo, inaonesha hapa kwamba, nafikiri kila mtu anaelewa pato la Taifa ukigawanya kwa *population*, then unapata *income per tax*.

Kwa hiyo, kwa kila Mtanzania ameweza kupata 1,725,290 kwa mwaka wa 2014 ambapo ukigawanya kwa miezi 12 unapata kama 1,044,000. Si mbaya, lakini bado siyo nzuri sana, naamini kwamba Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ina uwezo wa kufanya vizuri zaidi katika kuinua uchumi na pato la Serikali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujifunze tu hata kwa wenzetu, si lazima tuende Ulaya, tujifunze kwa nchi zetu hizi za Afrika; Botswana, Swaziland, Namibia. Tujilize wenzetu wamefanya nini kufikia hatua hiyo nzuri kiuchumi, kwa nini sisi tujifunze kwao. Ukiangalia Tanzania tuna kila kitu ukilinganisha na hizi nchi ambazo nimezitaja. Botswana nadhani wanajidai zaidi na *diamond*. Nashangaa na nawapongeza sana Swaziland wameweza kuwauzia hata umeme South Africa kwa nini sisi tushindwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kama tukiwa na mipango mizuri zaidi, hapa tulipo si pabaya, lakini kama tukijipanga vizuri tuna uwezo wa kufanya vizuri sana na kujengea heshima nchi hii ukizingatia Mungu ameibariki ina *resources* za kutosha. Tuna madini ya kila aina, tuna kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani! Tuangalie hata wenzetu nchi za G20 pamoja na utajiri mkubwa walionao kwenye nchi zao, lakini mwaka 2008 waliona wana kila sababu ya kubuni mbinu mpya itakayowawezesha kuongeza pato la Serikali ya nchi zao, ndipo walipoamua kuanzisha mpango madhubuti kabisa wa kushirikisha makampuni yote makubwa na wafanyabishara wakubwa, walitengeneza utaratibu wa kubadilishana taarifa sahihi. Vyombo vyote vya fedha vilikuwa vikibadilishana taarifa sahihi na makampuni makubwa na wafanyabiashara wakubwa pamoja na *revenue authority* za kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kiliweza kuwasaidia sana wenzetu kujua ni nani na nani wanalipa kodi sawasawa na nani hawalipi sawa sawa. Kwa nini na sisi tusifikirie kila siku mbinu mpya? Tunaamini kabisa uchumi unaweza kukua na kwenda vizuri zaidi kama tutakuwa vizuri katika eneo la ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tukikaa vizuri katika eneo hilo nina uhakika kabisa tunaweza tukafanya vizuri, tukatoka kuwa wa 17 katika nchi zenye uchumi mzuri Afrika, sisi ni wa 17 inasikitisha sana kuona tunatanguliwa na vinchi vidogo vidogo ambavyo havina hata rasilimali nyingi kama za kwetu. Kwa hiyo, naamini kabisa chini ya Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi na Viongozi wazuri tunaweza kabisa tukafanya vizuri na tukafika kule ambako tunataka kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia niende ukurasa wa 46 ambapo hotuba hii inazungumzia habari za mambo ya madini na jinsi ambavyo yameweza kuchangia vizuri kuinua uchumi wa nchi yetu. Naipongeza sana Serikali mpaka hapa ilipofikia, lakini nasema bado sana. Sekta ya madini ingeweza kutufikisha mbali zaidi tusingeweza kuishia kwenye hizi dola 1,794 milioni. Naamini kabisa tunaweza kufika mbali zaidi kwa sababu kwanza mimi mwenyewe natokea Mkoa wa Geita ambako dhahabu inatoka, lakini mpaka ninavyozungumza sasa hivi wachimbaji wa Geita hasa wale wadogo wadogo hawajakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Geita *Goldmine* ina *mining license* ambayo ime-cover eneo kubwa sana kiasi kwamba wachimbaji wadogo wa Geita wamekosa maeneo ya kuchimba. Naamini kabisa hawa wachimbaji wadogo wangepatiwa maeneo sahihi ya kuchimba wangeweza kuongeza sana hili pato la Taifa na wangeweza kujikimu kimaisha kwa sababu ni haki yao kutumia rasilimali ambazo Mungu amewajali katika eneo lao. Sasa leo hii Wachimbaji wadogo wa Geita wanaishi maisha magumu utafikiri si haki yao kutumia *resources* ambazo Mungu amewapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kwamba Serikali itafanya kila linalowezekana. Kwa sababu tukiangalia wenzetu wa Ghana, wenzetu wa Ghana wamewezaje kuchanganya samaki mkubwa na mdogo wakaweza kuogelea kwenye bwawa moja. Kwa maana kwamba mchimbaji mkubwa na mdogo wanachimba katika eneo moja, lakini wamewekewa utaratibu mzuri unaowawezesha wao kuchimba wakubwa na hawa wadogo kuchimba bila kudhuriana chochote. Sisi tunashindwa nini hawa Waghana walioweza? Maana kama kosa tayari tumeshalifanya, tumegawa maeneo makubwa kwa Wawekezaji, watu wetu tumewasahau kidogo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tumeshafanya hilo kosa tuwaige wenzetu wa Ghana walivyofanya, wamewaweka wachimbaji wadogo na wakubwa wanachimba pamoja na wawekewa utaratibu tu mzuri ili maisha yaendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo la Semina, kuna eneo la Nyamasagata, kwanza mchimbaji mdogo huyu ukizingatia hana vifaa vya kuchimba mpaka afike mbali aweze kuchukua dhahabu kubwa ya kumpunja huyu mwekezaji wenu. Sasa inashindikana vipi kufikiria kwamba huyu mchimbaji mdogo ambaye anaparaparua anapata vidhahabu vya juu juu kwa nini usimwekee eneo akachimba tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni kama kisimizi kipo juu ya tembo, yaani uchimbaji wa hawa wenzetu wenye *machinery* kubwa, *heavy duty* na hawa wenzetu na sisi akina Vicky hapa tunaachimba hatuna vifaa, kwa hiyo hatutawadhulumu, hatutawapunja, hatutawaumiza hawa wawekezaji. Naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu katika majumuisho yake na naamini kabisa atalizingumzia hili jambo la wachimbaji wadogo wadogo wa Geita kwa sababu limeshakuwa kero ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo wadogo wa Geita ni wastaarabu na ni wavumilivu ndiyo maana mpaka sasa Geita kuna amani pamoja na ugumu wa maisha ambao

unawakuta. Naamini kabisa Serikali inawapenda, inawathamini kwa hiyo itafanya lile linalowezekana kuhakikisha kwamba hawa wachimbaji wadogo wanapatiwa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika kipindi cha lala salama, naamini Bunge hili ndiyo tunamaliza maliza tunarudi tena kwa waliotutuma hapa kama watatupa ridhaa ya kurudi tena tutashukuru, wasipotupa basi tutajumuika nao katika kuwapigia kura wengine maana maisha ni lazima yaendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Jakaya Kikwete na Serikali yake vile vile na wao ndiyo wanamaliza, sasa kama anamaliza Mheshimiwa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete naongea kwa niaba ya Wananchi wa Geita, ahadi ni deni. Katika huu muda wake mfupi uliobaki, wananchi wa Geita wanaomba atimize ahadi yake aliyowahidi wananchi wa Nyarugusu mwaka 2010. Aliwaambia kwamba lile eneo lililokuwa la STAMICO atawapatia wachimbaji wadogo, hivyo wakajiweka katika vikundi vya SACCOS 23 wakiadini ahadi ya Rais ni ahadi ambayo haiwezi kuchelewa na ni ahadi ambayo haiwezi kukwepeka.

Kwa hiyo, wamesubiri kwa muda mrefu na wanajua sasa hivi Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Serikali yake inamaliza muda, lakini wanaamini kwamba Rais Kikwete atamkabidhi kijiti mtu mwingine ambaye ni maridadi na ana uwezo kutoka Chama cha Mapinduzi, bado wamenituma pamoja na kwamba wanaamini atakayekuja anatoka Chama cha Mapinduzi, wanasema ahadi aliyoitoa yeye wanataka atimize yeye mwenyewe asimwachie yule anayekuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni ombi na Mjumbe hauwawi, naomba Rais Jakaya Kikwete atimize ahadi ya wananchi wa Geita ya kuwapatia eneo la STAMICO ambalo liko Nyarugusu ambayo ni ahadi yake ya mwaka 2010 na aliirudia mwezi wa 12 mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ningependa niwashukuru wananchi wote wa Geita, akinamama wote walionichagua kunileta hapa. Naamini kwa nguvu zangu zote na kwa uwezo wangu wote ambao Mungu amenijalia nimejitahidi kufanya pale nilipoweza na narudi kuendelea kushirikiana nao kama...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kaihula!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Waziri wetu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitazungumzia ya kushauri Chama cha Mapinduzi na Serikali yake, bali nitathibitisha kwa nini ni lazima wabadilishwe kwa sababu wameshindwa, wamechoka, wamelegea, wameonesha wazi kabisa kwamba hawawezi. Kwa hiyo, saa hizi siyo wakati tena wa kuwaambia tuwashauri, wameshindikana hawa, wameshindikana kabisa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu sana kwa kuniweka katika Bunge letu Tukufu kwa muda wa hii miaka yote mitano. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu, ya amani aliyoiweka, lakini pia, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu, nilipoanza tulilikabidhi hili Bunge kwa Waombaji. Nawashukuru sana waombaji wote ambao wameendelea kuliombea Bunge letu hili kwamba, libaki katika amani na nchi yetu ibaki katika amani. Naamini watafanya hivyo mpaka hata Serikali ya CHADEMA katika UKAWA itakapokuwa imechukua mamlaka na madaraka ya kuongoza nchi na kuonesha mfano wa jinsi gani ambavyo inapaswa kuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nizungumzie kwamba, Chama cha Mapinduzi kimeifanya Serikali yake, ambayo ni kama mtoto wake, isiweze kufanya kazi kwa sababu, hakijawa kikiisimamia vizuri Serikali yake! Badala ya kuisimamia Serikali, kinaibeba! Kwa hiyo, napenda niwapongeze sana UKAWA na Kiongozi wa Upinzani kwa kazi nzuri aliyofanya ambayo imefanya nchi hii angalau ibakie kidogo hivi ilivyo, maana bila kazi tuliyofanya kubwa ya kuwashauri, kuwakosoa kama ambavyo tulivyotumwa kama Upinzani, nchi hii ingekuwa imekwishauzwa zamani, kwa maana mpaka sasa iko rehani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Mapinduzi wameshindwa kazi ni wachovu. Kwa nini? Kama alivyosema mmoja ambaye alitumia Ilani yao wenyewe ya kwamba, wao watafanya hivi, *BRN*, hakuna! Elimu, hakuna! Kilimo, hakuna! Afya, hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu inasikitisha sana kwamba, Chama cha Mapinduzi kimeipotisha Serikali yake mpaka ikaifanya nchi ikadidimia. Kwa sababu, wamefanya kwamba, uwongo ni lbada! Saa hizi watasema hivi! Saa hizi watafanya hivi! Niambie toka tumeanza na hata tunakoendelea mafungu yote ambayo yalikuwa yameahidiwa kwamba, yatapelekwa, kwenye sekta zote, hakuna lililotimilika hata kwa nusu! Chama cha Mapinduzi uwongo umekuwa lbada na mnajua kabisa kwamba, haifai! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe fikiria...

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kumpa Taarifa Mheshimiwa Mbunge anayeongea; anapothibitisha Bunge hili kwamba, Chama cha Mapinduzi katika mambo yote na Serikali yake kimekuwa kikisema uwongo na hakifanyi ukweli! Naomba kumpa Taarifa kwamba, si sahihi hayo anayoyasema! Aseme ule upungufu, lakini mambo mengi yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi punde tu, leo asubuhi Mheshimiwa Mchuchuli, Mbunge wa *CUF*, ameipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi wakati akiuliza swali la nyongeza ndani ya Bunge kwa kufanya vizuri kurekebisha matatizo ya umeme Wilaya ya Kilwa. Jana pia wakati Mheshimiwa Bwege, Mbunge wa *CUF* akichangia humu Bungeni alisema pia Serikali imefanikiwa kumaliza barabara ya lami kutoka Dar-es-Salaam mpaka kilwa na kujenga daraja la Mto Rufiji!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kumpa Taarifa Msemaji kwamba, hayo anayoyasema aende kwenye upungufu, lakini si kweli kwamba, Chama cha Mapinduzi hakijafanya kitu kwenye elimu. Chuo Kikuu cha Dodoma kiko pale na watoto wake wanasoma pale Dodoma. Kwa hiyo, si sahihi aseme upungufu na katika chuo hicho hicho tulichokijenga kizuri, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akienda pale na kufanya siasa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampa taarifa tu kwamba, tunaendelea, tumefanya mazuri. Yako mapungufu, tutayatekeleza na tunakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba apokee hiyo Taafika.

MWENYEKITI: Pokea Taarifa, Mheshimiwa Kaihula!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namsikitikia sana mwanangu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kaihula, kubali yaishe!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei na nataka kuthibitisha kwamba, kwa nini sipokei na nazidi kueleza kwamba, wamedidimiza nchi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kwanza nasikitika kwa sababu, wao wanaamini sana katika udhaifu! Yaani ubora hawana. Kuna sababu gani ya kuwa na vitu vingi ambavyo ni dhaifu vinaleta badala yake madhara. Vyuvo vikuu vingi, havina wanafunzi wazuri, Walimu ni hivyo, halafu hata mnashindwa kuwapa pesa za kuendeleza! Watoto wetu wa kike wanashindwa hata kuendelea mwisho wanapata ni mimba! Ninyi, nasikitika. Hilo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya! Mnasema uwongo! Nathibitisha; mnasema kwamba, kuna madawa mahospitalini, hakuna madawa hospitalini! *In fact* nyie mmemaliza madawa kwa kuchukua pesa hizo kifisadi! Halafu kwa nini nisiwaambie mambo ya ukweli?

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu! Niwambie nini katika...

MHE. ASUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa!

TAARIFA

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kumuuliza au nataka kumpa Taarifa kwamba, CCM haiwapi watu mimba! Kwa hiyo, CCM haifanyi kazi hiyo. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Pokea Taarifa ya Mimba!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sio mlezi mzuri! CCM sio mlezi mzuri na nilianza hivyo hivyo na kwa sababu, wanakwenda kujenga mashule mengi halafu hawaweki *hostel*, hawaweki usimamizi! Ni sawasawa na mlezi ambaye baba na mama watoto wao wanapata mimba hovyoy. Kwa kweli, hata katika Sheria inapaswa iwekwe hiyo wapate adhabu wazazi badala ya watoto, CCM ndivyo mlivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuendeleza kwamba, CCM kwa kweli, mna matatizo makubwa, mmechoka! Mmelegeta! Kwa kweli, ninyi wananchi hatuhitaji hata kuwaambia kwamba, muwatoe, wananchi wenyewe huko wanatangaza dira ya kusema hawa jamaa lazima watoke, lazima tubadilishe waweke watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili wala msogope, mkubali. Jitayarisheni kisaikolojia kwa sababu, kusema ukweli mwanangu Jenista wewe unanifahamu mwanangu! Ni hivi, katika nchi zozote zinazotaka kuendelea ni lazima kuwe na kubadilishana kwa sababu, mtakapokaa kule, ndiyo mtajifunza kwamba, alaah! Kumbe pale mahali, walikuwa wanatwambia kweli! Lakini mkikaa tu hivi hivi mnabweteka kwa hiyo, lazima ninyi mkapumzike, tuwaweke *bench* na halafu wananchi waone kazi ya CHADEMA watakavyofanya! Maana yake...

TAARIFA

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu niseme hii kauli ya CCM imechoka ni vizuri watu wakawa wana, wanaozungumza wengine wakatazama jinsi walivyo! CCM imechoka au na yeye dada pale kachoka? (Kicheko)

MWENYEKITI: Haya, pokea Taarifa ya kuchoka! (Kicheko)

Mheshimiwa Machali! Mheshimiwa Machali?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(1), ikisomwa sambamba na Kanuni ya 64(1)(a) kwamba, Mbunge hatatoa Taarifa ambazo hazina ukweli Bungeni. *Concept* nzima ambayo tumeizungumzia kama Wapinzani kwamba, Serikali ya CCM imechoka ni kwa sababu ya kushindwa kuendana na mpango au programu ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watuambie kwa miaka 10 iliyopita ni mwaka gani ambao Serikali iliweza kutekeleza bajeti yake kwa 90% tu! Wasimame hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapowaambia kwamba, wamechoka ni kwa sababu, ni katika mantiki hiyo. Kwa sababu, wamefeli kutekeleza...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali umeshaeleweka. Umeshaeleweka, kaa chini.

Mheshimiwa Kaihula, endelea!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wasinichanganye. Mimi nawaeleza na nimezoea, hata waseme vipi! Mimi ni Mwalimu, tena sio Mwalimu wa kupapasa, ni Mwalimu hasa, kuanzia *Kindergarten* mpaka Vyuo Vikuu, najua hiyo na nimefundisha mpaka watoto watukutu na wengine wako humu! Kwa hiyo, kusema nimechoka, mimi sijachoka! CCM imechoka na imelegea ndiyo maana haitekelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea! Umelinda muda wangu, *partner*? Muda wangu ulindwe!

MWENYEKITI: Taarifa tunapata! Muda wako nimelinda.

Mheshimiwa Kaihula jamani, tulishindana Jimbo moja Ilala 2010 na anaingia tena! Ndiyo maana nimempa nafasi, ili ajiandae nije kumgaragaza tena 2010. (Makofi)

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Partner* ahsante. Nakwambia *Partner* ujiweke tayari kisaikolojia, *ki-physically* na kila kitu kwa sababu, safari hii nakuja sawasawa. Nikwambie kabisa, kwa hiyo, mambo ya Mchikichini yale manyumba, yale *ma-fly overs* ambayo hujaitengeneza! Ambavyo vitu vilikuwa kwenye Sera yangu, ulipoona kwamba, nitakushinda ukavichukua halafu hukuvifanya vizuri! Vyote vile ndiyo vimekuangusha kabisaa! Vi-Machinga *Complex* zile! Sijui nini! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Partner*, sasa mbaya sana na mvua safari hii imekuumbua! Miundombinu hakuna Dar-es-Salaam kabisa! Wewe Machinga kila wakati! Nakwambia *Partner* bye-bye! Kwa heri...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sendeka!

TAARIFA

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kutoa Taarifa kwa Msemaji. Nimevumilia kupita kiasi, nimemsikiliza Waziri Mkuu, nimemsikiliza Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni, nimesoma Taarifa yake; wanasema Serikali ya CCM imechoka!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba hii ya Waziri Mkuu kuna mambo ya Afya, Elimu, miundombinu ya barabara. Nionesheni katika Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, chochote! Ina mambo mawili, ukurasa wa kwanza mpaka wa 34, ina mambo ya uchaguzi tu! Kurasa nyingine zilizobaki zinazungumzia porojo nyingine.!

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani nikuhakikishie hakuna shule, hakuna elimu, hakuna zahanati. Nionesheni mahali ambapo imeandikwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakionesha...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kaihula endelea! Mheshimiwa Machali na nani! Kaeni.

Mheshimiwa Kaihula, endelea!

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kweli, Mheshimiwa Sendeka namheshimu, lakini sikudhani kwamba, yuko *below that much!* Kwa sababu, sisi hatukusanyi kodi! Kodi mnayo ninyi, halafu hayo mabarabara unayoyasema, mabarabara yenyewe mmeyaharibu! Mnaacha kujenga reli, mabarabara mnapenda milori yenu ya mizigo itembe humo, hamjengi reli! Ufisadi mtupu! Nakuheshimu sana, hakuna mlchoweza ninyi! Ninachosema ni cha kweli. Wewe niambie, mafuriko ya kule Dar-es-Salaam yalikuwa yanapaswa kuwa mpaka saa hizi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamjui vipaumbele, hamna nini, ninyi kila wakati sifa za uwongo! Ibada kwenu, uwongo ni ibada kwa nini? Msitupigishe laana! Naendelea! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa halafu sisi tuna laana ya kuwadanganya wazee kila wakati! Wazee wametupa laana; ooh, mtatibiwa bure hospitali, hamuweki Sheria! Kwa hiyo, mpaka leo wazee hawapati hata hiyo! Mnakwenda kuweka nyumba za wazee, hamzitendei haki! Mmewatupa huko, mna laana! Hamko *friendly* si kwa vijana! Vijana wenyewe vijana wenu mmewasomesha wengine mmewaweka huko! Kwa nini mnashindwa kwenda kuwakusanya kwenye makundi mkawawekea dhamana kwenye mabenki wakaweza kufanya kazi zinazoeleweka, Wasomi Wataalam? Mko *very selfish*; yaani mnajipenda mno kazi yenu kujaza pesa kwenye utawala sio kwenye maendeleo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana tunasema mmechoka! Mmechoka! Mmelegea! Hamuwezi! Nawaambia na wananchi ndivyo wanavyowa-rate, wala hatuwadanganyi ndugu yangu *Partner!* Sasa utafanyaje, mimi nakuja! Eeh! *I'm coming!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana mambo yenyewe haya, mimi nakupenda *Partner* wangu kwa sababu, wewe tunaelewana, mmh! Tunakwenda kupimana huko! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea. Sasa fikiria *Partner*, hizi barabara mnazojisifu barabara, barabara! Migongo hiyo tunayopita hiyo! Mmeharibu na migari yenu ya ufisadi! Mnatuambia nini, CCM mmechoka! Mmechoka, mmechoka, mmechoka! Mnapaswa muondoke mtupe nafasi sisi CHADEMA katika UKAWA tuweze kufanya mambo ya maana. Wala saa hizi sio wakati wa kuwashauri ninyi, hamshauriki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyie sasa hivi jitayarisheni kutukabidhi, sisi tuendeshe nchi muone tutakavyong'oa nanga, hamna vipaumbele, hamna nini, nyie watu gani ni *hand to mouth* kila kitu! Hata nchi ya watoto wenu mmeuza yote! Hamna mipango! Mikataba yenu ufisadi tupu! Nashindwa kuelewa! Ewe Mwenyezi Mungu, tusaidie kabisa tutokane na hawa watu kwa sababu, ni watu ambao wanaombewa, lakini hawaombelek! Mungu wetu, kwa kweli... (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Ahsante sana, *Partner*.

MHE. NAOMI A. M. KAIHULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *you are welcome Partner*. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kirigini!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwenye Bunge lako Tukufu kupitia Kanuni Namba 68(7) ambayo inasema: "Mbunge yeyote anaweza kusimama na kuomba Mwongozo wa jambo ambalo limejitokeza wakati wa majadiliano."

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waheshimiwa Wabunge wakiendelea kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, limejitokeza jambo ambalo ni la kusononesha na la kusikitisha. Naomba ku-*declare interest*, mimi ni Mkuu wa Wilaya, lakini vilevile ni Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati majadiliano yakiendelea hapa Bungeni, wakati Mheshimiwa Mbunge wa Karagwe ametoa lugha ya vitisho na uchochezi mkubwa dhidi ya Mheshimiwa DC wa Karagwe. Naomba Mwongozo wako, kwa kuwa, Mheshimiwa DC wa Karagwe tunatambua kwamba, ndio msimamizi Mkuu wa amani na hata yeye yuko hapa ndani na anamtegemea Mheshimiwa DC yule, sasa nilikuwa naomba Mwongozo wako kwa kutambua nafasi hii ya u-DC kwamba, DC ndio mwakilishi wa ulinzi na usalama na mwakilishi wa Rais kule Wilayani. Naomba Mwongozo wako, uchochezi huu uliotolewa hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikiliza Mheshimiwa Blandes wakati akichangia. Tumesikiliza Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Rosemary Kirigini. Jambo hili, sisi kwa kuwa, tuko humu ndani na Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo inayoratibu shughuli zote za Serikali ndani na nje ya Bunge, jambo hilo sisi Serikali tumeshalichukua na naomba tuachiwe kuendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutalifanyia kazi kwa taratibu zile ambazo zitakwenda kupima pande zote mbili kwa mwongozo wa Mheshimiwa Rose Kirigini! Zitakwenda pia, kuangalia yale yaliyosemwa na Mheshimiwa Blandes na Serikali itaendelea na taratibu zake za kuchukua hatua na kusimamia utendaji kazi wa watumishi mbalimbali wa Serikali kwa mujibu wa miongozo na taratibu tulizonazo. *(Makofi)*

MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA: Mwongozo wa Mwenyekiti!

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Sendeka tafadhali kaa!

Wachangiaji wetu wote waliopangwa mchana wamekwisha. Licha ya kuwa tunao muda, lakini kuna wachangiaji watatu ambao walikuwa na kazi maalum leo ambao ni Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Profesa Kahigi na Mheshimiwa Jafo; hawa wataanza jioni kwa namna nilivyowataja. Ataanza Mheshimiwa Christowaja, atafuatia Profesa Kahigi na atamalizia Mheshimiwa Jafo na baada ya hapo Serikali mjiandae kutoa majibu kwa namna mtakavyojipanga, kuanzia Saa 10.30.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

(Saa 7.37 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea.

Kama nilivyozungumza kabla sijaahirisha, tutaanza na Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Profesa Kahigi na Mheshimiwa Jaffo, tunaanza na Mheshimiwa Christowaja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza jioni hii leo nami niweze kuchangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai mpaka siku hii ya leo ambayo nadhani ni bajeti ya mwisho kwa Bunge hili la Kumi na nitoe shukrani zangu kwa familia yangu kwa kuniombea mpaka muda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye bajeti na nianze na suala la elimu, kwenye elimu nitazungumzia kero kubwa sana ambayo inawakera Walimu wetu, hususan madeni ya Walimu. Hili nitaomba nipate ufafanuzi kutoka Ofisi ya TAMISEMI, inayoshughulikia mambo ya elimu tena *specifically* lipate taarifa na ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Kassim Majaliwa kaka yangu kuhusu madeni ya Walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, ambayo nilikuletea kwa maandishi tangu mwaka jana. Madeni hayo ni ya Walimu 63 ambayo yana thamani ya jumla ya sh. 81,497,502/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni hayo yanajumuisha uhamisho, matibabu, kujikimu, mishahara nauli au usumbufu. Mheshimiwa Naibu Waziri naomba maelezo ya kina kwa sababu mpaka sasa hivi Walimu hawa bado hawajapata haki yao. Hapo kwenye madeni ya Walimu kabla sijatoka, naomba mtueleze kinagaubaga ni kwa nini hawa Walimu wapya mliowaajiri juzi bado hamjawapa hata posho za kujikimu? Wanaendelea kutangatanga kana kwamba ni wakimbizi, ni kwa nini mnawatesa Walimu kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme wazi hizo ajira mlizozitangaza nyingi ni za kisiasa mlisema ni Walimu wa sayansi lakini Walimu wengi ni Walimu wa masomo ya *art*, Walimu waliotoka Mtwara TCC hawajasoma sayansi, lakini mmewaandika ni Walimu wa sayansi. Mfano

mwingine unaonigusa ni binti yangu mimi mwenyewe wa kwanza, binti yangu hajasoma masomo ya sayansi Chuo Kikuu, binti yangu amesoma masoma mengine kabisa ya Art, mmempanga kama Mwalimu wa sayansi tena Kigoma. Kwa nini mnafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai tunahitaji Walimu wa sayansi, lakini msifanye siasa kuonesha kwamba mna Walimu wengi wa sayansi kumbe siyo, tunahitaji uchambuzi wa kina, ni Walimu wangapi wa sayansi mmewapa ajira na Walimu wangapi ambao siyo wa sayansi, lakini siyo kutoa idadi yote kwamba ni Walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo na suala la madeni ya wazabuni wanaopeleka vyakula kwenye shule zetu za Serikali. Juzi hapa shule za Serikali zilifungwa, shule kadhaa zilifungwa kwa ukosefu wa chakula. Fedha tulizosikia za wazabuni tulisikia kwamba zile pesa tayari zilishapelekwa TAMISEMI toka Hazina, lakini TAMISEMI ukiwauliza wanawarushia mzigo Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu nao ukiwauliza, danadana wanasema TAMISEMI. Sasa Mheshimiwa Waziri tunaomba mtuambie hizi pesa za wazabuni zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza Waziri wa Elimu anavyotangaza anasema Walimu Wakuu wa shule waliofunga shule wachukuliwe hatua za kinidhamu. Hivi unamchukulia Mwalimu hatua ya kinidhamu kwa kufunga shule, hao wanafunzi wangekula mawe au mchanga? Huyu Mwalimu Mkuu angewalisha kitu gani wakati Serikali imeshindwa kupeleka madeni kwa wazabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Walimu waendeleo kutendewa haki, Walimu ni watumishi wa muhimu sana katika Serikali hii ya Tanzania, bila Walimu sisi tusingekuwa hapa. Kada zote zinamtegemea Mwalimu, Mwalimu asiwe anatomika kisiasa kwenye chaguzi bali Mwalimu alipwe stahiki zake sawasawa, pamoja na kutendewa haki. Naunga mkono kabisa hoja ya Mwenyekiti wangu wa Kamati ya kuanzishwa chombo kimoja cha Walimu na Muswada huo mtuambie utaletwa lini ili chombo hiki kiweze kutimiza kazi yake kwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Hawa Ghasia ameelezea kuhusu maadili na nidhamu kwa watendaji au watumishi wa umma. Nieleze jambo moja na amesema watumishi wote wa umma wanaokiuka taratibu au wanaokiuka masuala ya kinidhamu wajiepushe ili wasichukuliwe hatua za kisheria au za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano, Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata wamekuwa ni maharamia wakubwa kwenye maeneo tunayotoka. Watendaji hawa wamekiuka maadili yao ya kazi kwanza wanachangisha wananchi michango ambayo kila siku mnaipigia chapuo hapa, michango ya maabara, michango ya madawati, michango ya zahanati, michango ya madarasa, lakini cha kushangaza hawasomi mapato wala matumizi. Wananchi wakiuliza hawapewi majibu, matokeo yake wanakamatwa na hao Watendaji wa Kijiji wanafungwa kwenye ofisi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji wa namna hii unatoka wapi? Watendaji wa vijiji wa namna hiyo au watendaji wa Kata hatuwahitaji kwenye maeneo yetu, sasa hivi wananchi wamejanjaruka na niwashukuru Wapinzani wote kwa kutoa elimu ya uraia na kuwafanya wananchi wajitambue kuuliza pesa zao zinatumiwa kufanya nini. Nawaambia wazi sisi tunawakataza wananchi kuchangia michango ambayo inaliwa na watendaji, hatutawaruhusu kuchangia kama hawatasomewa mapato na matumizi, sasa msituambie wachangie maabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, naomba nitoe mfano *live*, kuna Mtendaji wa Kata, ninakotoka mimi Jimbo la Singida Magharibi, Mtendaji wa Kata ya Iglansoni, ni mwanamama simtaji jina, mwanamama huyo amekuwa ni mvunjifu mkubwa wa amani. Jana aliongea Mheshimiwa Selasini hapa kwamba viongozi wetu waliochaguliwa kwenye Serikali za Mitaa sasa hivi wanafungwa, wanafunguliwa kesi za bandia, hii imenikuta hata kwenye Jimbo ninalotoka, Kata hii ya Iglansoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa Kijiji waliochaguliwa ni Wenyeviti wa Chama chetu cha CHADEMA. Matokeo yake huyu mama Mtendaji wa Kata amewafungulia kesi ya kubambika sasa hivi hakuna kinachofanyika, DC aliyehamishwa anajua Mkurugenzi kila siku nilikuwa nikimweleza anafahamu, mpaka Mkuu wa Mkoa anafahamu, huyu mama ndiye DC, huyu mama ndiye Mkurugenzi, huyu mama ndiye Polisi, ndiye mgambo anawatesa wananchi kama vile ni wakimbizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtuondolee huyu Mtendaji mkitaka shughuli za maendeleo zifanyike katika Kata hiyo tuondoleeni huyu mama. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sana kwa mustakabali wa amani ya Jimbo la Singida Magharibi huyu mama tunaomba mtuondolee, alishakuwa na kesi nyingi mbaya, kila mtu anafahamu ajabu analindwa, sijui nani anamlinda, tunaomba huyo anayemlinda na yeye mmwangelie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi tatizo analifahamu, pia Mkurugenzi wetu ni mzigo, tunaomba mtusaidie Mkurugenzi wa Wilaya ya Ikungi, ni mzigo kwa sababu Mheshimiwa Hawa Ghasia huwa anatuambia masuala ya Watendaji wa Vijiji au wa Kata ni madogo sana, twende kwenye Halmashauri, tumeshakwenda lakini hakuna kinachoendelea, tusaidieni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunakaa kwenye maeneo ambayo wenzetu Wasukuma, walinyang'anywa maeneo yao huko Shinyanga na Tabora wamekuja huku kwetu. Hawa Wasukuma watozwa kiingilio cha kuja kwenye maeneo na watendaji, hivi hii ni nchi gani? Kiingilio cha Mtanzania kuja kwenye eneo lingine, anatafuta mahali pa kukaa wanatoza kiingilio kutoka sh. 200,000 mpaka 500,000 kutokana na mifugo aliyonayo. Huu unyanyasaji wa aina gani huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata zote za Jimbo la Singida Magharibi, ziko Kata 15, ambazo zinapona ni Kata ya Puma na Kata Ihanja basi, zingine zote wananyanyaswa hao Wasukuma. Hivi Wasukuma siyo watu? Wasukuma ni wakimbizi kutoka Burundi? Naomba watu hawa watendewe haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hawa Watendaji wa Vijiji wamekuwa wakijimilikisha, kuna msitu mmoja unaitwa misitu ya Minyughe, hifadhi wa Minyughe, wamekuwa wakiuza maeneo kwa wananchi, wanawauzia maeneo wanawajimilikisha wao, halafu wanasema huu msitu ni hifadhi ya kijiji, wakati siyo, kama ni hifadhi ya kijiji kwa nini wanauza hayo maeneo, tunaomba mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni bajeti ambazo hazipelekwi. Bajeti za barabara za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Hawa Ghasia ameelezea vizuri sana, lakini naomba niseme, natoka katika Jimbo la Singida Magharibi nimesema katika Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya barabara za Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, hazijapelekwa, zimepelekwa asilimia 23 tu. Barabara zile ni mahandaki, barabara zile ni mbovu, hazipitiki, akinamama wanapokwenda kujifungua wanajifungua njiani kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza, wakijifungua njiani wakifika hospitalini wanatozwa faini ya sh. 15,000/= mpaka sh. 30,000/=, kwa nini umejifungulia njiani? Hivi huyu mwanamama angefanyaje, barabara haipitiki anatembea kwa gari ya kukokotwa na ng'ombe bado Serikali hii ya CCM imeweza kumdhulumu hata huyu mama mjamzito tunaombeni mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na kura ya maoni, kura ya maoni hii ambayo imezungumzwa vizuri sana na hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani...

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Kahigi jiandae Mheshimiwa Jaffo!

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ili nami nichangie hotuba ya Waziri Mkuu na Waziri wa TAMISEMI. Ninayo machache, lakini labda nitaanza na mawili, nitaanza na kuwashukuru wananchi wa Bukombe, kwa mshikamano na ushirikiano ambao wameuonesha, tumeweza kufanya mambo mengi katika hii miaka minne na nusu kuliko katika miaka yote ambayo Bukombe imekuwa ni Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia maji, maji bado ni changamoto kubwa sana katika Jimbo la Bukombe, vijiji vingi bado vina tatizo la maji. Ule mradi wa Benki ya Dunia haukufaulu sana kwa matatizo ambayo Wabunge wameyazungumzia katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa katika ziara yake Bukombe pale Ushirombo, tulimkaribisha vizuri sana, tukaongea naye kuhusu ufugaji wa nyuki na kadhalika, lakini pia akawa ameahidi shilingi bilioni moja kwa ajili ya kutandaza mabomba kwenye mji wa Ushirombo. Kwa bahati mbaya hiyo bilioni moja haijapatikana mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Maghembe alipokuja akiandamana na Rais katika ziara yake huko Bukombe, alituhidi kwamba kuna mpango wa Serikali wa kuleta maji ya Ziwa Victoria kutoka Kahama, kwa sababu tayari yameshafika Kahama, yakipitia Mbogwe kuja Bukombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda nimwombe Profesa Maghembe watujibu watu wa Bukombe kama mwaka huu unaokuja huu mradi utanza. La pili, naomba pia Waziri Mkuu atujibu kuhusu hiyo bilioni moja ambayo alituhidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bukombe wa Maji ulifunguliwa na Waziri Hawa Ghasia, Bukombe pale kijijini, Bukombe center. Kwa bahati mbaya huu mradi mpaka leo pamoja na kwamba ulizinduliwa tayari na wale waliokuwa wanauzindua wakasema kwamba umeshakamilika asilimia mia moja, mpaka leo hautumiki, kila wakifungua hayo maji mabomba yanapasuka.

Naomba wahusika wachunguze kuna tatizo gani pale katika huo mradi isije kuwa kwamba huo mradi ulichakachuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kuongelea ni mawasiliano. Kweli katika hii miaka minne na nusu tumeweza kuishawishi Serikali tukapata minara ya mawasiliano katika maeneo kadhaa, lakini maeneo mengi bado hayana mawasiliano. Mathalani huko Butinzya huko Ng'anzo, Iyogelo, Bugelenga, Namonge na hata maeneo kadhaa ya Busozo

mawasiliano bado ni tatizo. Tunaomba wahusika watueleze yale maombi tuliyoyapeleka kwenye Wizara husika yamefikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuongelea ni hali ya utawala bora Bukombe. Wenzangu wameshazungumza, kuhusu hawa Wakuu wa Wilaya au Watendaji wa Kata ambao wanawaandama wana CHADEMA na hasa viongozi wao baada ya uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa. Pale Bukombe kinara wa ukiukwaji wa utawala bora ni Mkuu wa Wilaya, namuuliza Waziri Mkuu haya maagizo ambayo yametoka katika ofisi yako kwamba Wakuu wa Wilaya wawatese Wapinzani? *(Makofi)*

Kwa sababu yeye kwa fikira yake huwa anasema waziwazi yeye hafichi mtu, yeye yuko pale kutetea Chama cha Mapinduzi na Wapinzani wataipata na kweli kuna Mwenyekiti wa Kijiji cha Kazilamlaye anadamwa andamwa na viongozi wengine na anawatumia hao Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi mimi huwa si mgomvi, watu wanarifahamu, lakini naomba Ofisi ya Waziri Mkuu itusaidie. Papo hapo namshauri kwa nia safi kabisa huyu Mkuu wa Wilaya azingatie Katiba na misingi ya utawala bora ambayo aliapa kuilinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho ambalo napenda kuliongelea ni kuhusu umeme. Ni kweli tumefanikiwa katika hii miaka mitano kuishawishi Serikali ituletee umeme na umeme umekuja katika maeneo hasa ya barabarani ya Bukombe na mijini lakini maeneo mengi kwenye Kata nyingi bado hayana umeme na hasa Kata ya Busonzo, Runzewe Mashariki na Magharibi, Iyogelo, Bugelenga, Butinzya, Ng'anzo na Namonge. Naomba katika majibu Mawaziri husika wanieleze ni lini umeme wa REA utapelekwa katika maeneo hayo kwa sababu nimefuatilia sana katika maswali Bungeni humu na katika maongezi na Mawaziri hatujapata kauli thabiti ni lini umeme utapelekwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningependa kumaliza kwa kusema kwamba mijadala imekuwa ni mingi kuhusu CCM ya sasa hivi. CCM ya sasa hivi kwa kweli siyo kama ya zamani, sisi ni waanzilishi wa hiyo CCM ya zamani na akina Mheshimiwa Pinda hapa na wengine. CCM ya zamani ilikuwa ni Chama cha wakulima na wafanyakazi, sasa hivi siyo tena chama cha wakulima na wafanyakazi. Ndiyo maana hata ukiangalia mwelekeo wa kibajeti hausisitizi miradi hiyo ya wakulima na wafanyakazi, una matanuzi mengi, kuna haya masuala ya ufisadi na mambo kama hayo na ukiukwaji wa utawala bora. Kwa mfano, matukio haya ya ukiukwaji wa misingi ya utawala bora yasingetokea nyakati hizo katika CCM ya zamani. Mkuu wa Wilaya alikuwa ni mlinzi wa watu wake, alikuwa siyo mtesaji wa watu wake. Kwa hiyo, naomba mtafakari hili. Kama mnataka kuendelea kweli kutawala nchi hii, lazima mtafakari huu mwelekeo wa CCM ya sasa la sivyote mtang'olewa na UKAWA. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jafo.

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, kwa wazi kabisa napenda kufurahi kwa kupata fursa hii na mimi jioni hii ili niweze kuchangia lakini kubwa zaidi nimshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Profesa Kahigi, miongoni mwa watu ambao katika mjadala huu nadhani wamechangia kutuongoza kwa busara zake nadhani ametuongoza vizuri zaidi. Profesa Kahigi tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima ndugu zangu tukubali, kila jambo kuna mahali tunapoanzia na sehemu tunapoishia. Nilikuwa nafuatilia mjadala huu kila mtu akiwa na agenda yake akiwa na jinsi yake ya kueleza lakini tukijua wazi na wananchi wakijua wazi kwamba sasa hiki ndiyo kipindi cha mwisho baada ya miaka mitano kila mtu anatafuta kura zake zitakuwa vipi kwa wananchi wake, nadhani ndiyo kikubwa kilichotawala zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nilikuwa nafadhaika sana, kama watu tunasimama hapa Bungeni tunasema kwamba miaka hii mitano Serikali chakavu na kadhalika, ina maana kwamba sisi tumeshindwa kuishauri Serikali kama Wabunge. Mimi naamini ndani ya miaka hii mitano tumefanya kazi kubwa sana ambapo kila Mtanzania analiona hili wala halina kificho. Kazi hii imefanywa na Wabunge sisi wote kwa ujumla wetu. Leo hii tukiona watu waliokuwa hawana madaraja Malagarasi kule leo kuna daraja la Umoja na Mtambaswala limejengwa, Bunge hili lilifanya kazi ya kuisimamia Serikali. Kubwa zaidi namshukuru sana Mheshimiwa Kahigi kwa sababu anasema umeme umetawanyika sehemu zote. Maana Wabunge waliweza kufanya kazi ya kuisimamia Serikali na Serikali ikatimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nina imani na wala sina mashaka katika hili kwamba Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa asilimia kubwa imetekelezeka ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata wale wanaokaa Dar es Salaam pale Kigamboni wanakuta daraja kubwa limejengwa liko ndani ya Ilani, yote hii mipango mizuri. Naamini mambo haya na wananchi wataendelea kukipa sifa Chama cha Mapinduzi kwa sababu kina viongozi imara na makini lakini lengo kubwa ni kwa ajili ya kuipeleka nchi yetu mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu kubwa ni kwa ajili ya kuishauri Serikali. Naomba Ofisi ya Waziri Mkuu inisikilize katika masuala yafuatayo. Moja, Ofisi hii inashughulika na Watendaji wote wa Halmashauri wa Serikali za Mitaa. Naiomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu inapokuja kuhitimisha hapa itueleze ni madai mangapi watumishi wa Serikali wa Halmashauri wanadai, hasa Walimu, Wahudumu wa Afya na Mabwana Shamba. Naamini sasa huu ndiyo muda muafaka na hii ndiyo kazi ya Wabunge lazima tuibane Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu utakapokuja kuhitimisha hapa utueleze ni mkakati gani uliokuwepo katika bajeti hii ili kushughulikia suala la madeni ya Walimu, Mabwana Shamba, Maafisa Kilimo na watumishi wengine wa Halmashauri ili waweze kulipwa. Hatuwezi kukaa ndani ya miaka mitano tunajidai tu, najua kazi kubwa imefanyika lakini hiyo sehemu iliyobaki tunaenda kuitatua vipi ndani ya kipindi hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme na kwenye Bunge la mwezi wa pili nilisema hapa, katika suala zima la madai ya wafanyakazi na hasa katika Mifuko yao ya Hifadhi ya Jamii lakini suala zima la bima ya afya, nilisema watumishi wa Halmashauri wanalalamika na wanalalamika kwa sababu hapo zamani ilikuwa mtu akiwa na ndugu zake au watoto wa ndugu zake wameachwa yatima watu wale walikuwa wanahudumiwa na Mfuko wa Bima ya Afya. Katika suala zima la uboreshaji uliotokea wa sasa hivi wale watu ambao siyo watoto wa damu wametolewa katika utaratibu huu. Ofisi ya Waziri Mkuu siku ile ilisema itaenda kulishughulikia suala hili. Sasa mimi niliyetoa hoja ile siku ile hapa naomba nipate majibu wakati Waziri Mkuu anahitimisha, jinsi gani tumeweza kusaidia wafanyakazi hawa wa Halmashauri ambao kipato chao ni cha kawaida lakini wanalea watoto wengine ambao wako katika mazingira magumu na wao wahakikishe kwamba zile fedha wanazolipia kila mwezi katika Mfuko wa Bima ya Afya wanapata fursa ya kuweza kupata matibabu. La sivyo ina maana

tunaweza tukawa na Mwalimu lakini hana uwezo wa kumsaidia mtoto wa ndugu yake ambaye anaishi naye ndani ya nyumba kiasi kwamba tunaona ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba zote za Waziri Mkuu kipindi kilichopita tulikuwa na Mpango Mkakati wa Serikali wa miaka mitano, jinsi gani imejipanga kujenga ile *Kisarawe Freight Station* kwa ajili ya kuhakikisha mizigo iliyokuwa bandarini iweze kutoka na kuja kwenye bandari kavu Kisarawe. Nimepitia hotuba ya Waziri sikuliona hili. Naomba Waziri Mkuu anapohitimisha anatutolea kauli gani watu wa Kisarawe kuhusu ujenzi wa bandari kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba tuelezane wazi, ujenzi wa bandari kavu Kisarawe siyo kwamba itawafaidisha watu wa Kisarawe isipokuwa itapunguza ule msongamano wa Jiji la Dar es Salaam. Tukijenga bandari kavu ya Kisarawe maana yake tunaenda kuchochea uchumi wa Tanzania. Leo hii ni magari mangapi yananasia kutoka Kibaha mpaka kuingia katikati ya Mji? Kama bandari kavu ya Kisarawe ingekuwa imejengwa, malori yote tungeyapiga marufuku kuingia katikati ya mji. Nina imani jambo hili lingeweza kusaidia sana kuchochea uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nikasema hapa, pale kuna mwekezaji mwingine tayari ameshaweka na hatua za awali kabisa, jinsi gani Serikali inasukuma hili? Kwa hili, naomba nipate majibu sahihi kwa sababu kuna habari za kutatanisha kwamba bandari kavu ile inataka ichakachukuliwe. Ninaamini jambo hili haliwezi kuwezekana kwa sababu mpango ule uko kwenye Mpango wa Taifa wa miaka mitano, bandari kavu ile itajengwa. Lengo ni kuchochea uchumi wa Tanzania hali kadhalika kuleta ajira kwa wana wa Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba nizungumzie huduma ya afya. Naishukuru sana Serikali, tulipokuja kutoa hoja hapa kwamba Hospitali yetu ya Wilaya tangu mwaka 1975 ilikuwa haina *mortuary*, Serikali imetusaidia sasa hivi tumepata *mortuary*. Tumefanya *record* ya kutosha, miaka yote tulikuwa na zahanati 18, kipindi hiki kifupi mpaka ikifika Desemba tutajenga zahanati mpya 22. Sasa naiomba Serikali itusaidie na siyo Kisarawe peke yake, kuna tatizo la wahudumu wa afya maeneo mbalimbali, hakuna wauuguzi, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba zahanati zilizojengwa zinapata wataalam wa kutosha ili mradi wananchi waweze kupata huduma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kuzungumzia suala zima la miundombinu ya barabara. Najua Ilani imezungumza lakini juhudi za upembuzi yakinifu na *detail design* imeshakamilika lakini tulikuwa tunatarajia mwaka huu barabara ya kutoka Kisarawe mpaka Mananemango ingekuwa imeshanza kujengwa mpaka sasa inaonekana *flow* ya pesa siyo nzuri. Bahati nzuri hapa Naibu Waziri wa Fedha yupo, Serikali itafanyaje kuhakikisha kwamba pesa zinakuja ili ujenzi wa barabara zile ziweze kuendelea? Kwa sababu tuna imani kubwa, ujenzi wa barabara zile zitachochea kwa kiwango kikubwa ukuaji wa uchumi. Leo hii ukienda ofisi ya TANROAD hali siyo nzuri sana kutokana na mtiririko wa fedha za Mfuko wa Barabara. Hazina itafanya vipi kuhakikisha TANROAD inapewa fedha zake kama ilivyopitishwa na Bunge hili ili kazi katika Halmashauri yetu iweze kwenda vizuri. Mimi nina imani tukifanya haya, haya ndiyo matatizo ya wananchi wetu yanayotukabili katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika suala zima la maji, nashukuru sana *investment* iliyofanyika katika miaka mitano hii tumesaidia kujenga visima katika vijiji 27. Kwa mara ya kwanza angalau baadhi ya vijiji wananchi wanaanza kuona maji ya bomba yanatiririka. Hata hivyo, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu, katika miradi mikubwa, tuna mradi kule Chole ambao una karibu shilingi *1.5 billion* ni za ujenzi wa lambo, mradi wa Kiluvya, mradi wa Mafizi, miradi hiyo yote sasa imekwama kwa sababu *flow* ya pesa siyo nzuri, wakandarasi wameondoa mitambo kutoka *site*. Bahati mbaya, kazi inaposhindwa kukamilika kwa muda gharama ya mradi inaongezeka. Kibaya zaidi kule kuna lambo moja ambalo nimesema gharama yake ni shilingi

bilioni moja na milioni mia tano, mvua hii inavyonyesha lile lambo likiharibika maana yake *variation* ya mradi ule itafika mpaka shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapofanya maamuzi kama haya, naiomba Serikali tuhakikishe *flow* ya pesa kwa kipindi hiki kilichobakia inakwenda vizuri twende tukamalize matatizo yale. Nimekutana na Katibu Mkuu pale amesema kweli changamoto ni ya fedha, najua Waziri wa Fedha na Naibu wake wako hapa atatueleza. Kwa sababu suala la maji, najua Serikali imefanya juhudi kubwa lakini tutafanya vipi kuhakikisha miradi iliyopangwa mwaka huu wa fedha inakamilika ili wananchi waweze kuona kwamba sasa yale matarajio waliyoyapata yanaendelea kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la madai ya watumishi naomba nilizungumzie. Nilisema pale mwanzo lakini kikubwa zaidi nataka tuhakikishe kwamba watumishi wandalipwa kwa sababu najua kwamba tusipowalipa vizuri mwisho wa siku ni kwamba wanakosa morali ya kazi, wakikosa morali ya kazi maana yake ufanisi hauendi vizuri. Mimi nawathamini sana watumishi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu mafanikio haya makubwa yaliyopatikana wamefanya wao. Kwa hiyo, tuhakikishe watu hawa wanafanya kazi wakiwa na ari ya kutosha na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho naomba kuzungumzia suala zima la ada ya mitihani ya wanafunzi. Sasa hivi kuna wanafunzi wengine mpaka leo hii hawajalipa ada ya mitihani wa *Form IV* na *Form II*, ina maana mpaka leo hii ukiona mtu hajalipa ada ya mitihani mzazi wake hana uwezo. Serikali inatamka nini kuhusu suala hili? Wale wazazi ambao mpaka leo hii hawajalipa ada za mitihani, tuwape msamaha, nadhani hii itakuwa ni jambo kubwa sana kwa Watanzania. Kwa sababu leo hii tukisema kwamba kulikuwa na *deadline* na kila mwezi ile gharama inaongezeka, je, Serikali imejipanga vipi katika suala hili? Naomba Waziri Mkuu atupe majibu ya suala hili. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Mbowe.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili name nitoe mchango kidogo tu kwa muda mfupi niliokuwanao kwa mambo machache tu ambayo ningependa pengine kuya-address kwa Waziri Mkuu na timu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na Jiji la Dar es salaam. Kama kuna mahali ambapo tunapata aibu ni Jiji la Dar es Salaam na kama kuna eneo ambalo Serikali inahitajika kutoa majibu siyo tu ndani ya Bunge na Watanzania waelewe ni Jiji la Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika historia ya nchi yetu baada ya kupata uhuru Jiji la Dar es salaam limefanyiwa *master plan* mara mbili, naomba Waziri Mkuu anisikilize kwa makini. Mara ya kwanza tulifanya *master plan* ya Jiji la Dar es Salaam mwaka 1968 wakati huo kulikuwa kuna wakazi 273,000 katika Jiji la Dar es Salaam na hakukuwepo na watu wanaoishi eneo ambalo halijapimwa. Watu waliishi Magomeni kumepimwa, watu waliishi Kinondoni, Gerezani, Temeke, Tandika, Upanga na Sea View.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *master plan* ya pili ya Jiji la Dar es Salaam imefanywa mwaka 1979 yaani miaka kumi baadaye chini ya utawala wa mtu yuleyule Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Wakati huo *population* ya Jiji la Dar es Salaam imeongezeka kutoka wakazi 273,000 ya mwaka 1968 mpaka wakazi 770,000. Hiyo ndiyo *master plan* ya mwisho Ndugu zangu Wabunge

kufanyika kwa Jiji la Dar es Salaam. Tunapozungumza leo ni miaka 36 imekwisha, siyo utawala wa Mwinyi, siyo utawala wa Mkapa na siyo utawala wa Kikwete ambao umewaza kufanya *master plan* ya Jiji la Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *population* ya Dar es Salaam tangu *master plan* ya mwisho imefanyika miaka 36 iliyopita imeongezeka imefika 4.5 million people. Tunapozungumza leo asilimia 72 ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wanaishi kwenye maeneo ambayo hayajapimwa. Ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam katika Afrika ni mojawapo ya Majiji yanayokua kwa kasi sambamba na Jiji la Mwanza na Jiji la Mbeya kwa sababu ya kuhama kwa watu kutoka maeneo ya vijiji kuja maeneo ya mjini kitu ambacho kinaitwa *rural urban movement*. Sasa hii *rural urban migration* inasababisha watu wengi ku-migrate to the cities or urban centres kwa sababu ya hali ngumu ya maisha huko vijiji, kwa sababu tumeshindwa kuwa na *economic policies* ambazo ni *sustainable* ili kuwa-sustain watu wetu katika maeneo ya vijijini, watu wetu wanaona kuna neema mjini wanakimbilia mjini lakini sisi tunawapokea mjini hatuna miundombinu ya kuwapokea watu kwa Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Jiji la Dar es Salaam lina *traffic* ambayo ni aibu, si kwamba tuna magari mengi sana. Jiji la Nairobi lina magari mara ya tatu ya magari ya Dar es Salaam na hizi takwimu zipo. Dar es Salaam kuna mambo matatu makubwa. La kwanza, *lack of planning*. Hakuna *planning*, hakuna *master plan*. Atakuja Waziri wa Uchukuzi hapa sijui Waziri wa Barabara atasema tunajenga *flyover TAZARA, that is not a solution to Dar es Salaam crisis*. Hizo *flyovers* tumezungumza tangu Bunge hili la Kumi limeanza, tunamaliza Bunge la Kumi tunazungumza tu, TAZARA itajengwa, Ubungo itajengwa, sijui wapi itajengwa, havijengwi, tukiwaambia mmechoka mnasema ooh Wapinzani hamna shukrani. Mmefanya ndiyo lakini mliyofanya hayalingani na kile ambacho kilistahili kufanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, adha ya *traffic*, yaani mtu unakwenda ofisini Dar es Salaam au kwa sababu ninyi wenzetu mnakwenda na *motorcade* hamjui hili tatizo. Nimesikia na mapendekezo yanatolewa wanunuliwe helikopta ili watumie helikopia kwenda ofisini, halafu nani aingie kwenye *traffic*? Mimi nashauri tu viongozi wetu hawa waondolewe *motorcade* angalau kwa mwezi mmoja labda watajua maana ya *congestion* ya Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza masaa matatu kwenda ofisini halafu unapoteza masaa mengine matatu ya ku-burn fuel kurudi nyumbani. Mtu una spend masaa sita Dar es Salaam kwenda ofisini. Kuna watu siku hizi hawaendi ofisini shauri ya kuogopa *traffic* barabarani, sisi tunaona ni mambo ya kawaida tu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna sababu chungu nzima, kwanza kuna *environmental problem*. Magari yanasimama barabarani masaa matatu yanachoma fuel, tunaongeza cost ya *transportation* in Dar es Salaam, hizo ni *economic factors*. Tunaongeza *green gases* yaani kuna *impact* kwenye *environment* kwa sababu magari yanachoma mafuta yamesimama *idle* tangu mjini mpaka Mbezi, Kimara, Mbagala, magari hayaendi kwa sababu *infrastructure* wala *planning* hakuna. Sasa ni Serikali gani mnakosa *planning*? Kwa sababu hili jambo siyo la kuzuka na nakuambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika kipindi cha miaka miwili ijayo, Dar es Salaam kutakuwa hakuna *movement*. Kwa sababu *plan* zote, hata mkajenga *flyover* za TAZARA, mkajenga *flyover* ya Temeke Chang'ombe pale, makajenga *flyover* ya Ubungo ama mkajenga *intersection* za Morocco na kila mahali, haitakuwa ni *solution* ya kutosha kwa pace ya ongezeko la watu na magari inavyoongezeka Dar es Salaam, *where is the master plan*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *capital* ambayo inachangia kwenye *revenue* ya Taifa kwa asilimia 70 – 80, haina *infrastructure*, mnategemea nini, *where are the plan*? Mnakaa hapa

mnatuambia tu tutaongeza barabara, kuna mradi wa magari yanayokwenda kwa kasi, ndiyo magari yanayokwenda kwa kasi mangapi? Ukienda katika matatizo mengine ya kihuduma, ukiwa na mgonjwa leo Dar es Salaam anachukuliwa na *ambulance* anakimbizwa Muhimbili, kama hakufia barabarani una bahati. Kuna watu wanakufa bila sababu za msingi, *why, traffic!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia barabara inayojengwa leo ya Morogoro kuingia Dar es Salaam, *this is the main road* ambayo ina *feed* Dar es Salaam kutoka Zambia, Uganda, Kaskazini mwa nchi yetu, Kenya, Malawi, Kongo, Burundi, Rwanda mnajenga barabara ya *two lanes*. Nendeni mkaangalie Kenya hapo kitu kinachoitwa *Thika super highway* ina *lanes* kumi. Mnajenga *lane* mbili tena *vi-lanes* vyembamba, malori yakipishana yanaacha futi moja kati ya roli na roli, leo? Watu wanajenga barabara zina *lane* kumi, ninyi mnajenga *lane* mbili halafu mnasema mnafanya *planning*, Waziri Mkuu mnafanya *planning* gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema jamani, mambo mengine tuache utani wa kisiasa, Dar es Salaam ni *disaster*, inahitaji *SOs*, Dar es Salaam inahitaji *Special Operation* na wala siyo kuunda Kamati za Wanasiasa wala Kamati za Wataalam *otherwise* Jiji la Dar es Salaam linakwenda kusimama siyo zaidi ya miezi minne ijayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA*, kwa takwimu za mwaka 2011 kwenda mwaka 2013 walikuwa wana-*register* magari *an evarage* ya *1.2 million cars a year* na *70%* ya magari haya yanabaki Dar es Salaam. Barabara hakuna na hakuna mpango wa kupanua barabara, mnaweka *lane* mbili, *lane* mbili leo! Barabara inayo-*feed* mataifa nane mnaweka *lane* mbili za barabara, *where is the planning?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimesema nizungumze haya, watu wanapata *frustration*, watu wanapata *stress*, unakuta watu wamekaa kwenye *traffic* saa nne, saa tano, watu wanapata *stress*, wanaugua magonjwa ya ajabuajabu, wanavuta hewa chafu, ninyi mnapita na magari yenu yenye vimulimuli, mna *motorcade* hamuoni hili suala na mnashindwa kufanya *planning*, ni kwa nini msiondoke Serikalini tuingie watu wengine tubadilishe mambo haya? Kwa sababu *you simply cannot plan?* Kama Serikali haina *plan* ni kwamba Serikali haina *future*, *there is no future in this country*. Mnafanya kazi ya kupanga mpango wa kuongoza Serikali, mipango ya maendeleo ni miaka mitano, mnafikiria uchaguzi ujao, kwa hiyo mtapanga *plan* za miaka mitano, hamfikirii *30 years to come!* Inakuwaje Jiji la Dar es Salaam leo miaka 36, jamani hakuna *master plan*, mnaongea nini halafu tunadanganyana hapa, miaka 36 *there is no master plan!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia *flats* za Dar es Salaam, nilikuwa namwangalia Mheshimiwa Rais jana alitembelea mafuriko Dar es Salaam, Mheshimiwa Rais anauliza kwa nini haya maji yamesimama, nyumba mpaka kwenye *lintel* zimejaa maji wiki nzima, mvua zimeshakatika nyumba zimejaa maji, kisa, watu wamejenga wamezuia mitaro, hakuna *drainage system*. Leo tunazungumza habari ya visima, unasikia Wabunge wanasimama wanasema tunashukuru sana tumepewa visima, visima ni jambo la kuringia, ni mambo ya aibu leo *21st century* tunaongelea habari ya visima! Dar es Salaam ni *disaster*, *floods* kidogo tu watu wanaumia, kazi hazifanyiki. *Impact* yake kwenye *economy* hasa uki-*consider* kwamba Dar es Salaam ndiyo ina mchango mkubwa katika *economy* ya nchi hii, *impact* ya *traffic* Dar es Salaam *economically is enormous*.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dar es Salaam mnaitolea ufumbuzi gani kabla hamjaondoka Oktoba kwa sababu Novemba tutaingiza watu wenye vichwa wafanya kazi lakini *before we move into the office in October*, tunataka *between now and October* mtafute *temporary solution*, kwa sababu *after November is our job* siyo ya kwenu tena lakini mnachokifanya hapa kati ya sasa hivi na Novemba ni nini? Mnaacha nchi kwenye *mess* ya ajabu. Mnajisifiasia tu

hapa, Serikali ya CCM imefanya hiki, mmeacha nchi kwenye mess ya ajabu! Nimemaliza Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongee kitu kingine kimoja ambacho kwa kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu hiki nikuambie tu kwa sababu na wewe ulinikwaza sana hapa. Waziri Mkuu nilikuletea mradi wangu wa umeme katika Jimbo langu la Hai, mradi wa Kikuletwa ambao ulipangwa kufanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Hai, siyo Mbowe, mkakataa huu mradi usifanyike. Sisi kama Halmashauri ya Wilaya tulitafuta fedha za kujenga ule mradi, *over 20 million dollars* na tulikuwa na fedha na tulishasaini MOU. Tukaomba Serikali ule mradi wa Kikuletwa muurudishe Halmashauri ya Wilaya ya Hai tutengeneze *10 megawatts of power* isaidie Kilimanjaro na Mikoa jirani, mkakataa, mkasema mnawapa Chuo cha Ufundi Arusha, haya mmewapa, nikikuambia Waziri Mkuu hawa hawana *business plan*, hawana *finances*, hii kitu ni *white elephant like the white elephant to date, it will be white elephant tomorrow.* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema huko mbele ya safari, tuwe tunasikiliza na matakwa ya Halmashauri zetu za Wilaya. Kuna mambo mengine tunataka tuyafanye kwa nia njema, msione vivu kama ni Halmashauri inaongozwa na CHADEMA, CUF au CCM. Cha msingi ni kwamba kama mradi una manufaa kwa wananchi, ni lazima viongozi wetu wa Serikali muwe mna uwezo wa kusikiliza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilimletea Waziri Mkuu nikamuomba *in person*, Mheshimiwa Waziri Mkuu saidia huu mradi tupate Halmashauri ya Wilaya ya Hai, uka-*promise* utasaidia baadaye ukaenda ukaugawa kwa Chuo cha Ufundi Arusha bila hata ya kutueleza kwamba mmeutoa kwa sababu gani, matokeo yake haijajengwa, ile ni *potential* ya kuzalisha *hydroelectric power* ambayo ni *cheap electricity*, imekaa pale, inaozea pale, ni kwa sababu hamkuona kwamba kuna sababu ya kujenga hii Halmashauri kwa sababu pengine inaongozwa na CHADEMA. Mambo kama haya katika masuala ya maendeleo sidhani kama ni ya msingi sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda niliongelee sijui kama muda utaniruhusu ni suala la ushirikino wa nchi za Afrika Mashariki. Japo hili tutalizungumza tena wakati wa hotuba ya Mambo ya Nchi za Nje lakini kwa miaka...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nitoe hoja ya kubadilisha Kanuni na kabla ya kutoa hoja hiyo, naomba nitoe maelezo mafupi yatakayopelekea kujengwa kwa hoja hiyo ambayo itaamuliwa na Bunge lako ili kubadilisha Kanuni zifuatazo.

Kwa kuwa Mkutano wa Ishirini wa Bunge wa kushughulikia bajeti ya Serikali pamoja na shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa, umepangwa kumalizika tarehe 27 Juni, 2015;

Na kwa kuwa muda tulio nao wa kushughulikia bajeti ya Serikali katika mkutano huu ni siku 40 ambazo ni chache hivyo kulazimika kupata muda wa ziada ili kuwezesha Bunge kupata muda wa kutosha wa kujadili bajeti;

Na kwa kuwa katika kikao cha Kamati ya Uongozi ya Bunge, kilichofanyika tarehe 15 Mei, 2015, Wajumbe wote wa Kamati hiyo waliohudhuria waliazimia kuliomba Bunge likubali kutengua baadhi ya Kanuni kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa muda wa kutosha kufanya kazi za Bunge hili;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shuguli za Bunge, katika Mkutano huu wa Ishirini, Kanuni ya 28(15), Kanuni ya 99(8), (9), (12) na (13) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 28(15) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge halitakutana siku za Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko itenguliwe na badala yake Bunge likutane siku za Jumamosi za tarehe 16 Mei, 2015, tarehe 23 Mei, 2015, tarehe 30 Mei, 2015, tarehe 6 Juni, 2015 na tarehe 27 Juni, 2015 kuanzia saa tatu asubuhi hadi saa nane mchana isipokuwa kwamba siku hiyo hatutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 99(8) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba muda wa Waziri anayewasilisha hotuba utakuwa ni dakika zisizozidi sitini itenguliwe na badala yake muda wa dakika 45 utumike kuwasilisha hotuba za Mawaziri kwa Wizara zote zilizopangwa kwa siku za Jumamosi na Wizara zilizopangwa mbili kwa siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 99(9) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba muda wa kuwasilisha maoni ya Kamati na ya Msemaji wa Upinzani utakuwa ni dakika zisizozidi thelathini itenguliwe na badala yake muda wa dakika ishirini utumike kuwasilisha maoni ya Kamati na ya Msemaji wa Upinzani kwa Wizara zote zilizopangwa siku za Jumamosi na Wizara zilizopangwa mbili kwa siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 99(12) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Mbunge anayejadili makadirio ya Wizara atasema kwa muda usiozidi dakika kumi itenguliwe na badala yake muda wa dakika saba utumike kwa Mbunge atakayejadili makadirio ya Wizara zote zilizopangwa siku za Jumamosi na Wizara zilizopangwa mbili kwa siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 99(13) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Waziri mtoa hoja atajibu ndani ya muda wa dakika sitini itenguliwe na badala yake muda wa dakika arobaini utumike kwa Waziri mtoa hoja kujibu kwa Wizara zote zilizopangwa siku za Jumamosi na Wizara zilizopangwa mbili kwa siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)
MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Spika, ninayo maoni machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni uboreshaji na utoaji wa huduma katika maeneo mbalimbali nchini. Haya yafuatayo yanatokea:-

(i) Bado kuna baadhi ya watendaji wanafanya kazi *as if* tuko katika karne ya 17, hawajali kuwa dunia inabadilika, teknolojia imebadilika na maisha yanazidi kuwa magumu na bei ya vifaa inapanda na itazidi kupanda;

(ii) Hawajui umuhimu wa kujali wakati na namna ya *ku-manage* muda wao wa kazi ipasavyo na umuhimu wa kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma;

(iii) Wako wanaoleta siasa katika kazi zao, *bureaucracy* zisizo na maana bado zinaendelea, jambo la kutatuliwa kwa siku moja linachukua wiki;

(iv) Siri za ofisi zinavuja na kuwafikia wasiohusika.

(v) Udhhibiti wa vifaa vya ofisi umepungua, karatasi za kuchapia na kudurufu ndizo zinazotumika kufungia vitu;

(vi) Bado *Undugunization* na urafiki kwa baadhi ya viongozi unaendelea. Tumeona katika nafasi za ajira zilizotolewa na waliopata kazi; na

(vii) Usimamizi ni hafifu.

Mheshimiwa Spika, pili, uwezashaji wa wananchi kiuchumi kwa lengo la kuboresha hali zao za maisha. Kazi kubwa inafanywa na Serikali ya:-

(i) Kuelimisha wananchi juu ya ujasiriamali;

(ii) Upatikanaji wa mikopo mbalimbali; na

(iii) Kuendeleza kilimo, uvuvi na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, sasa tuelekeze nguvu zetu kwa:-

(i) Kuwasaidia wajasiriamali kupata masoko ya bidhaa zao. Wengi wanaojiingiza kwenye kilimo wanakosa masoko ya mazao yao;

(ii) Elimu ya kusindika mboga mboga na matunda itasaidia sana kwao na upatikanaji wa zana za kuwawezesha kutekeleza kazi hiyo;

(iii) Umuhimu wa kuzingatia vifungashio vya mazao na vifaa vya usindikaji ili waweze kusafirisha bidhaa zao nje ya nchi na kuongeza tija;

Mheshimiwa Spika, tatu, huduma za wavuvi na jinsi ya kumwezesha mvuvi ili aweze kuishi na kuendeleza kazi hiyo.

Tumsaidie kwa kuondoa kodi katika vifaa vya uvuvi kama mashine/injini, nyavu na siyo nyuzi tu. Wasaidiwe kama walivyosaidiwa wakulima.

Aidha, tuendeleze ufugaji wa samaki kwani utasaidia sana hasa kwenye maeneo yasiyo na bahari na maziwa. Hii ni *source* nzuri ya *protein*.

Mheshimiwa Spika, nne, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu isaidie:-

(i) Upatikanaji wa fedha za kutosha za maendeleo katika Bunge ili ofisi za Wabunge zijengwe na zile zilizojengwa zimaliziwe, zikarabatiwe ili Waheshimiwa Wabunge waweze kupata maeneo ya kufanyia kazi.

(ii) Makabidhiano (*official*) yafanyike kati ya Bunge na Ofisi ya Waziri wa Mkuu – Tawala za Mikoa (zile ofisi za Wabunge zilizokamilika). Makabidhiano yawe na *assets* pamoja na *liabilities* zote ili shughuli zisije zikakwama pale fedha itakapopatikana.

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA: Mheshimiwa Spika, kwanza, kabisa naomba nichukue fursa hii kuipongeza Kamati ya UKIMWI, kupitia Serikali kwa kuona umuhimu katika kupambana na ugonjwa wa UKIMWI kwa kuanza kutenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya Mfuko huu. Ni imani yangu kwamba kiasi hiki kitaongezeka kwa kuiga mifano ya nchi za wenzetu kama Zimbabwe, Botswana Afrika ya Kusini, Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, pili, mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi, ni aibu kwa nchi yetu. Inapokaribia Uchaguzi Mkuu, mauaji ya Albino yanashamiri kwa imani potofu waliyonayo baadhi ya watu na waganga. Naiomba Serikali wawanyonge wote ambao wanajihusisha na unyama huu.

Mheshimiwa Spika, tatu, Muungano wetu umetimiza miaka 50 sasa toka uasisiwe na viongozi wetu ambao walikuwa na nia nzuri tu kwa wananchi wa pande zote mbili, Bara na Zanzibar. Kinachonisikitisha, miaka 50 ya Muungano huu bado kero zenye maslahi kwa wananchi wa Zanzibar mnasema eti mnaendelea na vikao kutatua zilizobakia za mgawanyo wa mapato ambao unajumuisha mgao wa misaada kutoka nchi za nje, misamaha ya mikopo, hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, faida ya Benki Kuu, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, ushiriki wa Zanzibar katika taasisi za nje, ajira za watumishi wa Zanzibar katika taasisi za Muungano, usajili wa vyombo vya moto na Tume ya Pamoja ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, hizi zote ni kero za Muungano, je, Serikali hizi mbili zina nia kweli ya kumkomboa Mzanzibar ambaye uchumi wake umeshuka kwa mtu mmoja mmoja? Naiomba Serikali kama ina nia ya kweli ya kumkomboa mwananchi wa Zanzibar baada ya miaka 50, sasa basi umefika wakati wa kutatua kero zote zilizobakia. Ni lini Serikali itatutua kero zote zilizobakia?

Mheshimiwa Spika, nne, Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Kila mtu aliyetimiza miaka 18 ana haki ya kuandikishwa na kupewa kadi ya kupigia kura ili mradi tu awe ametimiza vigezo vyote vinavyotakiwa na Tume.

Mheshimiwa Spika, kusema kuwa mpaka wafu wanapiga kura hatuna maana ya kuwa amefufuka lah. Mpango unatumika vipande vya marehemu hao, picha zinatolewa zinabandikwa picha nyingine lakini jina linatumika lile la marehemu. Fanyeni utafiti kama mna nia ya dhati ya kufanya uchaguzi wa haki na amani na Masheha ndiyo tatizo kwa Zanzibar hawatoi haki.

Mheshimiwa Spika, tano, Mfuko wa TASAF umeundwa kwa lengo la kusaidia kaya maskini. TASAF awamu ya I, awamu ya II na sasa tuna TASAF awamu ya III, nataka kujua tathmini ya awamu zote kama imefanyika na ni kwa kiasi gani imefanikiwa kumtoa mwananchi anayeishi katika kaya maskini kuondokana na umaskini?

Mheshimiwa Spika, naomba kufahamu kwa upande wa Zanzibar, mfuko huu unaratibiwa na ofisi gani na kaya ngapi zimefikiwa kwa kila Wilaya?

Mheshimiwa Spika, sita ni suala la madini. Tanzania tumejaliwa na aina nyingi sana za madini na kama tungekuwa tunayatumia vizuri basi shida ingekuwa hakuna.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli lazima tujifunze tunapokwenda katika nchi za wenzetu. Mfano Afrika ya Kusini, mji wa Johannesburg tulipokuwa kwenye ziara za Bunge tuliambiwa kwamba mji ule umejengwa kwa pesa za madini tu. Mfano mwingine ni Zimbabwe, kuna madini ya almasi nyeusi ile ya kukatia vioo, mwekezaji wa Kichina alipewa masharti na Rais Mugabe kwamba lazima ajenge nyumba za Askari, shule na *mall* ndipo achimbe na vyote hivyo amejenga tumeona.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali tufuate mifano ya nchi za wenzetu kutumia madini yaliyomo nchini kwa kuwapa masharti wawekezaji wa nje ili kuleta manufaa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Maana Mawaziri mnasafiri kila nchi, mnaona miji ya wenzetu ilivyopangika tuige basi na sisi kwa kutumia rasilimali zetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, saba ni Benki ya Wanawake. Ni muda mrefu sasa Benki ya Wanawake imezinduliwa na kutoa huduma kwa Tanzania Bara. Nataka kujua ni lini Benki ya Wanawake itafunguliwa Zanzibar?

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo, naomba kuwasilisha. Ahsante.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa mema yote. Katika Hotuba hii nianze na suala la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kupitia Kamati ya UKIMWI kwa kuona umuhimu wa kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa UKIMWI. Hii yote ni kuhakikisha kuwa, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya udhibiti wa UKIMWI unakuwa endelevu na kuondoa utegemezi kwani mtumiaji wa dawa za ARV hatakiwi kukoma hata siku moja. Hivyo, ombi langu kwa Serikali ihakikishe fedha zinasimamiwa ili zitumike kama jinsi zilivyopangwa na ziwafikie walengwa wote bila ujanjaujanja.

Mheshimiwa Spika, kumezuka tabia mbaya kwa watumishi wa afya kuuza dawa za ARV kwa waathirika wanaotumia dawa hizo kitu ambacho ni hatari. Wanaoshindwa kupata fedha za kununua wanaugua sana na kuvimba majipu, ni hatari. Naomba Serikali ikemee sana tabia hii.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye suala la reli. Serikali imesema imeboresha miundombinu katika reli kwa kununua injini mpya lakini tukumbuke reli ni kichocheo cha uchumi nchini. Pia wananchi karibu wote wenye kipato cha kawaida wanategemea treni kwa ajili ya usafiri na usafirishaji. Masikitiko yangu kwa Serikali ni injini zilizoletwa Mpanda. Injini tunazotumia Mpanda – Tabora ni mbovu sana tena ni mitumba. Injini zile ziko mbili ambazo ni 73 *class*, hazifai kabisa! Hazina hata uwezo wa kusukuma mabehewa 10. Injini hizo zinafeli kupanda mlimani, je, hii si hatari?

Mheshimiwa Spika, mazao yamelundikana katika stesheni ya Mpanda ambayo yalikuwa yanapelekwa Kaskazini. Ombi langu kwa Serikali, ituletee injini Mpanda 90 *class* ambazo zina uwezo wa kusukuma mabehewa mengi, kupanda mlima bila wasiwasi na usalama kwa wananchi. Kwa kufanya hivyo, mtakuwa mmetutendea haki Mkoa wa Katavi – Tabora ambao tumeachwa nyuma sana kwa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, barabara na madaraja. Pamoja na Serikali kusifia miundombinu nchini, ni kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, katika awamu zote ni Awamu ya Nne iliyojitahidi katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja, lakini wanaoangusha Serikali ni watendaji. Barabara zinazojengwa hazizingatii viwango, wasimamizi wa miradi

hawana uchungu wa fedha za walipa kodi wala uchungu wa nchi yao. Tumeona barabara na madaraja yakijengwa na kudumu kwa muda mfupi kisha kuharibika, huko ni kutumia fedha vibaya.

Mheshimiwa Spika, ipo Mikoa iliyosahaulika nchini kama Mkoa wa Katavi na Rukwa. Serikali inaelewa kama Mkoa wa Katavi na Rukwa ni Mikoa inayozalisha chakula kwa wingi nchini na yenye rasilimali nyingi lakini tumesahaulika sana kwa barabara za kiwango cha lami. Mfano barabara za Mpanda – Sumbawanga, Mpanda – Mishamo na Mpanda – Inyonga – Koga, miradi hii yote imesimama na kuwaacha wananchi wetu hoi na uchumi wetu kuyumba. Naomba Serikali inipatie majibu wakati wa majumuisho ni kwa nini mradi wa barabara ya Mpanda – Sumbawanga kupitia Kibaoni umesimama na ni lini utakamilika?

Mheshimiwa Spika, daraja la Mto Kavuu ujenzi wake unasuasua sana. Je, Serikali ipo tayari kutumia fedha za Mfuko wa Barabara na siyo za maendeleo ili mradi uende vizuri? Naomba majibu hayo.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye elimu. Serikali imesema imeboresha miundombinu ya elimu. Ni kweli Serikali imejenga shule katika kila Kata lakini imeshindwa kuboresha miundombinu ya elimu mfano shule za sekondari. Nashauri yafuatayo:-

(i) Kuhusu mimba kwa wanafunzi, nashauri watoto wa kike wajengewe hosteli hasa wale wanaofaulu na kupangiwa shule za mbali na makazi yao. Bodaboda ni kichocheo kikubwa kwa watoto wetu kupata mimba wakiwa shuleni.

(ii) Shule nyingi hazina maabara. Sasa tutapataje wanasayansi kwa kusoma nadharia? Kwa soko la ajira, tutaendelea kutawaliwa na Wakenya na nchi nyingine za jirani *because of lack of competence*.

(iii) *TEHAMA* haiwezi kwenda kama Walimu hawajaandaliwa mazingira. Serikali ingeweka maandalizi ya miaka mitano kuhakikisha kila shule ina umeme na komputa za kujifunzia, kwani wapo Walimu hawajui hata kutumia komputa.

(iv) Shule nyingi hazina visima virefu vya maji safi na salama kwa mahitaji ya wanafunzi. Nashauri visima vichimbwe kila shule.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, naomba nianze na kukupongeza wewe, Naibu Spika, Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote na Makatibu Wakuu katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Hali ya siasa nchini Tanzania; pamoja na kuwepo demokrasia ya kutosha katika nchi yetu, napendekeza kuwa Serikali ichukue hatua madhubuti kuhakikisha kuwa Vyama vya Siasa vinavyovuruga amani katika nchi yetu vinachukuliwa hatua za kisheria ili kuendeleza amani, umoja na mshikamano katika nchi hii.

Hali ya usalama kwa wananchi wa Tanzania si imara kwani kuna vitisho vya maafa, ujambazi, mauaji ya watu wenye ulamavu wa ngozi, matabaka kati ya matajiri na maskini, rushwa na kukosekana kwa haki katika vyombo vya maamuzi.

Ajali za barabarani; napendekeza sheria kali zitungwe ili kudhibiti ajali hizi. Pia suala la rushwa kwa Maafisa Usalama wa barabarani lishughulikiwe kikamilifu.

Ofisi za Wabunge Majimboni; napenda vile vile kusisitiza Serikali iangalie utaratibu wa kujenga Ofisi za Wabunge Majimboni ili kurahisisha utendaji kazi wa Mbunge awapo Jimboni kwake.

Haja ya kujenga *Bunge Tower* – Mjini Dodoma/ Dar es Salaam. Badala ya kupanga ofisi mbalimbali Mjini Dodoma au Dar es Salaam, nashauri yajengwe majengo makubwa mawili moja Dar es Salaam na lingine Dodoma ili yatumike kwa shughuli mbalimbali za Wabunge (Ofisi za Wabunge) na hata Kamati za Bunge.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi; napendekeza iwezeshe ili ifanye kazi kwa juhudi ili kuhakikisha kuwa uchaguzi mkuu unafanyika katika kipindi kilichopangwa.

Haja ya kuligawa Jimbo la Uchaguzi Tarime; kwa kuwa Jimbo la uchaguzi la Tarime lina Halmashauri mbili za Tarime DC na Tarime TC. Napendekeza Jimbo hili ligawanywe katika Majimbo mawili ya Tarime Vijijini na Tarime Mjini. Jimbo la Tarime Mjini lijumuishe Kata zote za Halmashauri ya Mji na pia Kata zifuatazo ziongezwe katika Jimbo la Tarime Mjini; Manga, Komawa, Kiore, Mwema, Susuni, Bumeru, Nyagicheri na Sirari. Jimbo la Tarime Vijijini lijumuishe Kata zote za Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Vigezo vyote vya kuligawa Jimbo hili vipo.

Msajili wa Vyama vya Siasa; napendekeza Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ajengewe ofisi ili iwe rahisi kuvihudumia Vyama vya Siasa. Pia, kupunguza gharama ya uendeshaji wa shughuli husika badala ya kuendeshea shughuli zake katika hoteli au katika jengo la kupanga. Ofisi hii pia iwe na ofisi ndogondogo za Vyama vyote vya Siasa.

Suala la uwekezaji; kwa kuwa, wawekezaji wa nje tulionao ni matapeli, napendekeza wazawa wawezeshwe kwa kadiri iwezekanavyo ili uchumi wa Tanzania ushikwe na wazawa. Nashauri uwepo mjadala wa Kitaifa kuhusu namna bora ya kuwasaidia wazawa katika suala zima la uwekezaji. Halikadhalika wawekezaji matapeli kama wale wa migodi mathalani North Mara wachukuliwe hatua kali kwani wanaijumumu nchi yetu na rasilimali zake. Mheshimiwa Waziri Mkuu amini usiamini nchi yetu haiwezi kuendelea kiuchumi kwa kuwategemea wawekezaji uchwara. Ni wezi, ni matapeli, ni wahujumu uchumi, ni watoa rushwa namba moja. Nashauri mikataba yote ya uwekezaji ipitwiwe upya.

Suala la ajira kwa vijana wa Tanzania; nashauri Serikali iangalie utaratibu wa kuanzisha makambi ya kilimo kwa kila mkoa. Makambi haya yanaweza kuwa yale ya JKT na kila Mkoa uchukue vijana wasiopungua elfu kumi (10,000) ili walime mazao ya biashara, chakula, matunda, mboga, ufugaji na kadhalika. Pia Serikali ijizatiti kuwatafutia soko la mazao watakayolima. Pia, ianzishe viwanda vidogo vidogo vya kuongezea thamani mazao hayo. Pia Serikali ijenge utaratibu wa vijana wanaohitimu elimu ya vyuo vikuu wapewe semina ya ujasiriamali kwa lengo la kujijiri badala ya kutegemea ajira rasmi toka Serikalini.

Sekta ya Utalii; pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali kuingia ubia na Mashirika ya Ndege ya Kimataifa, bado napendekeza kuwa Tanzania iangalie utaratibu wa kuliwezesha Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ili linunue ndege zinazoweza kufanya safari za nje ya nchi hasa nchi za Afrika, Asia na Ulaya kwa lengo la kuleta watalii wengi wa kutosha hapa nchini. Tukiamua tunaweza na sasa tuamue.

Sera ya elimu; ifafanuliwe vizuri ili kutoa fursa kwa Watanzania ili waweze kuelewa inalenga nini hasa. Pia, nasisitiza kuwa mipango madhubuti iandaliwe ili sera hii ianze kutumika mara moja na haraka iwezekanavyo kwani itakuwa ni mkombozi wa elimu hapa nchini.

Suala la miundombinu – Bandari, Viwanda vya Ndege na Barabara; Tanzania ina nafasi kubwa ya kuinua uchumi wake endapo Bandari ya Dar e Salaam, Tanga, Mtwara na Bagamoyo zitaimarishwa na kutoa huduma bora kwa kuwa lango kuu la uchumi hapa Afrika Mashariki. Viwanja vya ndege vipanuliwe hasa vya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Zanzibar, Mwanza na hata Mtwara kwa lengo la kuongeza ndege za Mashirika ya Kitaifa ili kuwaleta watalii na usafirishaji wa wasafiri toka pande mbalimbali za Tanzania na nje ya Tanzania. Tukitumia viwanja vyetu vizuri na tukinunua ndege zetu wenyewe kwa hakika tutaibadilisha Tanzania.

Suala la barabara na reli ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Napendekeza barabara zetu zilindwe na sheria kali zichukuliwe kwa wale wote wanaozidisha mizigo na kuchangia kuharibu barabara. Reli ya Kati, Reli ya Kigoma, Reli ya Tanga – Musoma na kadhalika ziimarishwe na kujengwa au kuboreshwa ili kubeba mizigo mizito na hivyo kupunguza uharibifu wa barabara zetu.

Suala la rushwa; kama Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilivyopendekeza kuwa wala rushwa wachunguzwe, wakamatwe, washtakiwe, wahukumiwe, wafungwe, wafilisiwe na hata ikiwezekana sheria itungwe ya kuwanyonga. Suala la rushwa lisivumiliwe kabisa katika nchi hii.

Kuisemea Wilaya ya Tarime. Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba maswali yafuatayo kuhusu Tarime uyajibu kwa ustadi mkubwa:-

Kwanza, ahadi yako; kuufanya mji wa Sirari kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo imefikia wapi? Kuipandisha hadhi barabara ya Mangucha – Masanga – Gibaso hadi Mrito kuwa ya Mkoa imefikia wapi? Kuondoa tatizo la Maji katika Wilaya ya Tarime limefikia wapi na kuondoa kabisa kero ya Mwekezaji wa Mgodi wa North Mara hasa kuwalipa fidia wananchi walioporwa maeneo yao. Pia ahadi za mgodi kwa wananchi hao. Utekelezaji wake umefikia wapi?

Pili, ahadi ya Rais; kujenga Chuo cha VETA, Wilaya ya Tarime. Kujenga barabara ya lami toka Tarime Mjini kupitia Nyamwaga – Nyamongo hadi Mto Mara na kuwasaidia wazee wa mila wa Tarime usafiri.

Tatu, suala la umeme Tarime; Vijiji 60 vilivyooneshwa kupelekewa umeme hadi sasa ni nguzo tu zimewekwa chini zinaoza lakini hadi sasa umeme huo haujaonekana. Tafadhali namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ashughulikie suala hili kwa umakini wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuchangia mchango wangu kwa kuongea, lakini nalazimika kuyaleta kwa maandishi. Kwanza hoja ya Bunge kupatiwa kiwanja cha kujenga ofisi za watumishi wa Bunge na kupata eneo la kupaki magari ya Wabunge, ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani watu wa kawaida kupewa kujenga eneo la utawala, wakati Bunge na Waheshimiwa Wabunge wanahangaika, Serikali ni moja, hivyo basi naomba kama kuna Wizara yoyote ina kiwanja eneo la Bunge, Serikali iangalie utaratibu wa kuwatafutia eneo lingine ili Bunge lianze ujenzi huo mara moja. Mipango ya ujenzi iko tayari.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, naomba miradi yote iliyoko katika Jimbo la Kasulu Vijijini ipewe fedha na ikamilishwe kabla ya mwaka huu kwisha hasa miradi ya maji, barabara, umeme vijijini, vituo vinne vya afya ambavyo vimeshaanza kujengwa katika Kata ya Makere, Rungwe Mpya, Nyanchenda na Nyamidaho.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya Mipaka kati ya Vijijini vya Kagerankanda, Mvinza, Katoto na Kitongoji cha Rugufu. Mbaya zaidi Kitongoji cha Rugufu ambacho hata kwenye Chaguzi za Serikali za Mitaa kilizuliwa na mpaka leo hakijafanya uchaguzi. Sasa nataka kujua kwenye zoezi la kujiandikisha hawa wananchi wa Tanzania zaidi ya elfu 13 wataandikishwa au hawataandikishwa?

Mheshimiwa Spika, mbaya kuliko zote Viongozi wa Serikali Mkoa na Wilaya wanataka kuwahamisha wananchi wakizingatia kuwa wako kwenye hifadhi na baadaye wajamilikishe ardhi hiyo kwa maslahi yao. Kwa kuwa tumejua ni vema Serikali ilimalize hilo mapema.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne ni Wakimbizi. Naomba Serikali ipange utaratibu mzuri wa kuwadhibiti wakimbizi bila kuleta usumbufu kwa Watanzania waishio mipakani hasa wakati wa zoezi na tatizo la kamata kamata inayofanywa na Uhamiaji juu ya Watanzania waishio mipakani kwa kuwahisi kuwa ni Warundi. Nashauri wabuni utaratibu mzuri wa kuwatambua wasio Watanzania ili wasiwe chanzo cha fujo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Serikali ijipange kutoa maelekezo kwa Watendaji wote katika Halmashauri, wafanye kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na siyo kufuata maelekezo ya wanasiasa ambao wana hofu ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Waziri Mkuu, Waziri wa TAMISEMI, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa TAMISEMI, kwa kuisaidia Wilaya Misungwi kuiondoa katika migogoro iliyokuwa ikisababisha maendeleo katika Wilaya nzima kudumaa.

Inatia moyo sana kuona sasa mapato yanakusanywa mara nne ya yale yaliyokuwa yakikusanywa kabla ya hatua zilizochukuliwa na Waziri Mkuu. Barabara sasa zinajengwa kwa kiwango kinachoridhisha. Napenda kuwatia moyo muendeleo kuchapa kazi, Tanzania yetu itabadilika sana.

Mheshimiwa Spika, mwamko wa wananchi umekuwa mkubwa sana na sasa wanadai haki zao nyingi baada ya kuona mafanikio haya. Mafanikio haya yanaleta changamoto hasa katika vijiji vilivyo karibu na bomba la maji liendalo Shinyanga na Kahama.

Ikumbukwe kuwa maji haya chanzo chake ni Wilayani Misungwi katika Kijiji cha lhelele ambacho nacho hakina maji hadi leo. Kwa bajeti iliyopita vijiji vilivyokuwa kando ya bomba hili vilikuwa vipatiwe maji, lakini wananchi wanasikia sasa maji yanakwenda Tabora na Igunga na kadhalika. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu afuatilie suala hili ili wananchi wanaoshi sehemu ambazo maji yanatoka na wao waweze kupata maji.

Eneo lingine lenye changamoto ni Miradi ya Vijiji, zabuni zake zina utata sana kiasi cha kufikia hatua ya Bodi ya Zabuni kumwomba Mkurugenzi ampe onyo Mhandisi wa Maji kwa udanganyifu. Naomba Mheshimiwa Hawa Ghasia au Katibu Mkuu, mchukulieni hatua Mhandisi huyu aliyefanya udanganyifu kwa kuweka nyaraka za kughushi mbele ya Bodi ya Zabuni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Spika, kwanza, napongeza Hotuba zote mbili; ya Waziri Mkuu na Hotuba ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

Pili, naunga mkono hoja hizo.

Tatu, naomba kupata majibu juu ya hoja zangu zifuatazo nilizochangia kwa kuzungumza Bungeni jana tarehe 12 Mei 2015:-

(i) Ukurasa wa 77 - 78 wa Kitabu cha Hotuba ya Waziri Mkuu umezungumzia maeneo mapya ya utawala, yaani Mikoa 4, Wilaya 19, Kata na Vijiji, lakini maeneo hayo yalitangazwa Mwaka 2010 kabla ya Uchaguzi Mkuu na yanafanyiwa kazi hivi sasa.

Tulichotarajia baada ya miaka mitano kupita Serikali ingetangaza maeneo mengine mapya kama ilivyo kawaida yake. Kuna maombi mengi ambayo yaliwekwa kiporo mwaka 2010 yahusuyo Wilaya, Halmashauri, Kata na Vijiji. Mfano, Wilaya ya Manyoni na Mkoa wa Singida, zimeomba muda mrefu kugawanywa kwa kuwa Wilaya hiyo ni kubwa. Aidha, iwe na Wilaya mpya ya Itigi au iwe na Halmashauri nyingine mbili kutokana na upana wake ili kusogeza huduma na ufanisi kwa wananchi. Naomba majibu ya Serikali juu ya hoja hii muhimu.

(ii) Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itenge Bajeti kwa ajili ya kuhakiki mipaka ya ndani ya nchi kupunguza migogoro mingi ya mipaka ili kudumisha utulivu na kuwapa nafasi wananchi kufanya shughuli za maendeleo bila kero.

Kwa mfano mgogoro Sikonge na Manyoni uliopo Mkoani Singida ambao ulianza wakati wa sensa ya mwaka 2012, ambapo Mamlaka ya Wilaya ya Sikonge ilifanya sensa ya watu kwenye maeneo yasiyo chini ya mamlaka yao. Maeneo hayo ni Vitongoji vya Matagata na Mwanatiga Kata ya Mitundu na Kata ya Mgandu Tarafa ya Itigi, Wilaya ya Manyoni. Maeneo hayo yamekuwa chini ya Wilaya ya Manyoni tangu kupata Uhuru, Awamu ya Kwanza, ya Pili, ya Tatu na ya Nne mpaka mwaka 2012 Sikonge walipokuja na GN yao inayoonyesha kuwa Matagata na Mwamatiga vipo Sikonge. Naiomba Serikali itengue GN hiyo siyo halali. Wananchi wa maeneo hayo kwa miaka yote wamepiga kura upande wa Manyoni na huduma zote wanapata kutoka Halmashauri ya Manyoni.

Naiomba Serikali itekeleze agizo au ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wa Serikali kupeleka Tume au Kamati ya Kuhakiki Mipaka iliyomaliza kazi yake Kiteto iende Manyoni na Sikonge ndani ya wiki tatu ikafanye uhakiki wa eneo hilo la mgogoro. Wananchi wa Mwamatiga na Matagata wanatawaliwa kwa mabavu na mamlaka ya Kata ya Kipili - Sikonge, kinyume cha utaratibu. Naomba majibu juu ya hoja hii na hatua zinazochukuliwa. Waziri na Naibu wake walimwagiza Katibu Mkuu wa AMISEMI atafute fedha za dharura kuiwezesha Tume ikafanye kazi eneo hilo.

(iii) Zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi kwa kutegemea kilimo na wananchi wanahitaji kulima mazao ya chakula na biashara, lakini wamekuwa wakikosa masoko ya mazao yao na hivyo kuwakatisha tamaa katika jitihada zao za kujikwamua kwenye umaskini. Serikali itafute masoko ya uhakika kuwatia moyo wakulima.

(iv) Mwaka huu Ukanda wa Kati haukupata mvua za kutosha (Dodoma na Singida). Aidha, hali isiyotabirika ya tabia nchi imepelekea mvua zisizotabirika pia. Naishauri Serikali ijipange mapema kupeleka chakula maeneo yenye upungufu mkubwa wa chakula ya Wilaya ya Manyoni.

(v) Barabara ya kutoka Mkiwa – Itigi – Rungwa – Makongolosi ni ahadi ya Rais na imewekwa kwenye Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa. Naishauri Serikali ianze ujenzi wa barabara hii muhimu inayopita maeneo yenye uchumi mkubwa.

(vi) Umeme kutoka Mitundu – Kalangali – Kiyombo – Kirumbi hadi Mwamagembe ulipangwa chini ya REA kuwa umeshapelekwa na kukamilika ifikapo Juni 2015, lakini hadi sasa Mradi huo bado haujaanza. Naishauri Serikali ichukue hatua za haraka za kuanza kwa Mradi huu muhimu kwenye maeneo yenye uchumi mkubwa wa mazao ya misitu, wanyamapori, asali na mazao ya tumbaku na chakula.

(vii) Halmashauri zetu zingeweza kufanya vizuri zaidi kama mtiririko wa fedha za maendeleo na matumizi ya kawaida ungekwenda vizuri 2014/15. Naishauri Serikali irekebishe hali hii ili kupeleka fedha kwa wakati kuepuka kusimama kwa ujenzi wa Miradi ya Maendeleo.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo yangu kwa njia ya kuongea, napenda kuchangia hoja hii kwa kuainisha matatizo sugu hasa katika Sekta ya Elimu, Afya na Nyumba za Watumishi wa Magereza.

Mheshimiwa Spika, hali ya shule zetu katika Mkoa wa Mara na hususan Wilaya ya Tarime siyo nzuri. Ili tuweze kuwa na ufaulu mzuri wa wanafunzi ni lazima tuwe na miundombinu ya shule kama majengo ya shule, matundu ya vyoo, nyumba za walimu, ofisi za walimu, maktaba na vitabu.

Mheshimiwa Spika, kuna shule nyingi sana zimefungwa kwa sababu ya tatizo la vyoo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na hata Halmashauri ya Mji wa Tarime. Shule ya Msingi Sirari imefungwa tangu tarehe 28 Machi, 2015 hadi leo wazazi ndiyo wanajichangisha kujenga bila mkono wa Serikali. Nimechangia sementi na nondo.

Tatizo langu ni kwa nini tuwanyime fursa watoto wetu, Serikali imekuwa wapi hata kufikia kufunga choo? Kwenye Halmashauri ya Mji, Shule ya Msingi Kabu ilifungwa na inahudumia shule tatu kwa *shift*. Shule ya Msingi Nkande ilifungwa pia kwa sababu ya choo. Shule ya Msingi Nyamisangura ipo hatarini kufungwa kwa sababu ya choo. Walimu hawana ofisi wanakaa kwenye miti katika Shule ya Sabasaba, Mapinduzi na Azimio ambazo ziko mjini kabisa.

Tatizo lingine linaloathiri ufaulu wa watoto ni juu ya shule tatu kutumia majengo ya shule moja, yaani wanaingia kwa *shift*. Hii inawapunguzia muda wa kusoma maana wanasoma kwa saa tatu tu. Hali hii haikubaliki na ni hatari. Shule hizi ni Sabasaba, Mapinduzi na Azimio, zilizopo Tarime Mjini.

Mheshimiwa Spika, Shule nyingine ni Nyamisangura na Tarime. Shule za msingi zote zipo Tarime Mjini. Kwa nini Serikali isitenge eneo na kujenga shule hizi ili wanafunzi hawa wasome muda wote kama wenzao kwani wanapimwa kwa maswali yale yale wanayopimwa wenzao wanaosoma muda wote? Hii pia ni kero kwa walimu maana inabidi wawe na muda mfupi wa maandalizi kwani nao wanaingia kwa *shift*.

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya shule za msingi ni ya enzi ya sitini na sabini, yamesazeeka hadi yanaanguka na kuwa hatarishi kwa wanafunzi kusoma; hivyo, kupelekea kufungwa na madhara ni kwa wanafunzi wetu.

Kwenye elimu pia nyumba za walimu ni za kusikitisha. Mfano, Shule ya Sekondari Inchungu, nyumba zao zimechoka, mvua ikinyesha wanahamisha vitu, hakuna huduma ya

choo ndani ya uzio wao kuna choo cha walimu ambacho kinatumika kama *staff toilet*, inabidi walimu wajisaidie ndani kwenye kopo ili asubuhi wamwage. Hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kama tuna dhamira ya kweli ya kuinua elimu ya Watanzania ni vyema sasa tuboreshe miundombinu kwa ujumla wake, kinyume na hapo hatutasogea mbele.

Mheshimiwa Spika, afya, kwa maana ya huduma za afya. Kwa hili Serikali bado haijaitimiza Makubaliano ya Abuja ya kutenga asilimia 15 ya bajeti nzima kwa ajili ya afya. Vijiji havina zahanati na vile vichache venye zahanati za zamani havina huduma na vifaa tiba. Hali hii imepelekea hata vifo vingi vya akina mama, maana miundombinu ya barabara ni mibovu, hakuna *ambulance, four-wheel* zinakwama; ni vyema sasa Sera ya Zahanati na Vituo vya Afya ifanywe kwa vitendo na si maandishi.

Mwisho na kwa masikitiko ni miundombinu ya nyumba za Askari Magereza ni ya kuhuzunisha na kwa aibu kabisa hawa Askari wanajijengea vibanda ili kujihifadhi, zile nyumba hazina hadhi ya kuishi binaadamu. Tunaomba Serikali ichukue hatua za kunusuru hali ya hatari ya wale Askari na familia zao. Zipo CD za nyumba zile nitazionesha.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

MWENYEKITI: Sasa namuita Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mchemba.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba na mimi nitumie dakika hizi chache ulizonipa kuchangia hoja hii ya Waziri Mkuu iliyoko Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Taifa letu liendelee ni vyema kila Mtanzania akatambua kwamba ana wajibu wa kutimiza. Kuna wenye wajibu wa kutimiza kwa majukumu ya kutekeleza na kuna weye wajibu wa kutimiza hata kwa kuelewa kile kinachotekelezwa na kuna wenye wajibu wa kutimiza kwa kutambua tu hali halisi ya nchi yetu. Tukitimiza wajibu huo, tutaweza kusonga mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukifuatilia mjadala ulioendelea hapa Bungeni hasahasa wananchi wakifuatilia, kama kuna mwananchi anayefanya uchambuzi vizuri kabisa atakuwa anatushangaa sana viongozi wake kwa maana ya Wabunge wote walioko humu Bungeni pamoja na Serikali, atakuwa anashangaa sana. Nitawaambia baadhi ya maeneo ambayo mwananchi wa kawaida anayefanya uchambuzi lazima ashangae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza, watu wengi wamelalamikia deni la Taifa na hii ni hoja inayoangukia Wizara ya Fedha, kwa hiyo, ndiyo hoja moja wapo nitakayoizungumzia. Watu wengi wamezungumzia au wamelalamikia deni la Taifa na wengine wanakwenda mbali zaidi, wanasema wakati Rais wa Awamu ya Nne akiingia deni lilikuwa kadhaa, wengine wanasema shilingi trilioni 10, wanasema wakati anaondoka limefika shilingi trilioni 30, ni kweli deni limepanda limefika kiwango hicho lakini wanalalamikia viongozi. Je, hivi viongozi hawa waliochaguliwa wawakilishi wa wananchi hivi kweli wametimiza wajibu wa kulitambua, wajibu tu, si wa kufanya kazi, je wametimiza wajibu wa kulitambua tu Taifa lao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ni uamuzi tu, Rais huyu angeweza kuamua hakopi kitu chochote, angeweza kuingia akamua hivyo, hakopi kitu chochote. Je, tumetafakari madhara ya kutokukopa kitu chochote, leo hii Taifa hili kama asingeongeza deni hata senti moja, leo hii Taifa hili lingekuwa kwenye hatua gani? Swali la kujjuliza ni hilo, maana yake uliofanyika ni uamuzi tu, hakuna nchi iliyokuja kutulazimisha kukopa, hakuna nchi imefunga safari

kutulazimisha Tanzania tukope lakini hebu fuatilieni takwimu halafu mniambie. Leo hii kama TRA ingekusanya kwa asilimia 100 kwamba wamefanikiwa kwenye malengo kwa asilimia 100, hiyo ni asilimia 57 ya bajeti ya Taifa letu hili. Kama TRA na Halmashauri wangekusanya maduhuli kwa asilimia 100, hiyo ni asilimia 62 ya bajeti ya Taifa letu. Hizi asilimia zinazosalia, asilimia 8 mpaka 12 ni misaada ambayo inaweza isije au ije, asilimia inayobaki hapa katikati ili utekeleze miradi ya maendeleo ni mikopo. Hivi kweli utakopa bajeti kwa miaka 10 halafu deni libaki palepale, ni hesabu ya wapi hii Watanzania wenzangu, ni hesabu ya wapi? Kwamba matunda ya vitu vinavyotokana na kukopa tunafurahia lakini deni tunalalamika kwa nini limepanda, ni hesabu ya wapi, unaipata nchi gani hesabu ya aina hiyo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na deni la ndani, kweli tumekopa, deni limepanda, tunadaiwa na Mifuko lakini ndiyo tumejenga UDOM, UDOM mnaipenda, deni lake hamlipendi. Tumekopa kwenye Mifuko kujenga ukumbi huu mlioko hapa ndani. Hivi kweli hata ukumbi huu hamjajua kama umejengwa kwa mkopo? Ukumbi huu mnaupenda lakini deni lake hamlipendi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tusingekopa madhara yake ni yapi, hii tafsiri ya kusema ni asilimia 62 ya deni maana yake ni nini? TRA ikikusanya shilingi bilioni 800 kwa wastani kwa mwezi maana yake 450 hapohapo zinakwenda kwenye mishahara, zinabaki 350, 300 mpaka mia tatu na zaidi zinakwenda kwenye deni la Taifa. Hebu niambieni kama tungeikusanya hiyo fedha inayosalia tukasema kila mwezi tukikusanya tutapeleka kwenye mradi, tungejenga miradi ipi, hii leo UDOM ingeshasimama hii? Tungepeleka shilingi mia tano mia tano kila mwezi tukasema tunajenga Chuo Kikuu cha Dodoma, tungeshajenga leo? Sasa watu badala wajjulize fedha zile zimekwanda wapi, mimi naweka Mezani kwako uchukue nakala hii ya miradi yote ya Taifa hili, kuanzia fedha ilikopwa wapi, ilikwenda mradi gani na ilikuwa kiasi gani, hii hapa naweka, wachukue mezani kwako. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitaja michache tu, iko miradi zaidi ya 360, Tumekopa Japan tumekopa barabara ya Iringa - Dodoma, barabara ya kutoka Iringa kuja Dodoma mnaipenda halafu mnataka baada ya kukopa deni libaki vilevile. Tumekopa India kwa ajili ya laini ya umeme Iringa-Shinyanga, mnataka umeme lakini deni libaki palepale. Tumekopa IDA kwa ajili ya maji Zanzibar, tumekopa kwa ajili ya uwanja wa ndege Zanzibar, tumekopa kwa ajili ya elimu, tumekopa kwa ajili ya barabara ya Arusha - Namanga, tumekopa kwa ajili ya maji Singida, tumekopa kwa ajili ya maji Dar es Salaam, tumekopa kwa ajili ya barabara Zanzibar, tumekopa kwa ajili ya maji Zanzibar, tumekopa kwa ajili ya maji Same, tumekopa kwa ajili ya maji Dar es Salaam, tumekopa kwa ajili ya barabara Shelui kwenda Nzega. Nikiwa nachunga Misigiri pale, magari yalikuwa yanakaa zaidi ya siku 30 yako katikati pale leo hii barabara imejengwa inapitika mnataka deni lile libaki vilevile lilivyokuwa mwaka 2005. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, miradi ni mingi, tumekopa kwa ajili ya kilimo, tumekopa kwa ajili ya SONGAS, tumekopa kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Songwe, tumekopa kwa ajili ya extension ya Muhimbili, tumekopa kwa ajili ya barabara ya Marangu - Tarakea, Kemwanga na zingine zaidi ya 360, kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kwamba tumekopa hivyo, uhimilivu wa deni unalipika. Marekani ile pale, deni lake ni zaidi ya asilimia 100 ya pato la Taifa, Japan ni zaidi ya asilimia 100 ya pato la Taifa, la kwetu kwa viashiria vyote bado linalipika. Hivi sasa na hivi tunavyoongea leo hii, shemeji yangu pale Mheshimiwa Mbowe, anasema mnajenga barabara mbilimbili, hivi kwa makusanyo ya kawaida unaweza ukajenga barabara kumikumi, kama nyie mnasema deni hili mpaka hapo lilipo halitakiwi kuendelea, unaweza ukajenga? Leo hii tunahitaji zaidi ya shilingi trilioni 15 kwa ajili reli ya kati, wote hapa mkisimama mnasema reli ya kati ijengwe

halafu kwa wakati uleule unataka deni libaki lilelile, hivi wale wanaotupatia fedha zile ni ndugu zetu kwa namna ipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niliona niwaambie ni vyema tukatimiza wajibu hata wa kulielewa Taifa letu. Watu wengine wanasimama wanasema Serikali hii imechoka, Serikali hii imechoka, mimi nawaambieni, ni kheri aliyechoka kwa kufanya kazi kuliko mvivu wa kufikiri na kutambua yale yaliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni uvivuuvivu tu, kama unapita kwenye barabara halafu hujui fedha yake imetoka wapi, kama Bunge unakaa lililojengwa kwa mkopo halafu hujui fedha yake imetoka wapi na ni kiongozi, kama hujui kwamba kwa utaratibu wa kisasa wa kuendesha uchumi una njia mbili tu za kutekeleza miradi mikubwa, ni ama ukope ama upeleke kwa ubia ama umuachie *private sector* mia kwa mia. Huwezi ukaenda kwenye Taifa kubwa kama hili ukasema bajeti ileile ya Serikali utakuwa unakusanya kidogo halafu unapeleka kuweka mradi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mara kwa mara huwa nikiona kwamba kuna watu wanalalamika na wanasema kwamba kuna uchaguzi na watashinda na hawajui Taifa hili likoje, linaendaje, linaendeshwaje huwa naona mechi hiyo ni rahisi sana. Hakuna uchaguzi ninaousubiri kwa hamu kama huu wa Oktoba kwa sababu tutaheshimiana baada ya huo uchaguzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mechi gani iko hapa, watu hawatambui lolote. Ukiwa na uwezo wa kukosoa na kutukana ni jambo rahisi sana lakini tutakapokwenda kuwaambia wananchi tunataka tuwafanyie nini, nawaambieni na naweza nikaapa kikwetu *Chunumau*, hata saa nne haitafika utasikia '*Iyena Iyena CCM Nambari One*', hamna mechi hapa. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mechi itoke wapi kwa sababu tunayoyaelezea, leo hii ukiwaambia wananchi wa Manyara kwamba hakuna kilichofanyika ukawalalamikia kuhusu deni la Taifa wakati barabara ya kutoka Singida kwenda Minjingu imejengwa kwa mkopo, wanajua hilo. Sasa kwa nini hayo tusiyatambue? Saa nne tu na hivi tulivyojipanga, pembeni kushoto atakaa Nape, kulia tutamweka Kibajaji, *center-half* Abdulrahman Kinana, namba tisa nitakaa mimi mwenyewe. *(Makofi/Vigelegele)*

MBUNGE FULANI: Waambie.

MBUNGE FULANI: Arumeru mlikimbia.

MBUNGE FULANI: Arumeru ilikuwaje?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. MCHEMBA): Bwana wewe, Barcelona ikicheza na *UKAWA United* hata refa awe shemeji yangu Mbowe Barcelona itashinda tu, CCM ni kama Barcelona. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulisemea hili la mikopo, jambo lingine tumeongelea pia hii habari ya OC, mimi niwaambieni, kuna Kamati ya Bajeti na Wabunge wake wanafanya kazi nzuri sana na wala siyo wa CCM peke yake, Mheshimiwa Selasini yuko mle, Mheshimiwa Hamad Rashid yuko mle na wengine, tulienda tukakaa mwaka wa jana, mimi mwenyewe nilisema haya matumizi mengineyo tukate kwa asilimia kumi, wakakaa Mwenyekiti wake akiwa Chenge, hivi mnajua kilichofuatia? Kwenye hizo tunazosema OC tulipokata kwa asilimia tulikuta

tumekata na MSD, tulikuta tumekata na mitihani, tulikuta tumekata na mitaji ya TIB, tulikuta tumekata na michango ya Jumuiya ya nje ya nchi ambako nchi yetu ni mwanachama. Kwa hiyo utatambua kwamba... (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa wewe hujibu hoja, unachangia na unachangia hapo hapo ulipo na Mheshimiwa Chiza amekupa dakika zake tano. Mheshimiwa Majaliwa zungumza na Kiti, changia ukiwa hapo hapo kwa dakika 15.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya mwisho nikiwa natenda tendo la kuanza kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara yangu na kwa kweli sitaweza kuvumilia kumshukuru Mheshimiwa Rais ambaye aliniamini kufanya kazi hii kwa kipindi chote cha miaka mitano kufikia leo hii. Pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye pia nimefanya kazi naye kwa muda mrefu na amenipa mwongozo mzuri wa uongozi, naamini sasa naweza kuendelea na kazi hii popote pale ambapo nitaweza kupata fursa hii. Bila kumsahau Mheshimiwa Waziri wa Nchi ambaye tumekuwa tukifanya naye kazi kwa karibu kabisa na kaka yangu Mheshimiwa Mwanri. Sitaweza kuwasahau kabisa wana Ruangwa ambao wametumia muda mwingi kunivumilia huku tukifanya shughuli za maendeleo na wanajua kazi kubwa tuliyoifanya kuleta maendeleo Wilaya ya Ruangwa kwa kauli mbiu yetu Ruangwa kwa maendeleo inawezekana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mjadala wetu wa bajeti hii kwenye sekta ya elimu kulikuwa na michango mingi iliyotoka kwa Waheshimiwa Wabunge na maeneo mengi yalikuwa yanahitaji ufafanuzi na mimi nimefanya *summary* kwa muda huu niliopewa kuona namna sahihi ya kuweza kufafanua zile hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wametaka kujua. Moja ni eneo la madeni ya watumishi ambao ni Walimu na wasiokuwa Walimu ndani ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kimsingi, ofisi yetu tumeendelea kuratibu na kupata mafanikio makubwa ya kupunguza kiasi kikubwa cha madeni ambayo yanajitokeza sana kwa watumishi wetu ambao ni Walimu na wale ambao siyo Walimu. Tumeshafanya uhakiki wa jumla kuondoa utata katika ulipaji wa madeni haya na uhakiki huu sasa unafanywa na CAG. Kwa mara ya mwisho tulipofanya uhakiki tulipata deni la shilingi bilioni 24.2 ambazo pia baada ya kufanya uhakiki huo tulibaini madai halali ni shilingi bilioni 18 ambapo tumeshaanza kulipa jumla ya shilingi bilioni 11. Kwa hiyo, kiasi kilichosalia tutaendelea kukilipa na tuna uhakika kwamba sasa tunataka tulipe madeni yote ya watumishi ili waweze kufanya kazi yao vizuri zaidi. Hii nilikuwa nazungumzia kwa watumishi ambao siyo Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa Walimu tulifanya uhakiki wa jumla na tulipata jumla ya madeni ya shilingi bilioni 53 ambayo yalikusanywa lakini baada ya CAG kuyapitia tumegundua kwamba madeni haya kwa kuwa yanalipwa kwa awamu, mpaka sasa tumeshalipa shilingi bilioni 25 kwa yale ambayo tumeweza kuhakiki na tumegundua kwamba yanaweza kulipwa sasa. Kuna madeni ambayo yanasubiri kuhakikiwa ya Walimu 7,169 lakini ambayo tayari yamehakikiwa ni ya shilingi bilioni 3.4 ambazo kwa mujibu wa taarifa za Hazina kufikia tarehe 30 Juni, tutakuwa tumeshalipa madeni haya na madeni haya yote yanalipwa kutoka Hazina na yanaingia kwenye akaunti za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ambao tumeuweka kwa kutambua Walimu ambao wamelipwa ni kwa Halmashauri kufanya mapitio kwenye *Pay Roll* ili kugundua ni Walimu

wangapi ambao wamelipwa na ambao hawajalipwa. Kazi ya kulipa madeni haya inaendelea vizuri, naomba Walimu waendeleo kutuamini kwamba kazi hii ya ulipaji tunaendelea nayo na tunaweza pia tukafikia hatua nzuri huku tukiwa tumeweka utaratibu wa kuzuia kuwa na madeni wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ya kuzuia madeni ni nzuri kwa sasa na madeni haya ukiondoa ya mishahara, tunayo madeni ambayo si ya mishahara, yale ambayo yamezungumzwa na dada yangu Mheshimiwa Mtinda yanayogusa eneo la uhamisho wa ndani, likizo kwa watumishi, wale wote wanaopata nafasi ya kusoma na matibabu, haya yanalipwa kupitia OC ya Halmashauri. Kwa hiyo, kila Halmashauri inaratibu vizuri watumishi wake wote, wanatambua nani wanamruhusu, nani wanamhamisha na tumeshatoa maelekezo ya msingi ya namna ya kudhibiti maeneo haya na kazi hii inaendelea kwa kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu alitaka ajue leo hii kwamba kule Mkalama madeni yanakwendaje. Kwa kuwa ameliuliza tukiwa tunakaribia kujibu hapa, naomba tu dada yangu wakati wote naweza nikakupa taarifa za mwenendo wa madeni yale ya Wilaya ya Mkalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Waheshimiwa Wabunge wengine ambao waliweza kuchangia eneo hili Mheshimiwa Meshack Opolukwa, Mheshimiwa Mwidau na Mheshimiwa Jafu juu ya mfumo mzima wa ulipaji wa madeni ya watumishi. Kwa hiyo, taarifa ambayo nimeitoa kwa kifupi bado inaonesha kwamba Serikali inaendelea na ulipaji wa madeni na tuna uhakika kwamba kazi hii tutaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la madeni liliguswa pia lile la wazabuni wa shuleni. Hili nimelieleza vizuri nilipokuwa najibu jibu kwenye swali la msingi asubuhi namna ambavyo tunaendelea kutekeleza ulipaji wa madeni haya ya wazabuni wetu kwenye shule. Kimsingi, kule liko tatizo la upungufu wa fedha ambazo tunawapeleka lakini ulipaji unafanywa na fedha ambayo tunalipa inatoshwa kabisa kulisha wanafunzi wetu kule shuleni na kila mwezi tunapeleka fedha. Takwimu ambazo nilizisoma asubuhi zote zinaonesha kuanzia mwaka wa fedha ambao tunaumaliza, Julai 2014 kila mwezi tunapeleka fedha shilingi bilioni 3.5 ambazo kwa hesabu ya idadi ya wanafunzi waliopo na shule tulizonazo inatoshwa kabisa kuwalisha watoto hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkanganyiko uliojitokeza ni pale ambapo wanafunzi walikuwa wanakwenda likizo na wakuu wa shule walikuwa wanawaambia msirudi mpaka mpate taarifa kutokana na upungufu wa chakula ambacho kipo lakini siyo kwamba kuna shule ambayo ilikosa chakula kabisa. Hata kule Kagera ambako shule ilifungwa kulikuwa na chakula cha kuweza kuwatosha kwa siku nne, ni vile tu hakufanya mawasiliano na Mkurugenzi wake ili aweze kupata namna sahihi ya ulipaji. Mwezi uleule tulikuwa tumeshatuma shilingi bilioni 8, fedha nyingi zaidi kuliko ambayo tunaituma kila mwezi, kwa hiyo hakukuwa na tatizo la fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba eneo hili hatuna shida nalo, tunatambua tuna watoto na ni binadamu wanahitaji kula na wanahitaji kuishi ili wasome na tunalizingatia hivyo. Nataka niombe pia wazabuni wawe na amani kwenye eneo hili, tunatambua madeni yao lakini tunatambua kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa huduma, naomba waendeleo kutoa huduma Serikali italipa madeni yake yote ya wazabuni kwa sababu tunatambua eneo hili. Kwenye eneo la madeni ni kama ambavyo nimeeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mheshimiwa Silinde alipokuwa anatoa mchango wake alitaka kujua mamlaka huru ya kusimamia elimu ambayo pia imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengine. Jambo hili linaendelea kuratibiwa na Serikali kupitia Wizara ya Elimu na kwa sasa Serikali inaendelea na utaratibu wa kuunda chombo hicho cha kudhibiti

ubora wa elimu na chombo ambacho alikuwa anakitaka yeye ni kile cha udhibiti wa elimu pamoja na kile chombo kimoja kinachoweza kuwahudumia Walimu. Taratibu zote zimekamilika na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi) atakapopata nafasi atakuja kueleza vizuri zaidi kwa sababu yeye ndiye analitekeleza kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo hili la ajira mpya za Walimu. Waheshimiwa Wabunge wengi akiwemo Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, Mheshimiwa Assumpter Mshama walitaka kujua tuna mpango gani wa kuongeza Walimu kwenye Halmashauri za Wilaya. Nataka nitoe taarifa kwamba ajira mpya tumeitangaza ya jumla ya Walimu 36,056 wa kurugenzi zote mbili sekondari na msingi na tulishatoa tangazo la awali, Walimu walishatoka majumbani kwao kwenda kuripoti na *deadline* ilikuwa ni tarehe 9. Taarifa tulizonazo zaidi ya asilimia themanini walisharipoti lakini tuna kundi kubwa ambalo halijaripoti bado. Kuna marekebisho tunataka tufanye kwa sababu wako vijana ambao hawakupata nafasi ya kuajiriwa, wale ambao walikuwa na *supplementary* na sasa wame-clear lakini hatukupata orodha yao kutoka kwenye vyuo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipobaini hili tulilazimika tusitisha kwenda kuripoti mpaka tarehe 9, ili pia tuwapeleke na hawa kwenye Wilaya ambazo tulikuwa hatujapeleka Walimu ili tuweke mgawo sawia. Baada ya muda mfupi kuanzia kesho tutatoa tena kwenye *website* ili sasa wale wote ambao hawajaenda waweze kwenda kwenye vituo vyao. Kwa wale Walimu wote ambao wamepangwa kwenda kuripoti ambao wamefika kwenye vituo wameambiwa wasubiri na tulitoa *press* kwamba wasubiri tangazo jipya litatoka. Tunazo taarifa kwamba kuna watu wameanza kupotosha kuwaambia kwamba ajira imefutwa, ajira ipo, orodha yao ipo, tunachokifanya tunaongeza ambao hawakuingia kwenye ajira na tukishatoa kwenye *website* wote watakwenda kuripoti kwenye vituo vyao na tutawapa muda kama ni wiki moja basi tunatarajia ndani ya wiki moja hiyo kila mmoja atakuwa ameripoti kwenye kituo chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge alitaka kujua kwa nini Walimu walioripoti kule hawajalipwa posho. Kimsingi hatuwezi kuwapeleka Walimu kule kabla ya kuwalipa. Hawa ambao wanalalamika ni wale ambao hawakusikia tangazo la kusitisha kwenda na sasa wamekwenda kwenye kituo tukiwa tumeshasitisha na utaratibu wa sasa ulipaji unatumia mtandao, tarehe 9 tulizima mtandao wa malipo, kwa hiyo wale ambao wameripoti taratibu zao zinaendelea, hawa ambao wamekwenda kwenye vituo kwa kutosikia tangazao ndio wale ambao wanatupigia simu. Tunaendelea kuwajibu vizuri kwamba wawe watulivu, tutakapotoa taarifa hii ya kwenda kuripoti wataanza kulipwa malipo yao kwenye vituo vyao, ile ya siku saba kama posho yao na nauli yao kutoka nyumbani mpaka kwenye kituo kipya. Kwa hiyo, taratibu hizi zinaendelea vizuri na tunaamini kila mmoja atapata huduma hii mahali hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge pia waliomba kujua suala la ujenzi wa miundombinu kwenye shule zetu. Tunaendelea vizuri kwenye miundombinu kwa kurugenzi ya msingi na sekondari. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba suala la uboreshaji wa miundombinu kwenye sekta ya elimu ni suala shirikishi. Tuna ubia kati ya Serikali, wananchi na wadau katika kuboresha miundombinu lakini Serikali tuna nafasi kubwa zaidi ya kuboresha miundombinu kwa shule za msingi na sekondari, kazi hii inaendelea kwa pamoja. Kwa hiyo, tumeendelea kuongeza vyumba vya madarasa lakini sasa tunaendelea na ujenzi wa maabara ambao pia tunaufanya kwa ubia, ingawa jambo hili limeingia lugha tofauti kwa sababu wako watu ambao wanasema kuna wananchi wanachangishwa kwa nguvu, hapana!

Mheshimiwa Rais alipotaka miundombinu hii iwepo kila kwenye shule, ni jukumu la kila Halmashauri kutafuta vyanzo vyao ili waweze kujenga maabara kwa vyumba vitatu ili kuweza kuanza kufundisha masomo ya sayansi. Serikali haijasema ichangishe wananchi kwa nguvu, kama Halmashauri husika walitaka kuchangisha ilitakiwa kwenda kuwaelimisha wananchi,

kuwaambia faida ya jambo hilo na tunaamini wananchi wetu wanajua faida ya uwepo wa miundombinu shuleni ili waweze kuchangia mchango ambao wenyewe wananchi wataamua, kwa hiyo, suala la miundombinu linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilijitokeza jambo la ujenzi wa choo kule Tarime. Mimi nasema choo kama choo ni *issue* tu inayofanywa na kijiji pale pale kijijini tena kwa shule ya msingi, kwa sababu shule hizi ni shule za vijiji. Kila kijiji kina shule ya msingi na kuna Kamati ya shule iliyoundwa na wanakijiji wenyewe, kwa hiyo ni juu yao kuona umuhimu. Wanapoona jambo hili limewazidi nguvu wanakwenda kwa Diwani, Diwani ataingiza kwenye *Council*. Pia hata Wabunge na sisi ni Wajumbe wa kwenye *Council* zetu, ni jukumu letu kutenga fedha ili kuhakikisha kwamba kila shule inakuwa na choo. Sasa kama kunakuwa na utaratibu wa jumla ambao sisi Wizara tunaweza kuwatumia fedha basi tunaweza tukachangia kwa utaratibu ule ambao sisi tumeona unafaa katika kuimarisha miundombinu ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitakiwa hapa kueleza tatizo lililojitokeza kule Meatu kwamba kuna Mwalimu anaumwa lakini pia Afisa Elimu kampa mke wake shughuli fulani. Jambo hili halina ukweli baada ya kuwa tumefanya ufuatiliaji. Ni kweli tuna Mwalimu anaumwa lakini taratibu zake zinaendelea kwa mujibu wa *recommendations* za Madaktari na matibabu yanaendelea lakini pia mgonjwa huyu itakapoonekana ugonjwa huu unaendelea tutamuundia Tume, jopo la Madaktari afanyiwe uchunguzi tuweze kubaini kama anaweza kuwa mtumishi au vinginevyo ili sasa tumtendee haki aweze kupata matibabu yake vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya Walimu kama nilivyoeleza, mgawanyo wa madeni ambayo yanalipwa na Serikali Kuu pamoja na Halmashauri. Kwa hiyo Halmashauri imetupa taarifa kwamba itashughulikia madeni yote ya ndani ili tuweze kuondoa mgongano uliopo kati ya Walimu na Halmashauri yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mangungu aliomba muda wa kuripoti Walimu wapya uongozwe, kama ambavyo nimetoa maelezo, tutawaongezea muda ili pia waweze kujiandaa na kusafiri vizuri ili wafike mahali ambako wametakiwa kuripoti. Kama ambavyo nimeeleza, naamini kila mmoja ataweza kufika kwenye kituo chake. Tunasisitiza sana kufika kwa muda kwa sababu pia tusingependa kuwe na utofauti wa upataji wa mishahara yao. Zile tarehe ambazo tunazitamka zinawasaidia wao kupata mishahara kwa pamoja. Kama nilivyosema tumejidhatiti kudhibiti madeni, kwa hiyo, ukichelewa muda ambao sisi tumekupangia maana yake utakosa mishahara wa mwezi ule na utanza kulalamika kwamba Serikali haijakulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo tumeendelea kuyasemea hapa ni yale ambayo ambayo yalizungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wote, kila mmoja alitumia lugha tofauti lakini akizungumzia jambo hilo hilo ambalo nimeweze kulieleza. Niseme kwamba Serikali inaendelea kuimarisha sekta ya elimu na kweli tunaendelea kuwashukuru Walimu kwa sababu tunaanza kuona matokeo mazuri. Wale wote wanaofikiri kwamba sasa sekta hii Walimu ambao tunawapanga hawana taaluma, Walimu wetu sasa wana taaluma ya kutosha kuweza kutoa elimu kwa kurugenzi ya msingi lakini pia kwa kurugenzi ya sekondari. Kama ambavyo Wizara ya Elimu imefanya mabadiliko ya Walimu wanaotakiwa na sifa za kwenda shule za msingi, sasa hivi shule za msingi hatuna *grade A* tena sifa ya mwisho ni diploma.

*(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwanri dakika 15.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba kabla sijaingia speed nitamke waziwazi kwamba mimi naunga mkono hoja hii. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu sana kwamba kwa kipindi chote cha miaka mitano nimefanya kazi na Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimefanya kazi na Mheshimiwa Hawa Ghasia, nimefanya kazi na Ndugu yangu Kassim Majaliwa na Katibu Mkuu pamoja na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na wale wengine wote ambao tumefanya nao kazi, napenda kuwashukuru sana na kuwaambia ahsante kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa. Nashukuru sana kufanya kazi chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nashukuru kwa maongozi yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee nimshukuru mke na watoto wangu. Najua mke wangu Grace ananiombea sana, namwambia ahsante sana. Nawashukuru pia na wale wengine wote ambao wananiombea. Nawashukuru wananchi wa Wilaya ya Siha na Jimbo langu la uchaguzi la Siha ambao wameniamini sana na ambao nina hakika kwamba imani yao bado iko juu, mimi nitakuja nyumbani tutaendelea na jambo hili wala wasiwe na wasiwasi. Wote hao nawashukuru na ninawaambia ahsante sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo linalozungumzwa hapa ni jambo ambalo linatupa taabu kidogo, labda niseme kwamba kabla sijajibu, kama hoja ingekuwa ikasema tazama bwana, sisi tumeona mmefanya hiki na kile lakini sisi tungekuwa ni ninyi tungefanya hivi, ningeelewa. Mimi nilifika mahali nikaishiwa nguvu nikisikia nikiambiwa hamna kitu hapa! *Problem* unayoipata ni *handling* yake kwa sababu ukiiweka hivyo unavyotaka kuiweka wananchi watapata taabu sana kupambanua, kuna wakati watafika mahali hawatajua wanaambiwa nini kwa sababu watakwenda Malagarasi watakuta daraja la Jakaya Mrisho Kikwete watapita juu yake halafu watasema hao wanaosema hakuna kitu hapa, hii ni nini? Wananchi wanaokwenda Mtwara watapita katika daraja la Benjamin William Mkapa na mnasema hakuna kitu hapa, wananchi watafika mahali watashindwa kupambanua. Watakuwa na watoto wao wataingia madarasani, watasoma *form I-IV* na *form V-VI*, watakwenda Chuo Kikuu UDOM, wakifika UDOM watajiuliza mbona tunaambiwa hamna kitu hapa? Watakwenda vijijini wataanza kusafiri kutoka Bukoba pale Muleba watakwenda mpaka Dar es Salaam, Dodoma na Mtwara kwa siku moja na wanajua ilikuwa inawachukua wiki moja hadi mbili hawafiki, watajiuliza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Max aliwahi kusema maneno yafuatayo, *the masses of the people are as accurate as a thermometer*. Naomba nitafsiri, umma ni sahihi kama kipimajoto. Utaupeleka hivi lakini utarudi wenyewe utakwambia ni hapa, unakwenda kama *pendulum*, utaupeleka hivi utarudi utakwambia ni hapa. Ndipo anapoingia mtu anaitwa Mao Tse-tung, namalizia, alisema asiyekutakia mema akishangilia jambo lako akakwambia safi sana hivyo unavyofanya Mama Hawa Ghasia, jambo hilo liache mara moja halifai. Akasema, ukimsikia asiyekutakia mema anasema hawa wachovu, hamna kitu pale, hamna lolote au wamelegea, songa mbele Mheshimiwa Waziri Mkuu unapatia, songa mbele Mama Hawa Ghasia, songa mbele Serikali kwani unapatia. *Opposition* haiwezi ikaja hapa ikashangalia ikasema sawasawa kabisa mmjenga shule, kazi yao siyo hiyo, hawawezi kushangilia. Sisi kazi yetu ni kusimama na kufanya kazi na ndiyo nataka niseme kwamba sisi tunasonga mbele, kazi tumefanya hiyo tuliyoifanya. Nawashukuru Wabunge wengi waliosimama hapa wametoa ushuhuda kwamba kuna kazi kubwa imefanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lililozungumzwa la kwanza Mheshimiwa Ole-Sendeka, alizungumza habari ya Orkesmet na akaeleza tatizo la maji lililopo pale na Orkesmet kuna tatizo limeingia pale la ukame, hawana maji kabisa. Nataka nimsomee, Serikali inatambua changamoto ya huduma ya maji katika mji wa Orkesmet na maeneo yanayozunguka mji huo.

Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali kupitia Wizara ya Maji imefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi. Kazi hii imekamiliwa pamoja na mapitio yake, *review of detail design* kupitia mpango wa uboreshaji wa huduma ya maji kwenye miji midogo hapa nchini. Kwa sasa taarifa ya kina ya usanifu imewasilishwa kwa wahisani wa BADEA kwa ajili ya kupata kibali na kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wa kitaifa wamekwenda pale na Mheshimiwa Sendeka amezungumza hapa, wametoa matamshi nataka nisema hapa baada ya kazi yote iliyofanyika hapa, ukingoja mpaka waende wakamalize kazi hii, kazi haitakwisha. Mwaka juzi walipangiwa fedha hazikwenda, mwaka jana walipangiwa fedha hazikwenda na safari hii tume-consult Mheshimiwa Waziri na nataka nimwambie Mheshimiwa Ole-Sendeka, Serikali imekubali na ameagiza Hazina watatafuta shilingi bilioni moja zitapelekwa kwa ajili ya kuchimba visima vya maji kwa sababu hawana maji kabisa watakufa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, imezungumzwa habari ya ugatuaji wa madaraka na amezungumza Mheshimiwa Kigwangwalla, *D by D*, kuna watu wengine wamesema rudisheni madaraka kwenye Wizara zenyewe, rudisheni madaraka TAMISEMI. Naomba nieleze, *D by D* maana yake ni nini? *D by D* maana yake ni kwamba huko nyuma maamuzi yote ulikuwa unayafanya Dodoma na Dar es Salaam lakini leo unayapeleka madaraka Hai, Siha, Mtwara, Newala na kadhalika, maana yake unawapa wananchi madaraka na mamlaka ya kufanya maamuzi. Unachofanya ni nini? Unasema hamisha nguvukazi, mtaji na rasilimali wapeleke wananchi mahali walipo, mawazo yametolewa hapa turudi nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ibara ya 145 na 146 inatambua mamlaka hizi ambazo tumezianzisha na tuliwahi kufika mahali tukasema vyovyote vile tunavyokwenda, kitendo chochote kinachowapa wananchi wa Kinondoni na Ilala mamlaka na madaraka kusema kwamba hivi ndivyo tunavyotaka, jambo hilo ni lazima liungwe mkono. Kwa hiyo, sisi tumeleza kwa kifupi hapa tukasema kwamba bado tunafikiri kwamba kazi kubwa ambayo tutafanya ni kuboresha mpango mzima wa kupeleka madaraka kwa wananchi walipo. Bado tunaendelea kuzungumza na wenzetu, Wizara mbalimbali zinatakiwa sasa zianze kuboresha na kuhakikisha kwamba zinawapa uwezo Halmashauri zetu kama ni watumishi waliopo wa Mifugo na Mabwana Shamba tuwasaidie ili waweze kufanya kazi kule na maamuzi yafanywe kulekule kwenye Halmashauri walipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, imezungumzwa habari ya mapato, mapato tumeimarisha, wanaotoka Temeke, Ilala na Kinondoni watanielewa na wanaotoka pia Mwanza na Arusha kidogokidogo wataanza kuelewa. Pale tumeweka utaratibu wa kielektroniki ambapo sasa utakuwa una-charge nje ya utaratibu huo ambao tumekuwa tunautumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajapan wamekuja wakatuelimisha, wakatuambia kwamba chanzo cha mapato kikubwa cha Halmashauri ni kitu kinachoitwa *Property Tax*, wanasema nchi yao ya Japan jeuri yao yote inatoka hapo. Tumeanzisha mpango huo, ukienda Temeke sasa hivi mapato yao yamepanda, ukienda Ilala pale kwako yamepanda na Kinondoni na maeneo haya mengine ambayo nimeyataja hapa. Utaratibu huu sasa tunataka tuu-rollover kwa nchi nzima kuhakikisha kwamba tunafanya hivyo ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lililosemwa hapa kama unasema Halmashauri zifanye ni lazima pia ueleze kwamba zitafanyafanyaje? Max aliwahi kusema, *always the economic base determines the super structure*, yanayosemwa hapa juu hapa chini patakataa. Halmashauri zetu zinapokea ruzuku ya Serikali, 95% inayotoka Serikalini, nyingi tu ukiacha hizi nilizozitaja hapa, 5% tu ndiyo una *generate*, kwa hiyo, *pump* ya kusukuma mambo haimo ndani. Nchi kama nchi sisi hapa tulipo 40% kutoka nje, *Local Government Capital Development Grant*

kutoka nje na 60% ndiyo una-*generate* kutoka hapa. Mimi nashukuru hapa ndani tumeanza kuzungumza *concept* ya kujitegemea, haya ndiyo mambo ambayo tunakusudia kuyafanya katika Halmashauri kwa maana ya kuja na *reforms* katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chacha Nyangwine na wenzake wamezungumzia hilo jambo ambalo nimelizingumzia lakini pia imezungumzwa habari ya O & OD. Wabunge wengi wamesema kwamba wananchi hawashirikishwi labda nieleze kwa kifupi tunafanyaje. Tunapokuja kwenye bajeti Vijiji na Vitongoji vyetu vinakaa, wanapitisha miradi ile ambayo wanafikiri kwao wao wanaona kwamba hawawezi kuendelea kama hawatakuwa na hiyo miradi. Kinachofanyika ni kwamba wanapeleka mapendekezo katika Halmashauri zao za Kijiji wanapitisha katika Mkutano wao Mkuu na Mwenyekiti wa Kijiji anakwenda kwenye *Ward Development Committee* na katika *Ward Development Committee* atasema kwamba hii miradi ndiyo miradi ambayo sisi tunafikiri kwamba kwetu sisi itatusaidia. Wakitoka hapo Diwani ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata anapeleka katika Halmashauri na kwenda *ku-table* sasa na kule watakachoangalia ni kipaumbele lakini pia na uwezo wao wa kuendesha shughuli zile, wakifika mahali wanamaliza, ndiyo inaingia sasa katika utaratibu watapitisha kwenye bajeti, mnafahamu, wakimaliza watakwenda Mkoani watapitisha katika *Regional Consultative Committee* na itakuja mpaka hapa Waziri mwenye dhamana atakuja *kui-table* hapa. Sasa tumeambiwa kwamba ninyi mkishaomba fedha, mkishapata hamfanyi kazi tena ya kwenda kuwaambia wananchi nini kilichopatikana na mambo ya mapato na matumizi yote yamezungumzwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zetu za kifedha zinaboreshwa kwa sasa hivi, hizi nilizoieleza na kwa utaratibu wetu. Kwa hiyo, tuna hakika kabisa kwamba kuanzia sasa Halmashauri zetu, wananchi ni haki yao wadai habari ya mapato na matumizi pale walipo, ni haki yao! Wakikataa kupeleka pale ni lazima wawajibishwe na Mtendaji aliyepo katika Halmashauri wale waliopo chini ya Watendaji wanawajibika kwake. Kwa hiyo, wananchi wanatakiwa waende waseme tunataka tupate taarifa ya mapato ya matumizi kila baada ya miezi mitatu. Sawa, najua kuna wengine ambao hawafanyi hivyo lakini mimi naeleza utaratibu ambao tunautumia hapa na Waheshimiwa Wabunge tunaomba mtusaidie katika hilo eneo ili kuhakikisha kwamba hayo yanatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa sababu najua muda unakwenda, najua mengi atazungumza Mama Hawa Ghasia atakapokuja kuelekezea lakini nizungumzie mwisho suala la usimamizi na kuzingatia mwongozo lakini kuna moja ambalo amezungumza Mheshimiwa Selasini, habari ya ofisi ambazo ni za Chama cha Mapinduzi na wengine wanasema ni za vijiji. Tumetafuta katika *documents* zetu tumegundua kwamba hili jambo limekwenda Mahakamani. Kwa hiyo, tumezungumza na hata asubuhi amekuja hapa ameniuliza, tsubiri tusikie Mahakama wanasema nini kuhusu jambo hili kwa sababu lili-*involve* mambo mengi, watu walipigana na kuumizana na kadhalika. Kwa hiyo, nasema hayo kwa kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nichukue tena nafasi hii kuwashukuru wale wote na kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais, Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana, sauti hii ni msisitizo tu, nashukuru kwa heshima kubwa ambayo nimeipata na kwa jinsi tulivyoshirikiana. Mungu awabariki sana na ahsanteni. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Chiza dakika 20, wewe unajibu hoja njoo mbele.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kujibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa. Naomba pia nimshukuru kipekee Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye msimamizi wangu mkuu kwa jinsi

anavyoniongoza na kunishauri na kunielekeza, kwa hakika huyu ni kiongozi shupavu ana kila sifa za uongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru pia wapiga kura wangu wa Jimbo la Buyungu wanaoendelea kunivumilia kila wakati napokuwa katika majukumu haya nikiwa nje ya Jimbo. Nasema endeleeni, tupo pamoja, msisikilize porojo hizi za ndugu zangu akina Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Mkosamali. Mheshimiwa Mkosamali yeye amekosa vyote kwani amekosa mali na Jimbo ameshakosa. Kwa hiyo, naomba muendeleo kumpuza tu maana wenzetu wakisema wanasahau na mimi siku zote nawakumbusha, sisi Waha tunasema hivi, ukiwa mwongo usiwe msahaulifu na ukijifunza kupigana ujifunze na kukimbia kuna kupigwa vilevile na siku ya kupigwa ni tarehe 25 Oktoba siyo mbali sana. Maana ukiwa unasemasema maneno mengi lazima uwe na majibu yake. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si nia yangu leo kuwapiga vijembe, nawakumbusha tu maana hapa mnasema mengi, Mheshimiwa Mbowe sasa hivi ametoa ushauri mzuri kweli kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali, mimi nashauri ni ushauri mzuri wa kuwa na *city master plan*, *flood control drainage*, ni jambo zuri. Hata hivyo, unasahau wakati huohuo unashauri sisi tukiwaambia wananchi tokeni mabondeni mnakwenda kuwaambia kaeni msitoke hapa, msihame hapa, Serikali inawasumbua, mafuriko yakija tena mnasema Serikali inashindwa kuwasaidia, jamani ukiwa mwongo usiwe msahaulifu.

WABUNGE FULANI: Aaaaah!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI): Kwa hiyo, tunaposhauri jamani tuwe pia tunatoa na *solution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uvumilie wala usiombe mwongozo, tunakumbushana tu, ndiyo maana nimeanza kwa kusema nimekubali ushauri wako wa *city master plan*, ni mambo mazuri lakini kumbuka na wewe unayoyazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa michango yote mizuri na hasa iliyojikita katika kuishauri Serikali hususani kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge walio wengi na hasa wale wa CCM kwa kweli wote wametoa michango mizuri ya kuishauri Serikali. Wapo wachache kama wawili hivi mimi niliwasikiliza ambao wameisaidia Serikali lakini pale waliposhukuriwa wakafikiri wamepata adhabu wakataka mwongozo lakini nawashukuru kwa sababu waliishukuru Serikali na kuishauri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaweza kujibu hoja zote kwa sababu nina hakika ni nyingi mno lakini kama ada, hoja nyingi tutazijibu kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge watapata majibu kama ilivyo ada. Naomba nianze kwa kujibu hoja au maelekezo tuliyokuwa tumepewa na Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara inayoongozwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina. Kamati ilikuwa na hoja kwamba Serikali lazima ifuatilie utekelezaji wa miradi ya uwekezaji mahiri ikiwemo ujenzi wa daraja la Kigamboni, ujenzi wa nyumba za gharama nafuu zilizopo Mtoni Kijichi na mradi mahiri wa ujenzi wa nyumba za kisasa za *Dege Eco Village* kwa lengo la kuweka msukumo ili kuharakisha utekelezaji wake. Naomba kusema tulifanya ufuatiliaji na mimi mwenyewe nilikwenda ziara ile na tuligundua uwepo wa ukuta unaozuia ujenzi wa barabara ambayo ni sehemu ya mradi mkubwa wa Daraja la Kigamboni, daraja ambalo ni katika mambo ambayo tuliyaaahidi na yanaendelea kutekelezwa. Pia tuligundua kwamba kuna upungufu wa miundombinu ya barabara, maji na umeme katika eneo la ujenzi wa nyumba za kisasa huko *Dege Eco Village*. Tatizo kubwa ni kwamba kutokuwepo miundombinu hii kunasababisha gharama za nyumba kuwa kubwa na kama tutamlazimisha mwekezaji kuiweka miundombinu hii maana yake ni kwamba gharama za nyumba naye lazima aziweke pale na atakapomuuzia mtu, maana nyumba zile zinajengwa kwa ajili ya kuuzwa, zitakuwa ghali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho ni nini ambao sisi Serikali tumeona? Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imefanya uthamini yaani *valuation* ya mali na mashamba katika eneo husika na kuainisha fidia inayopaswa kulipwa. Taarifa ya uthamini tayari imekamilika na imewasilishwa Wizara ya Ujenzi ambayo ndiyo ina makubaliano na NSSF, hapa nazungumzia ujenzi wa daraja na ule ukuta ambao ndiyo ulikuwa umezuia ujenzi kuendelea. Wizara ya Ujenzi yenye makubaliano na NSSF ambayo ndiyo mwendelezaji wa mradi huo, ipo katika hatua za kukamilisha taratibu za kulipa fidia ili ujenzi wa daraja hilo uendelee kama ilivyopangwa. Kwa mwendo ulipo sasa na taarifa ya utekelezaji iliyopo Daraja la Kigamboni linatarajiwa kukamilika na kuzinduliwa mwezi Julai 2015, haya ni mafanikio ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania imewasiliana na Taasisi zinazotoa huduma za maji, barabara, simu na umeme ili waweze kupeleka huduma hizo kwenye miradi ile ya ujenzi wa nyumba bora. Kwa sababu ya upatikanaji wa fedha kuwa hauwezi kupatikana kwa kasi ambayo tunaitarajia, mfumo ambao tunataka kuufanya sasa ili miundombinu hii iweze kupatikana na mahali pale paweze kukalika vizuri, tutaendelea kutumia utaratibu wa PPP ili miradi ile ijengwa kwa ubia na tayari Sheria ya Uwekezaji na ya PPP baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma zimeshapitishwa zinaweza kutumika sasa ili miradi hiyo iweze kutekelezeka kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelekezo ambayo tulipewa mahsusni na Kamati, naomba sasa kwa harakaharaka nijikite kwenye hoja mojamoya kama nitazifikia zote namshukuru Mungu lakini zitakazobaki tutatoa majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja zilizotolewa na Kamati ambazo ziliwasilishwa na Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, ambayo ilikuwa inasema Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kitoe elimu kwa umma na kujitangaza zaidi kwa huduma iliyoianzisha ya *One Stop Centre* ili kuhamasisha wawekezaji hasa wazawa waweze kuwekeza kwenye miradi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha huduma kwa wawekezaji, Serikali kupitia TIC tayari ilikwishaanzisha utaratibu wa mfumo huu wa *One Stop Shop*. Mkitembelea kituo kile, mtaona kimekwishaanzisha *One Stop Shop* au wengine wanatumia neno *One Stop Centre*, ukiingia tu pale unaweza kupata huduma pale. Bado kuna mambo ambayo tunaendelea kuyakamilisha lakini tunachotaka kukifanya pale ni kwamba ukitaka huduma ya upatikanaji wa ardhi, mambo ya *immigration, TRA*, maafisa ambao ni *authorized* wanakupa huduma hiyo palepale ndani ya kituo badala ya kukwambia uende kwenye Wizara zingine zinazohusika na kupoteza muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika kuboresha huduma hizo, mwaka huu 2015, TIC tayari imeanzisha mpango mpya wa kutoa huduma katika *One Stop Shop* kwa njia ya mtandao (*Tanzania Investment Window*) ambapo wawekezaji wanaweza kusajili makampuni, kupata leseni za biashara, kujiunga na mifuko ya kijamii, kujisajili na mamlaka ya mapato (*TIN* na *VAT*) na kufanya malipo kwa mtandao bila kufika katika ofisi za TIC ukiwa ndani na nje ya nchi. Serikali pia imeweka mkakati wa kutangaza mpango huo ambao unahusisha kutoa elimu kwa umma kwa njia ya vyombo vya habari na machapisho mbalimbali. Kupitia tukio la kuzindua rasmi huduma hii, kazi hii itaanza mwezi Julai, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine ambayo ilitolewa pia na Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, ambayo inasema kituo hiki cha TIC kiweke masharti kwa wawekezaji wanapokuja hapa nchini kuwekeza kwa ubia pamoja na wazawa ili tuweze

kunufaika kutokana na miradi hiyo kuliko kuwauzia maeneo ambayo wakiondoka nchi inabaki bila kitu. Sheria ya Uwekezaji Na. 26 ya mwaka 1997 imeweka utaratibu wa Watanzania na wageni kumiliki miradi. Miradi inaweza kumilikiwa kwa ubia baina ya Watanzania na wageni. Ili kunufaisha Watanzania zaidi, Serikali kupitia TIC inawahamasisha wageni kushirikiana na Watanzania kuwekeza kwa njia ya ubia. Kwa mwaka 2014, asilimia 23 ya miradi iliyosajiliwa na TIC inamilikiwa kwa ubia na hii taarifa pia aliitoa Waziri Mkuu. Aidha, uwekezaji katika sekta ya fedha, mawasiliano ya simu, bima, madini, unazitaka kampuni za nje kuwekeza kwa ubia pamoja na Watanzania. Kwa hiyo, huu ndiyo utaratibu ambao tumeweka ili kuhakikisha kwamba Watanzania nao wanamiliki uchumi wao badala ya kuwaachia wageni peke yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilitoka kwa Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul pamoja na Wabunge wengine ikisema, Serikali ilete Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji nchini ili kurekebisha kipengele kinachohusu kima cha chini cha mtaji kwa kupunguza kima hicho ili Watanzania walio wengi waweze kuwa na sifa ya kuwa wawekezaji katika nchi yao katika miradi mbalimbali. Majibu yake ni kwamba kiwango cha mtaji wa dola za Marekani 100,000 kilichowekwa kwa wawekezaji wa ndani huwekezwa kwa awamu kwa kipindi cha miaka mitano yaani mwekezaji wa ndani amewekwa kiwango hicho lakini halazimishwi kulipa chote kwa mara moja. Anaweza kulipa kwa awamu katika kipindi cha miaka mitano cha utekelezaji wa mradi husika. Mwekezaji wa ndani pia anaweza kuanza na kiwango chini ya kiasi hicho. Kwa hiyo, utaona kwamba bado tumewapendelea wenzetu wawekezaji wa ndani na siyo kweli kwa dhana ile iliyopo kwamba tunakumbatia wawekezaji wa nje kwa kiasi kikubwa, hapana! Tumeweka nafasi kabisa kuhakikisha wawekezaji wa ndani nao waweze kushiriki. Utakuta kwamba hizi *flexibilities* huwezi kuzipata unapokuja kuangalia zile *conditions* ambazo tumewepa wale wawekezaji wa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa pia imetoka kwa Mheshimiwa Pauline Gekul, Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji), ikisema Serikali ieleze ni jinsi gani Kituo cha Uwekezaji Tanzania kinaratibu shughuli za wawekezaji kutoka nje. Kwa hivi sasa kuna wimbi kubwa la wageni wanafanya biashara ndogo ndogo nchini ambazo zingeweza kufanywa na wazawa. Naomba hapa tuelewane kidogo. Kuna tofauti kati ya wafanyabiashara wadogo wadogo na wawekezaji. Kuna *investors* na *traders* na watu walio wengi hapo wanachanganya. Wakikuta wageni, maana wengine wanasema kuna Wachina, Wahindi wanafanya biashara ndogo ndogo ambazo zingekuwa ni za wazawa na wanathubutu kusema hawa ni wawekezaji. Hii ni *misconception* tu. Hawa siyo wawekezaji, ni wafanyabiashara tena ni wachuuzi. Mwekezaji halisi akifanya *investment* hawezi kuanza kupata matokeo yake hapo hapo siyo kwamba biashara yake mapato yake ni jioni, ndiyo maana wanaomba hata *tax holiday* maana aki-*invest* anahitaji miaka mingi kabla hata hajaanza kupata matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wafanyakazi wageni wanaofanya kazi nchini wanaingia kupitia njia mbalimbali ikiwemo miradi inayoandikishwa na TIC kwa ajili ya uwekezaji. Wapo pia wanaokuja nchini kufanya kazi kwenye kampuni zinazohusiana na biashara au *trading* na ndiyo hao wadogo wadogo wanaozungumzwa. Hivyo kwa wale wanaokuja kwa ajili ya uwekezaji kupitia Sheria ya Uwekezaji, idadi inayoruhusiwa kisheria ni watano. Yaani mwekezaji akija nchini kuwekeza sheria inamruhusu moja kwa moja kuja na wataalam watano. Anaweza kuongeza akiweza ku-*justify* na sisi tukakaa katika vikao vyetu vya NISC tukaona kwamba kweli huyu anastahili. Kwa kawaida sheria inatambua watano kwa kila mradi ingawa kwa baadhi ya miradi michache sana wanaweza kuajiri zaidi ya watano kulingana na mahitaji yake hasa pale ambapo wataalam wanaohitajika hawawezi kupatikana ndani ya nchi. Hivyo, Kituo cha TIC hakishughulikii vibali vya kazi kwa wageni wanaokuja kufanya biashara ndogondogo, bali inashughulikia wale wawekezaji mahiri tu ambao ndiyo hao nilieleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine inasema Serikali itoe ufafanuzi kuhusu mwingiliano uliopo wa kazi za Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara za kisekta kwenye masuala ya uwekezaji. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu huratibu shughuli za uwekezaji nchini zinazohusisha miradi mikubwa inayoshirikisha sekta zaidi ya moja. Kwa mfano, uratibu wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ambayo inahusisha Wizara ya Fedha, Katiba na Sheria, Ujenzi, Viwanda na Biashara, Uchukuzi, Maji na Wizara ya Nishati na Madini. Aidha, miradi yote ya uwekezaji ikiwemo miradi mikubwa na ile ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi huibuliwa na kutekelezwa na Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja inasema Ofisi ya Waziri Mkuu inasimamia mifuko 13 ya uwezeshaji, hamna mantiki ya kusimamia mifuko hiyo wakati kuna mifuko inayotoa huduma kama hizo kupitia Wizara za Serikali. Naomba nitumie muda kidogo kwa sababu naona kuna haja ya kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo mifuko 13 ambayo yote ni ya uwezeshaji na yote hii inawahudumia wananchi na mingi iko katika Wizara nyingine za kisekta. Sasa naomba niseme kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo mratibu wa shughuli zote za Serikali nchini. Mifuko hii ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi ilianzishwa kisheria na inatekelezwa na Wizara mbalimbali za kisekta. Ofisi ya Waziri Mkuu inaratibu mifuko hiyo ili kuhakikisha inatimiza malengo ya kuanzishwa kwake na kuwezesha wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitaje Mifuko ambayo tunayo iko kama 13 na nafikiri ninaweza kuifikia yote. Mifuko ya Uwezeshaji iko 13 na kati ya hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu inasimamia mfuko mmoja tu yaani *Mwananchi Empowerment Fund*. Mifuko hiyo na Wizara ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi, huu uko Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi na unaratibiwa moja kwa moja na Ofisi ya Waziri Mkuu;
- (ii) Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao unaratibiwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo;
- (iii) Mfuko wa *Small Entrepreneur Loan Facility (SELF)*, huu uko chini ya Wizara ya Fedha;
- (iv) Mfuko wa *National Entrepreneur Development Fund*, huu unaratibiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara;
- (v) Mfuko wa Pembejeo, *Agricultural Inputs Trust Fund*. Huu mmeuzoea na uko chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika;
- (vi) Mfuko wa *Presidential Trust Fund* na huu unaratibiwa na Ofisi ya Rais;
- (vii) Mfuko wani *Rural Energy Development Fund (REA)*, huu uko chini ya Wizara ya Nishati na Madini;
- (viii) Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, huu uko Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto;
- (ix) Mfuko wa *Export Guarantee Scheme*, huu uko Wizara ya Fedha;

(x) Mfuko wa *Small and Medium Enterprises Guarantee Scheme*, huu uko chini ya Wizara ya Fedha;

(xi) Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Wanawake katika sekta isiyo rasmi na huu uko chini ya Wizara ya Kazi na Ajira;

(xii) Mfuko wa *Tanzania Social Action Fund (TASAF)*, huu uko chini ya Ofisi ya Rais; na

(xiii) Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira, alimaarufu Mabilioni ya Kikwete, huu unaratibiwa na Benki Kuu ya Tanzania (*BOT*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo mifuko ambayo iko katika sekta mbalimbali na Ofisi ya Waziri Mkuu inaratibu mifuko hii kuhakikisha kwamba mambo hayaendi vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa Serikali iondoe urasimu kwa baadhi ya taasisi zake zinazohusika na masuala ya uwekezaji. Hili nimeishalitolea majibu kwa kueleza kwamba tayari *TIC* imeanzisha kituo cha *One Stop Shop* ambacho kinatoa huduma zote hizi. Hii ni kwa ajili ya kupunguza adha za wawekezaji na wote wanaotaka kupata huduma ili wasilazimike kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda huu nilionao, nilisikia kengele ya kwanza imegonga lakini liko jambo moja ambalo nafikiri nitakuwa sijalitendea haki nisipolieleza vizuri hapa. Ipo hoja ambayo inasema Serikali ilipatie fedha za kutosha Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili liweze kuratibu vizuri suala la uwezeshaji wananchi wote hasa wanawake, vijana na makundi mengine. Sambamba na hilo, Serikali iharakishe Kamati za Uwezeshaji Wananchi kiuchumi zinazoundwa na ngazi zote kuanzia familia hadi Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilipokuwa najibu swali niliweza kutoa majibu lakini naomba niongezee kwamba Serikali itaendelea kulitengea fedha Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kadri uwezo wa fedha wa Serikali utakapokuwa unaimarika. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kichumi limetengewa jumla ya shilingi bilioni 3.5, kati ya hizo shilingi bilioni 1 ni kwa ajili ya maendeleo ya kuwezesha wananchi kiuchumi. Hapa kwa namna ya pekee naomba nitoe hongera na sifa za kipekee kwa *VICOBA* na hususan kwa Mheshimiwa Likokola kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kuwezesha vikundi 23,000, wanachama 700,000 na hivi sasa wana mtaji wa takribani shilingi bilioni 86. Mlimsikia mwenyewe akisema sasa tuanze kufikiria hawa watu waanzishe benki badala ya kuendelea kuitwa *VICOBA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kusaidia watu wa namna hii. Namuomba Mheshimiwa Likokola ambaye ndiye *champion* wa *VICOBA* aendelee, tuko pamoja naye na wengine wote ambao wanakwenda kwa mtindo huu tutaendelea kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa inasema Serikali ihakikishe Kamati za Uwezeshaji Wananchi kiuchumi zinaundwa katika ngazi zote kuanzia ngazi ya familia hadi Taifa. Serikali imeanza kuratibu utaratibu na mchakato wa kuunda Kamati za uwezeshaji wananchi kiuchumi nchini. Mwongozo tayari umetayarishwa ambao unapendekeza kuundwa kwa Kamati hizi katika ngazi ya kitaifa, kisekta, kimkoa, wilaya, kitarafa na ngazi ya kijiji na hapa Mheshimiwa Likokola alikuwa ameulizia swali jana. Muundo wa Kamati umeelezwa vizuri kwenye mwongozo. Vilevile Mwongozo unaelekeza kuundwa kwa Madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambapo Madawati haya yatakuwa yanasimamia utekelezaji wa kila siku wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Mwongozo unaelekeza Kamati kukutana kila robo mwaka. Mwongozo huu tayari umeishawasilishwa kwenye mkutano wa wadau ambapo maoni ya

kuboresha yamepokelewa. Baada ya marekebisho, Mwongozo utatolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Waraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kulikuwa na hoja nyingine inasema Serikali itekeleze miradi mingine kwa njia ya PPP ili kuondoa tatizo la upungufu wa fedha za Serikali. Hili niliishalieleza kwamba ili kuongeza uwezo wa kifedha au kupunguza mzigo wa kifedha wa Serikali, tayari Serikali na Bunge hili liliishapitisha Sheria ya PPP na tuna miradi ambayo tayari imeishaanzishwa kwa ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitaje miradi mitatu tu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Muda umekwisha, miradi hiyo mitatu utaiandika. *(Kicheko)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI): Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo nitaiandika kwa maandishi. Naunga mkono hoja, asanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, shughuli zote zilizopangwa leo zimekwisha, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

(Saa 1.54 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 16 Mei, 2015 Saa Tatu Subuhi)